

‘MWINGILIANO WA FANI NA MAUDHUI KATIKA USHAIRI WA KITHAKA WA
MBERIA’

MWASILISHI: PERMENUS KASILU NZUKI

GARY AFRICANA COLLECTION


TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.



SEPTEMBER, 2003


UNGAMO

“Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa mahali
popote kwa mahitaji ya shahada ya aina yoyote ile”



Permenus Kasilu Nzuki
(Mtahiniwa)

“Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama
wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu”.



Bw. Timothy Arege



Dkt Rayya Timammy

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia binti yangu mpendwa Joan Mbiviu

Kipenzi johari yangu, binti mwana adibu,
Kuna dunia na mbingu, zin'okutaka wajibu,
Utende lis'o machungu, ulekele kwa Rajabu,
Hilo lichukue kwangu, litwae litakutibu,
Soma durusu vitabu, huo ndo wasia wangu.

YALIYOMO

UKURASA

UNGAMO.....	i
TABARUKU.....	ii
SHUKRANI.....	iii
DIBAJI.....	iv
YALIYOMO.....	v

SURA YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI.....	1
1.2 TATIZO LA UTAFITI.....	5
1.3 MADHUMUNI YA TASNIFU.....	5
1.4 UPEO NA MIPAKA.....	5
1.5 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO.....	6
1.6 NADHARIA TETE.....	7
1.7 UDURUSU WA KAZI NYINGINE.....	7
1.8 MSINGI WA KINADHARIA.....	9
1.8.1 NADHARIA YA UMUUNDO.....	9
1.8.2 NADHARIA YA KISOSHOLOJIA.....	12
1.9 NJIA ZA UTAFITI.....	14

SURA YA PILI

USHAIRI HURU WA KISWAHILI.....	15
2.1 UTANGULIZI.....	15
2.2 USHAIRI WA KISWAHILI KABLA YA USHAIRI HURU.....	18
2.3 USULI NA MAENDELEO YA USHAIRI HURU KATIKA KISWAHILI.....	23

2.3.1 HATUA ZA MAENDELEO YAKE.....	26
2.4 VIGEZO VIKUU KATIKA USHAIRI HURU.....	29
2.5 SWALA LA MGOGORO WA USHAIRI.....	32
2.6 ULINGANISHAJI KIHISTORIA WA USHAIRI HURU NA ULE WA KIMAPOKEO....	38
2.7 HITIMISHO.....	41
 SURA YA TATU	
 MATUMIZI YA MBINU ZA LUGHA KATIKA KUJENGA MAUDHUI.....	42
3.1 UTANGULIZI.....	42
3.2. SIASA.....	45
3.2.1. TASHBIHA.....	48
3.2.2. TASHIHISI.....	50
3.2.3. SITIARI.....	52
3.2.4. TAASHIRA.....	53
3.2.5. MASWALI YA BALAGHA.....	54
3.2.6. TAKRIRI.....	56
3.2.7. MSISITIZO BAYANI.....	58
3.3 MAZINGIRA.....	60
3.3.1. TASHIHISI.....	61
3.3.2. TASWIRA.....	63
3.3.3. USAMBAMBA.....	64
3.3.4. MSISITIZO BAYANI.....	66
3.4 UTAMADUNI.....	67
3.4.1. TAKRIRI.....	68
3.4.2. UHUISHI.....	69
3.4.3. USAMBAMBA.....	70
3.4.4. SITIARI.....	72

3.5 DHULUMA YA KIMAPENZI.....	73
3.5.1. TASHBIHA.....	74
3.5.2. TASHIHISI.....	75
3.5.3. TASWIRA.....	77
3.6 HITIMISHO.....	78

SURA YA NNE

SITIARI ZA KIMCHORO NA VIPENGELE VYA KIFANI.....	80
4.1 UTANGULIZI.....	80
4.2 SITIARI ZA KIMCHORO.....	80
4.3 MANDHARI.....	86
4.4 TONI.....	92
4.5 HITIMISHO	98

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	100
5.1 HITIMISHO.....	100
5.2 MAPENDEKEZO.....	102
MAREJELEO.....	104

SHUKRANI

Katika kiumba kazi hii wapo watu wengi walionishika mkono. Ningependa kuwataja na kuwashukuru baadhi yao tu kwa sababu ni wengi mno.

Kwanza kabisa ningependa kuwarudishia shukrani furifuri wasimamizi wangu; Daktari Rayya Timammy na Timothy Arege. Hawa wamekuwa mhimili wangu mkuu katika safari hii ndefu. Kwao, Mungu awazidishie rehema zake.

Napenda pia kuwashukuru kwa dhati wahadhiri wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika ambao walinipa maarifa ashirafu. Hao ni kama vile Dkt Kineene wa Mutiso, Dkt Mwenda Mbatia, Dkt Kyallo Wamitila, Dkt John Hamu Habwe, Dkt Alfred Buregeya, Richard Mgullu, Ayubu Mukhwana, Basilio Mungania, James Michira, Francis Musyoka, Profesa Mohamed Abdulaziz pamoja na mwenyekiti wa Idara Dkt Kithaka wa Mberia. Nilifaidi sana maarifa yao. Kwao, Mungu awazidishie maarifa.

Hali kadhalika nawashukuru sana wanafunzi wenzangu ambao daima tulisaidiana kimasomo. Hao ni kama vile: Elizabeth Auma Ocholla, Prisca Jerono, Mogere Osoro, Timothy Bwire, Kirera Mutugi, Akeya Magare, Mukoma Kamau, Adziaya Amadi. Hawa tulishiriki pamoja mijadala iliyokuwa changa moto muhimu kiusomi. Walinifaa pengi pia kwa mashauri ya kimaisha. Nawaombea ufanisi maishani.

Sina budi kuwashukuru wazazi wangu walionilea na kunisomesha pengi. Hawa ni babangu mpendwa Bw. Michael Nzuki Kimaa na mama mpenzi Sabina Mbiviu Nzuki. Nyie ndio jicho langu la kwanza. Mungu awaweke imara.

Na kwa bibi yangu muhebi, Priscah Muli, Mungu akupe raha siku za maisha yako yote. Wewe ulivumilia nyakati ngumu nikiwa masomoni. Nitakupenda daima.

Hatimaye namrudishia Shukrani Bw. Samuel Ng'ang'a aliyenitayarishia kazi hii katika tarakilishi.

Kwenu nyote, nawaombea baraka za Bwana. Mungu na awakirimu mema yote mtakayomuomba.

Sitahasahu kukishukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa ufadhili wa kimasomo kilionitunukia.

Moyo huo na ludumu.

DIBAJI

Tasniifu hii ni uchanganuzi wa vipengele vya fani na maudhui katika diwani za Mchezo wa karata (1997) na Bara Jingine (2001). Inachunguza kuchangiana kwa vipengele hivi katika kiumba kazi nzima. Tumeainisha maudhui manne makuu yanayojitokeza na kuonyesha mchango wa vipengele vya kifani katika kuyajenga.

Baada ya kutoa malengo yetu, na kuweka wazi nadharia zitakazotuongoza katika uhakiki wetu, tumedurusu kazi mbali mbali zinazoufaa uchanganuzi wetu. Haya yote ni katika sura ya kwanza.

Sura ya pili imeweka msingi wa kuuelewa ushairi wa Kiswahili, kihistoria kufikia kuzuka kwa ushairi huru. Tumeonyesha humo fasili na nafasi ya ushairi huu kiulinganishi.

Katika sura ya tatu, tumeyashughulikia maudhui yaliyomo pamoja na mbinu mbali mbali za lugha zinazotumiwa kuyaendeleza. Tumeziangalia mbinu hizo kama vijenzi vya maana na mbinu za kujengea taswira za kisanaa.

Hali kadhalika tumechunguza, katika sura ya nne, mbinu nyingine za kifani za ziada ya lugha na kuonyesha jinsi zilivyosaidia katika ujenzi wa maudhui. Tumeainisha matumizi ya sitiari ya kimchoro katika diwani hizi. Pamoja na kuchunguza kifupi usuli na maana yake, tumeonyesha mchango wa mbinu hii katika kuyajenga maudhui. Tumetathmini humo humo nafasi ya mandhari na toni katika kuyaibua maudhui. Tumeonyesha jinsi vipengele hivi vinavyochangiana na kukamilishana katika ukuzaji wa fahiwa za kifasihi. Tumeeleza pia umuhimu wa vipengele vya lugha katika kuvikuza vipengele hivi vya hatua ya pili ya fani (visivyojonyesha moja kwa moja kivyake).

Hatimaye tumetoa hitimisho letu katika sura ya tano. Katika sura hii tumeonyesha kwa muhtasari sifa kuu na bainifu za kisanii zinazojitokeza katika diwani zenyewe na kusaidia katika ujenzi wa maudhui. Tumezitolea hukumu na mapendekezo yetu. Hukumu yetu imeangaza uthabiti na udhaifu tulioweza kugundua katika tungo zenyewe.

SURA YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI

Katika fasihi ya Kiswahili, ushairi huru unahusishwa na juhudi zilizoanzia miaka ya sitini ya karne ya ishirini za kuutoa ushairi kwenye 'ufunge' wa vina na mizani. Ukiushi huu kutoka kaida za kimapokeo umehushishwa hasa Chuo cha Tanzania cha Ushairi (Tanzania School of Poetry). Huku baadhi ya wasomi wakikadiria utalakiano huu kuwa wa karibuni zaidi, wengine huamini kuwa mwanzilishi wa mkabala huu ni marehemu Shaaban Robert kwa tungo zake za miaka ya nyuma, hata miaka ya hamsini ya karne hiyo. Yeye anadaiwa kukiuka ushairi wa Kirasimu wa wakati wake, ule wa kitarbia, kwa jaribio la kuufufua ushairi wa nyakati za nyuma zaidi, na kwa jinsi alivyotokea na mashairi ya mikondo anuwai isiyozoleka wakati ule. Haya ni kwa mujibu wa Kazungu (1988).

Ushairi huru umeweza kufasiliwa kama ushairi ambao ni kiushi dhidi ya kanuni za kimapokeo za utunzi, huku baadhi ya wanamapokeo sugu wakikataa kuukubali kamwe kuwa ni ushairi. Umetokea kubandikwa majina kama vile: mapingiti, mavue, masivina , ushairi wa kimapinduzi, ushairi wa kisasa, mionganoni mwa mengine.

Waandishi mbali mbali wametoa fasili anuwai kuuhusu ushairi huru. Akitoa kijilezi chake, kuuhusu ushairi huru, H.E. Lambert (1946) anasema kuwa:

Mashairi huru huwa ni mkusanyiko wa tungo zenye anuwai za ufundi wa kuzisana,

Anaeleza kuwa ni mashairi ambayo hayagawiki katika mikondo naye J. Kitsao (1982: 36) anayaeleza mashairi huru kuwa ambayo hukwepa kabisa kaida za kimapokeo za utunzi. Anavyoonelea, mashairi haya huhisika kuwa ya kinathari lakini yaliyo katika umbo la kishairi.

T.I.M. Arege (1998) anautaja ushairi huru kuwa:

...ambao haifuati kanuni za kijadi katika utunzi wake. (uk.1)

Naye R. Diyanni (1994) akieleza maanzili ya utukiaji wa ushairi huru anasema kuwa ulitokea kama kibadala cha ufunge wa umbo, na kwamba ni wenyewe maumbo legevu, yaliyo wazi na huru zaidi. Lakini anatahadharisha kuwa umbo wazi au legevu halimaanishi ukosefu wa umbo. Yeye anaeleza kwamba uibukaji wake ni mwendelezo wa uhuru wa kishairi tu unaowalinda washairi dhidi ya ufunge banifu.

Kwa hiyo, waandishi wameuona ushairi huru kama anuwai ya ushairi tu ambao unadhamini zaidi uhuru wa mtunzi, na kwamba huitumia fani tofauti na ule wa kijadi katika kuyaeleza mawazo mbali mbali.

A.Mazrui (1988) hata hivyo, anayapa sifa ya ziada kuyapiku yale ya kimapokeo. Katika utangulizi wa Chembe cha Moyo, anasema kuwa mashairi huru ni yale yasiyofuata mizani, vina wala vituo, na kuwa:

Mashairi haya mapya yamejengeka vizuri zaidi katika maudhui yake kuliko ya kimapokeo.

Kauli yake hii inaoana na mawazo ya baadhi ya washairi huru kuwa ushairi huru ni makinifu zaidi na ushughulika na maswala nyeti zaidi kuliko ushairi wa kijadi. Hili ni swala la mjadala.

K. Wamitila (2002) anatahadharisha kuwa mashairi huru si kwamba hayana sifa maalum ya kuyatambulisha lakini ni yenyewe uanuwai wa mbinu. Anaeleza kuwa badala ya kutegemea mizani kuzua wizani, haya hutegemea mbinu zingine kama vile mpangilio wa sentensi, unyumbuaji maneno, mpangilio wa maneno, muundo wa beti, kuzulia hisia nzito katika utungo wa kishairi (uk.95)

Kwa hiyo, kwa mujibu wa maoni yake, hivi ndivyo vipengele vyta kimsingi katika kuutambulisha. Aghalabu mipangilio yake anuwai uzua utata katika kuzitenga sifa zake mahususi.

Katika miaka ya nyuma M. A. Berthon (1924) kama anavyonukuliwa na Preminger (1979)

aliueleza ushairi huru (vers Libres) miongoni mwa watungaji wa Kifaransa kwa kusema kuwa:

Shairi litasemwa kuwa limeandikwa kwa mkondo wa huru wakati linapo jumuisha mistari yenyeye idadi yoyote ya silabi, iliyo changanya apendavyo mshairi na bila mpangilio nazo tungo za aina hii si duni kamwe na uhitaji ujuzi mahsusini wa ridhimu,sikio makinifu, na zinaweza kushughulikiwa kwa ufanisi na mtu mahiri tu.

Kijelezi chake hiki kinaegemea zaidi upande wa fani, na hasa mpangilio na umbo la shairi kama kipengele muhimu kuutambulisha ushairi huu. Anakariri umuhimu wa makini katika kushughulikia fani katika ushairi huru, kwani fani ndicho kipashio kinachobeba fahiwa inayolengwa.

Kuhusu fani katika ushairi F.E.M.K. Senkoro (1982) ametoa mawazo ya wataalamu kadha wa kimagharibi. Kwa mujibu wake, Valery, mwana fasihi na mwana nadharia wa Kifaransa, ambaye alionyesha kupendelea zaidi fani kuliko maudhui, anadai kuwa:

...maudhui si kitu kingine zaidi ya fani chafu yaani fani iliyochanganyikana... fani daima hutawala Fikra huwa nyenzo tu wala si mwisho wa usawirishaji (uk.85).

Kwake yeye fani aghalabu ndiyo huzua maudhui, na kwa hiyo ndicho kipengele cha msingi katika kulishughulikia shairi, au utungo wa kifasihi yeye anaonyesha, hata hivyo, ugumu wa kuyatenganisha maudhui na fani. Anaelekea kukuza wazo kwamba mawazo ya akilini mwa mtunzi hutegemea ufundi fulani katika kuyawasilisha, na hii ndiyo fani.

Cleanth Brookes, mhakiki wa Kimarekani, anyenukuliwa na Senkoro pia anaiangalia fani na kupendeketekeza uchambuzi wa kazi kiimuundo huku akipinga hali ya kulijadili shairi kinathari katika kujaribu kutoa maana yake. Huyu anaelekea kuenzi mkabala kuwa viungo mbali mbali vya kifani huwa na dhima yake mahususi katika kuupitisha ujumbe, na hivyo ubidi kuchunguzwa ili kuona mchango wake katika mtungo mzima.

Baada ya kupata mawazo ya wataalamu kadha Senkoro anataja kuwa

Badala ya kutumia istilahi ‘fani’ iletayo maana ya umbo la nje, afadhali kutumia ‘muundo’ ambalo uhusisha unje na undani wa kazi ya fasihi. (Uk.87).

Upana wa maelezo haya unatufikisha kwenye muoano wa umbo na yaliyomo.

Inaelekea kuwa watunzi wengi waliohusishwa nao wameathiriwa na usomaji wa mashairi ya kimagharibi. Hawa husisitiza kuwa ni hatua ya kimaendeleo katika utanzu wa ushairi, kwani kitu chochote kile huishi,kukua na kubadilika. Huonelea kuwa kilicho muhimu katika shairi si vina na mizani tu bali muundo wa shairi, umuziki wake, pamoja na upitishaji wa mawazo kwa lugha ya kimkato, iliyofupika.Wanachojali zaidi ni matumizi ya kirazini ya picha na taswira.

Miongoni mwao ni pamoja na: E.Kezilahabi:Kichomi (1974) na Karibu Ndani (1988); K.K. Kahigi na M.M Mulokozi: Mashairi ya Kisasa(1973), Malenga wa Bara (1976) na Kunga za Ushairi na Diwani yetu (1979); A.Mazrui: Chembe cha Moyo (1988); K.Mutiso: Mizani Yangu(1986); K.Mberia: Mchezo wa Karata (1997) na Bara Jingine (2001).Hawa ni watunzi waliopata elimu ya vyuo vikuu pamoja na tajriba pana ya utunzi wa kilimwengu kinyume na wengi wa wanamapokeo walioelekezwa na ilhamu na mwito wa kiungu. Wengi wa washairi huru pia wameweza kutunga wakifuata kanuni na arudhi za kijadi.

Kazi za Mberia: Mchezo wa Karata na Bara Jingine ni mionganii mwa diwani za hivi karibuni kabisa zenyenye kufuata mkondo huu. Pamoja na kuonyesha mpangilio unaoenzi ushairi huru, kazi hizi zimepiga hatua zaidi ya kutumia maumbo ya kimchoro, jambo ambalo ni geni katika ushairi wa Kiswahili.

1.2 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo la utafiti wetu ni uhakiki wa jinsi vipengele vya fani na maudhui vinavyochangiana katika diwani za Kithaka wa Mberia: Mchezo wa karata (1997) na Bara jingine (2001). Shughuli yetu ni kuonyesha mwingiliano wa vipengele hivi viwili vya fasihi, fani na maudhui katika kuupitisha ujumbe katika diwani hizi.

Baadhi ya wanamapokeo wanasema kuwa ushairi huru ni mkorogano wa maneno usiofikia hadhi ya kuitwa ushairi. Hali kadhalika kuna wanaodai kuwa michoro haichangii kuleta maana katika ushairi na kuwa haina mchango katika kuzua ujumi. Utafiti wetu umelengwa kuchunguza madai haya.

1.3 MADHUMUNI YA TASNIFU

Tumelenga kuchunguza mchango wa jamii katika kuathiri maudhui na fani anayotumia mtunzi Pili, tutaainisha jinsi vipengele vya kifani vinavyochangiana katika kupitishia maudhui katika diwani hizi.

Tatu, tutachunguza nafasi ya sitiari za kimchoro katika ushairi wa Kiswahili.

Tunauia pia, kuhimili msingi wa utafiti wa tungo zenyenye mwelekeo huru na hivyo kuchocha zaidi uchunguzi wa aina hii katika ushairi wa Kiswahili. Hili litapewa uthabiti kupitia mapendeleko pamoja na hukumu tutakazotoa hatimaye.

1.4 UPEO NA MIPAKA

Utafiti wetu tutaukita kwenye uchanganuzi, wa kifani na maudhui, wa diwani za mshairi Kithaka wa Mberia: Mchezo wa Karata (1997) na Bara Jingine (2001). Tutaangalia mwingiliano wa vipengele mbali mbali vya kifani na maudhui katika kupima uwajibikaji wa

vipengele hivyo. Tutatathmini pia mchango wa mazingira ya kijamii katika kuvikuza vipengele hivi.

Kimsingi, tutatathmini jinsi vipengele vya kifani vinavyochangiana katika kuyakuza maudhui. Tutachunguza pia mshabaha wa maudhui na mazingira ya kijamii. Uhakiki huu utafanywa kwa kuzinasibisha diwani hizi na ushairi huru. Japo kazi zingine zitapitiwa, tathmini kuzihusu hazitatolewa humu. Mifano ya kwingineko italengwa tu kuhimili tathmini ya Mchezo wa Karata na Bara Jingine. Mifano hiyo itatumwa pale tu inapolazimu, kusudi isipotoshe malengo yetu.

1.5 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO

Kuzuka kwa ushairi huru katika ushairi wa Kiswahili ni tukio maarufu katika maendeleo ya utanze huu wa fasihi. Tumevutiwa na maendeleo ya haraka yanayoshika kani katika ushairi huu mpya ambao umezua mvutano mkali miongoni mwa washairi wa Kiswahili.

Fani na maudhui ndivyo vipengele vya kimsingi katika kazi yoyote ya kifasihi. Tumehiari kuvitumia katika kufanikisha uchanganuzi utakaozionyesha kwa uwazi, diwani hizi kama za kishairi huru.

Tumezichagua diwani hizi mbili, kwa sababu ni za hivi karibuni na kwamba hazijashughulikiwa kwa kina na wahakiki. Pia diwani zenyewe zina namna ngeni ya utunzi wa mashairi inayotumia sitiari za kimchoro. Hivyo tumeona haja ya kutathmini nafasi ya mbinu hii katika ushairi wa Kiswahili.

Kazi za kihakiki za awali hazijashughulikia fani katika ushairi huru kwa mapana. Kwa hivyo pamekuwa na pengo nyeti la kiusomi katika uwanda huu. Hii ni changamoto iliyotuvutia kusudi tuchangie kiziba pengo hilo katika ulimwengu wa kiusomi. Kwa kufanya hivi tunatarajia kuwa tumechangia ukuaji wa mtalaa huu.

1.6 NADHARIA TETE

Haipothesia zitakazoongoza uhakiki wetu ni kuwa:

Uwashilishaji fasaha wa maudhui hutegemea sana uteuzi na mpangilio wa vipengele nya kifani pamoja na maingiliano ya vipengele hivyo katika kuleta maana.

Maudhui yaliyomo yana mshabaha mkubwa na hali ya kijamii na mazingira wakati wa utunzi wa tungo zenyewe.

Sitiari za kimchoro huwa na nafasi katika kudhibiti ujumbe pamoja na kiwango cha umbuji.

Diwani hizi mbili zina mchango mahususi wa kipekee katika kuukuza ushairi huru wa Kiswahili.

1.7 UDURUSU WA KAZI NYINGINE

Diwani hizi za Mberia ni za hivi majuzi tu na hazijashughulikiwa kwa kiwango chochote makinifu mbeleni. Hata hivyo zimegusiwa kwa ufinyu hapa na pale kama mifano ya kisasa katika ushairi wa Kiswahili, hasa kuihusu fani na mtindo wake mgeni katika ushairi wa Kiswahili, wa kutumia sitiari za kimchoro.

Hata hivyo, imetuhalisi kupitia kazi anuwai zinazoshughulikia fani katika ushairi, hasa ushairi huru, ziwe nyenzo na kielekezi cha uhakiki wetu. Tumezipitia nyingi ya kazi hizo na kuchota baadhi ya mawazo yanayotufaa katika kuzihakiki diwani hizi.

Kuyahuusu mashairi ya Mberia, Wamitila (2002:106) anayataja kuwa yenyeye kuonyesha kwa uwazi sifa ya uchimuzi (ukuzaji unaofanya jambo kuvutia), ambao aghalabu husababishwa na ukiushi wa kiisimu kama vile mpangilio usio wa kawaida. Wamitila anasema kwamba huu ushairi wa Mberia unaonyesha sifa ya uchimuzi kupitia matumizi ya sitiari za kimchoro katika

baadhi ya mashairi yake. Anaeleza kuwa katika mashairi huru ya Mberia uchimuzi umeweza kutokezwa kwa njia ya mpangilio wa tungo na miundo yake – hasa yenye michoro.

Wamitila anauita ushairi huu wenye uchimuzi wa matumizi ya sitiari za michoro, kuwa ni “Ushairi–ruwaza” na kuutaja kuwa ni unaopatikana

Katika fasihi ya jamii mbalimbali huko Marekani ya kusini, Uchina, Urusi na hata nchi za Kimashariki (uk 106)

Akieleza ‘uvukaji mipaka’ ya ukiushi wa vina na mizani katika ushairi huru, T.I.M Arege (1998) anautaja ushairi wa Mberia kama uliozusha

.... mbinu nyingine mpya ya kuyaandika mashairi haya (huru) ambapo michoro ilitumika.

Anataja mfano wa shairi ‘Nyumba’ (katika Mchezo wa Karata) kama linalofuata mkondo huu (uk.23). Yeye anayaona mashairi ya Mberia kama yaliyopiga hatua ya ziada katika ukiukaji wa kaida za kutungia kimapokeo.

N.N. Abiud (1998) anayeichanganua diwani ya Mchezo wa Karata kimaudhi anasema kuwa:

... yote katika diwani ya Mchezo wa Karata (1997) ni mashairi huru.... Mtunzi wa diwani hii ameukuza utunzi wa ushairi huru wa Kiswahili kufikia daraja mpya na tofauti na wanamtiririko wale wengine wa ushairi huru wa Kiswahili ...ndiye aliyeanzisha ‘mashairi –picha’ katika ushairi wa kiswahili (uk.49)

Anaeleza ‘mashairi – picha’ kuwa ni mapambo ya uhuru wa kimatindo na kifikra. Yeye anauona kama mwendelezo wa uhuru wa kishairi. Anautaja mtindo huo kuwa unaochangia maudhui kwa kiasi kikubwa. Akiyanukuu mawazo ya mwandishi mwenyewe kuuhusu huu mtindo mpya Abiud anaandika:

‘mashairi –picha’ yameundwa kutohana na muungano wa aina mbili ya sanaa. Sanaa hii ni ya uchoraji kutegemea mpangilio wa maneno na usanifu wa kiufasaha (uk.50)

Kwake yeye, sitiari ya kimchoro katika ushairi, kama kijenzi muhimu cha maana, huwa ni tukio la ujumuishaji wa sanaa tofauti pia. Katika uchangamuzi wake wa kimaudhui, Abiud ameeleza mengi pia kuihusu fani mpya ya ushairi huu. Ameteua mashairi kadha kama mifano yenye upekee wa kifani kutoka diwani ya Mchezo wa Karata. Hata hivyo, Abiud aghalabu alilenga kuyashughulikia maudhui na wala sio fani katika diwani hiyo. Kwa hiyo, hakutoa tathmini ya kutosha kuihusu fani yenywewe.

1.8 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti wetu utaongozwa na mseto wa nadharia mbili: nadharia ya Umuundo, na ile ya kisosholojia. Hii ni kwa sababu tunashughulikia fani pamoja na maudhui. Katika kuweka wazi nafasi ya vipengele vya kifani katika kutoa maana tutatumia nadharia ya Umuundo kama kielekezi chetu. Nadharia ya kisosholojia itatuongoza kuchanganulia maudhui. Nadharia zote zitatumika kwa pamoja.

1.8.1 NADHARIA YA UMUUNDO

Kimsingi nadharia hii ni ya kiisimu na hivyo tunaitumia ‘kianalojia’ katika uhakiki wetu. Tumevitumia vigezo vyake vya kushughulikia isimu ili kutuongoza katika uhakiki wa mchango wa vipengele vya kifani katika kuibua maana.

Uasisi wa nadharia ya Umuundo unahusishwa na mawazo ya Mswisi Ferdinand de Saussure (1857 –1913). Saussure alirithi mtazamo wa kimapokeo kuwa ‘dunia’ imeundwa na vitu huru.

Kwa mujibu wa T. Hawkes (1977), Saussure alisema:

...Lugha ni mkusanyiko wa vitu huru viitwavyo maneno ambavyo
kila kimojawapo kina maana tenge (uk. 19)

(Tafsiri yetu)

Katika kazi yake, 'A Course in General Linguistics' (1974) anaieleza lugha:

... ni mkusanyiko wa faridi zinazoshabihiana na thamani ya hizi
faridi hutegemea mahali pake katika mfumo wenyewe ... (uk. xxi)

(Tafsiri yetu)

Dondoo hizi zinakariri wazo kuwa kazi ya kifasihi hujengwa kwa vipashio mbali mbali, ambavyo kwa pamoja huunda maana nzima. Huu ndio msingi wa nadharia ya Umuundo kwamba matini kamilifu huwa 'mkusanyiko wa elementi mbali mbali jenzi'.

Saussure alitokea na dhana tatu katika kushughulikia uwajibikaji wa mfumo wa lugha: 'langue', 'langage' na parole, Aliieleza 'langue' kuwa mfumo dhahania wa lugha ambao hujumisha kanuni ambazo huwepo kuongozwa lugha; ni mfumo -lugha. 'Langage' ni lugha mahususi, ya jamii fulani ya watu, ambayo huwa mego la kanuni za ;'langue'. Nay'o 'parole' aliiona kama mtazamo wa lugha ya kibinafsi ambayo hali ya usawiri wake huamuliwa na kanuni za 'langue'.

Utumiaji wa nadharia ya Umuundo hiziegemea sana dhana za 'langue' na 'Parole'. Katika kuchunguza miundo ya lugha na kanuni za uundaji wake. Hapa, nadharia hii huelekeza kwenye mwingiliano kati ya isimu na fasihi. Upangiliaji wa miundo hiyo hiyo ndio unaoelekea kwenye utoaji wa fahiwa za kifasihi. F.J. Newmeyer (1963) anaandika kuwa:

... mtazamo wowote ulionuia kuchanganua uwajibikaji wa ndani wa
mfumo huu (langue) ulikuja kuitwa 'isimu - miundo' (uk. 3)

(Tafsiri yetu)

Isimu - miundo ilishughulika na vipengele vya kiisimu, hasa kuhusu sheria za lugha na matumizi yake. Ushughulikiaji wa aina hiyo wa matini hatimaye ulizua nadharia ya Umuundo.

Saussure (1974) anasema:

Kwa kweli, ambacho sasa kinaitwa Umuundo kulizuka wanaanthropolojia;
wahakiki wa kifasihi... walipoona kuwa mifano ya kiisimu ingesaidia katika
kufanikisha walichajaribu kufanya katika mitalaa yao., .(uk. 20)

(Tafsiri yetu)

Uwezekano huo unaipa nafasi nadharia hii katika uchanganuzi wa kifasihi. Hii ni kwa sababu vipengele vya kiisimu, kama vile maneno, ndivyo hutumiwa kuundia maana katika kazi ya kifasihi.

Ni kufuatia uyumbifu wa nadharia ya Urasimu, katika miaka ya sitini, ya karne ya ishirini, ambapo mawazo ya Saussure yalitumiwa kuiasisi nadharia ya Umuundo. Kwa mujibu wa nadharia hii, umbo lolote huwa mkusanyiko wa vipengele bia vinavyochangiana kuliunda.

Nadharia hii huafiki kauli ya kimsingi ya kitafakuri iliyedai kuwa:

Hali ya kila kipashio katika maingiliano ya maazili yoyote haina umuhimu wowote bila ya kuelezw na uhusiano wake na vipashio vingine vinavyojumuishwa katika maanzili hayo (Hawkes, k.h.j: Uk.18)

(Tafsiri yetu)

Kanuni hii inakariri umuhimu wa ‘Ujumuishaji’ ambao hudhaminiwa sana na nadharia ya Umuundo. Ni kwa misingi hiyo ambapo kazi yoyote huchukuliwa kuwa mchango wa vijisehemu mbali mbali vijenzi. Kwa misingi hiyo, kazi ya kifasihi ni mkusanyiko wa kunga mbali mbali za kifasihi pamoja na vipengele anuwai vya kiisimu.

Nadharia hii huthamini umuhimu wa muwala, mkubaliano, pamoja na kuchangiana kwa vipashio katika kujenga kazi nzima. Hapo, nadharia hii hupendekeza utathmini wa kazi ya kifasihi katika ujumla wake, kama mchango wa vipengele anuwai. Ni kwa mujibu wa mkondo huo wa mawazo ambapo beti, vina, mizani, urefu wa shairi, msamiati, vituo huwa vipengele muhimu katika uchanganuzi wa shairi kumuundo.

Tathmini ya vipengele vya kitaashira, kunga anuwai za kifasihi, hupewa nafasi pia, katika uchanganuzi wa kumuundo wa vijenzi vya kazi ya kifasihi. Mkabala huu hukita kwenye mawazo ya Saussure kuhusu ‘kiishara’ na ‘kiashiriwa’ kwamba; kila umbo au tukio huwa ni ishara ya maana fulani. Alidai kuwa umbo au dhana yoyote huwa na kiashiriwa (au maana) chake katika ulimwengu halisi. Kwa misingi hiyo J. Culler (1978) anaeleza kuwa:

Mshairi wa kimuundo atawana kudai kuwa usomaji wa fasihi hujumuisha tendo nyeti la kupangilia kazi, kuisoma kama ishara ya aina fulani na hapo kuipa maana ... shughuli yenyewe ni ile ya kutafsiri maana kapa ambazo huhimili anuwai za maana kamili...(uk.119).

(Tafṣiri yetu)

Kimsingi nadharia hii hupendekeza utathmini wa vipengele vyā kimuundo kwa kuangalia kufaa kwake katika kuisana maana, na sio katika ombwe tu. Kiasilia wanaisimu wa shule ya Isimu ya Prague, kina Levi-Strauss, na Roman Jakobson walipoitanguliza nadharia hii walisisitiza uchanganuzi wa kifasihi uelemee jinsi vipengele na kanuni fulani za kifani zinavyofanya kazi katika kazī ya kifasihi.

Kwa misingi hii, nadharia ya umuundo hujaribu kuweka wazi jinsi taarifu ilivyoundwa kutokana na elementi-jenzi zinazosaidiana katika kujenga maana. Katika fasihi, elementi hizi huwa ni kunga mbali mbali za kifasihi pamoja na vipengele vyā kiisimu.

Hata hivyo, uchanganganuzi wa kimuundo hauthamini ushughulikiaji wa vigezo vilivyo nje ya kazi yenyewe, wala kuihusisha kazi na mtunzi mwenyewe katikauzuaji wa maana. Yenyewe husisitiza ufanuzi wa kazi za kifasihi kuzifasili bali sio kiufasiri. Hii ndiyo sababu tunaiambatanisha na nadharia ya kisosholojia katika kufanikisha uhakiki wetu.

1.8.2 NADHARIA YA KISOSHOLOJIA

Hii ni nadharia ambayo huichukua fasihi kuwa zao au tukio la kijamii. Imenasibishwa na Mfaransa Hippolyte Taine (1828-1893) kama mwasisi wake. Yeye alisisitiza uelewa fika wa mazingira ya kijamii anamotungia msanii ili kuielewa kazi yake.

Msingi wa mawazo ya nadharia hii huonekana katika enzi za urasimu huko Ugiriki na Roma (baina ya 850 K.K. na 1780 B.K) Hawa waliegemeza mawazo yao mengi katika nadharia ya

'mwigo'. Kwa mfano, Plato (katika The Republican) alimtaja mshairi kuwa mwigaji tu wa hali halisi.

Kwa misingi hii, sanaa huonekana kama umithilishaji wa hali fulani ya ulimwengu: umithilishaji wa alichokiona msanii katika mazingira yake. Kwa hivyo, nadharia hii hulenga kuonyesha kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya jamii. Yaani msanii wa kifasihi hutunga kazi ambayo ni kioo cha jitihada za binadamu za kuingiliana na mazingira yake ili kujikimu kimaisha. Kwa hiyo mazingira ya utunzi yana nafasi kubwa katika uchanganuzi wa mkondo huu. Ilivyo, mtunzi huathiriwa na nguvu za kijamii, kisiasa na kiuchumi za jamii anayoiandikia.

Nadharia hii husisitiza kuwa fasihi isiangaliwe kama ya ajili ya fasihi tu, bali inayowiana na hali ya jamii –lengwa. Kwa hiyo uhakiki wa kisosholojia hunua kupima kiwango cha kufaa cha maswala yaliyozuliwa kwa kuangalia umuhimu wake katika jamii inayosawiriwa. Uhakiki wa misingi hii hutathmini kiwango cha ubunifu kwa kuongozwa na misingi ya kihistoria, kuihusu jamii.

E. W.Gachukia (1980:35) anaeleza kuwa nadharia hii hupendekeza:

...kuchukua na kuelewa misingi ya kihistoria, kisosholojia na kisiasa ambavyo mwandishi wa kibunifu ameielemeza kazi yake. Ni vigezo hivi ambavyo huchochea ubunifu

(Tafsiri yetu)

Hivi ni kwamba, nadharia hii hutambua uwepo wa jumuia ya thamani zinazoshikiliwa, pamoja na mandhari ya kitamanduni.

Kimsingi, nadharia hii hulenga kutuo kauli ya kijumla kuhusu mandhari ya kijamii (aina, mazingira, utamaduni, mivutano, utabaka n.k) na umuhimu wake katika kukuzia maudhui.
Hapo hupendekeza:

Uhakiki uwe na dhima ya kifasiri, ambapo mhakiki hujaribu ... kufasiri kazi ya mwandishi kwa hadhira pana, kwa misingi ya mandhari inayohusika ya kijamii. (Gachukia, k. h.j:35)

(Tafsiri yetu)

Kwa kuwa mbinu na kaida za utunzi huzuka na jamii pia, nadharia hii haitaliki kabisa uchunguzi wa kimtindo. Hii ni kwa kuwa, kwa mujibu wa A. Welleck na A. Warren (1994) fasihi (fani na maudhui) inachukulika kuwasasi ya jamii inayotumia lugha kama chombo.

Kauli hii inaimarishwa na mawazo ya Hall (1979:39), anayanukuliwa na Mbatia (1999) kuwa:

“...sosholojia ya fasihi huchukulia kuwa umbo na yaliyomo huenda pamoja”.

Hili humpa mhakiki fursa ya kutoa maoni kuhusu maswala ya mtindo wakati wa kuchunguza yaliyomo.

1.9 NJIA ZA UTAFITI

Katika kutimiza uhakiki wetu tumelenga kudurusu kazi za maktabani zitakazotoa mwongozo bora kuihusu mada yetu. Makala kutoka kwa utandawazi yatapitiwa ili kuifadhili shughuli hii.

Udenguzi makinifu utafanyiwa diwani za Mchezo wa Karata na Bara Jingine katika kuichanganua fani pamoja na maudhui yake.

Tutamhoji pia mwandishi wa diwani hizi pamoja na kujadiliana na wataalamu wengine katika nyanja hii.

SURA YA PILI

USHAIRI HURU WA KISWAHILI

2.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutashughulika kuonyesha suala la ushairi huru katika fasihi ya Kiswahili kwa matazamo wa kihistoria. Tutaulinganisha na ushairi wa kihafidhina wa Kiswahili. Tutafanya hivi kwa kuangalia vigezo vyake vikuu pamoja na utalakiano wake na ushairi wa kijadi. Kwa sababu ya mkabala huo wa kiulinganishi basi, tunataka kuonyesha humu fasili uliopewa ushairi wa Kiswahili kabla ya kuzuka kwa wanamabadiliko. Hatimaye tutatathmini tafsili zilizotolewa na wanamtiririko kuhusu maana ya shairi.

Mojawapo ya fasili za kale kabisa kutolewa kuuhusu ushairi (hasa wa Kiswahili) ni ile ya Shaaban Robert, Kuwa:

Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi...

Shairi ni wimbo mkumbwa na utenzi ni upeo wa ushairi.... Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari.

(Harries, L; 1962:272)

Abedi Kaluta katika utangulizi wa Waadhi wa Ushairi, anashikilia msimamo huo huo kwamba:

Mashairi si kitu kingine ni nyimbo (1964: utangulizi)

Hii inaonyesha kwamba fasiri za mwanzo zilithamini zaidi ule umuziki au uimbikaji wa shairi kuliko hata maudhui. Wazo hili linapigwa mwengo na maelezo ya Mnyampala (1971) ambayo pia yanasisitiza fani: Anandika:

Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Kitu kilicho bora sana....
kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa
urari wa mizani na vina maalum...

(1971:Dibaji)

Fasili hizi zilielekea kusisitiza zaidi jinsi ya kuwasilisha ujumbe. Walienzi hasa suala la vina na mizani ili kuleta mdundo unaogusa hisia za msikilaji, pamoja na lugha ya mkato. Kwa hiyo,

tunaona jinsi ushairi wa enzi hizi ulivyoafiki arudhi za kimapokeo, ilisitisizwa kwamba shairi la kiswahili lilikuwa na umbo lake, ambalo liliongonzwa na vina na mizani. Hali kadhalika, shairi lilitazamiwa kupangika katika beti zinazojitosheleza, yaani uwe na maana kamili bila kutegemea kutoshelezwa na ubeti mwengine. Kaida hizi zilitarajia beti zile kuwa na usawa wa mishororo.

Mbali na fasili hizo zilizokariri kuelezeaka kwa shairi kisheria, wanamabadiliko walitokea kuzua tafsili jumlishi zaidi. Kwa mujibu wa E. Kezilahabi, (Mayoka, 1986)

...Shairi ni tukio, hali au wazo ambalo limeonyeshwa kutokana na upangaji wa maneno fasaha yenye mizani kwa kifupi ili kuonyesha ukweli fulani wa maisha. (uk.2)

Hapa kezilahabi anajumuisha mambo mengi kama vile: muundo, uteuzi, lugha ya mkato pamoja na yaliyomo katika ufasili wa shairi. Fasili hii ina mshabaha na zile zilizotolewa kuuhusu ushairi huru.

Akiutalii ushairi huru, I.H. Evans (1981) anasema kuwa ushairi huru, ambao ni ukiushi dhidi ya uandishi wa kimapokeo wa mashairi, uliambatana na ubadilishaji wa ruwaza sahili za kiusemaj. Kauli hii inapuuza swala la arudhi za kihafidhina.

Preminger (1974) akiuzungumzuia ushairi wa Walt Whitman, ambao ni huru, anasema kuwa ni:

... usioegemea kwenye urudiaji wa lafudhi ya msisitizo kwa ruwaza zinazokadirika bali unaoegemea kwenye upangiliaji usiokuwa na utaratibu wa wizani... wenye mpishano wa virai mahsus, ruwaza za kitaashira n.k (uk. 288)

(Tafsiri yetu)

Anaueleza kuwa ushairi ambao ni aina fulani ya nathari yenye sifa bainifu za kishairi.

Anaeleza:

...popote na wakati wowote kunapopatikana ukosefu wa utaratibu maalum wa ruwaza maarufu za kimpangilio, huo unaweza kitwa ushairi huru. (k.h.j)

Akizungumzia 'vers Libre', M.A. Berthon (1924), anayetajwa na Preminger (k.h.j), anasema:

Shairi litasemwa kuwa limeandikwa kwa mkondo 'huru' wakati linajumuisha mistari ya idadi yoyote ya silabi iliyogawanywa apendavyo mshairi, bila utaratibu.... Si kwamba ni duni likilinganishwa na shairi la kiarudhi... lenyewe huhitaji ujuzi mahsuswi wa ridhimu, sikio makinifu, na unaweza kushughulikiwa kwa ufanisi tu na mtu mahiri. (utangulizi)

(Tafsiri yetu)

Kwa kuegemea tafsili hizi, katika sura hii tutazamia uchunguzi wa shairi huru katika Kiswahili kiusuli, vigezo vyake vikuu huku tukiulinganisha na shairi la kihafidhina.

Tunakiri kuwa kuna tofauti kati ya ushairi huru na ule wa kihafidhina. Hapo tutalenga kuchunguza sababu za kuzuka kwa huu ushairi mpya. Katika kufanya hivyo, inatubidi kuchunguza mawazo ya waandishi mbali mbali kuhusiana na uzukaji wa ushairi huru. Tutatathmini mawazo kama yale ya wanamabadiliko kuwa 'kuzidi kufuata kanuni kongwe ni utumwa', na kwamba ni juhudzi za kijiepusha na huu utumwa zilizouibua ushairi huru.

Kezilahabi aliandika kuwa:

Ushairi wa Kiswahili ulikuwa umefikia uozo:

... kupanga mavina na mapambo bila kujali maana, ndiyo sababu ya kuibuka kwa wanamabadiliko.

(Tuki, 1983:145)

Baadhi ya hawa waandishi wa kisasa wanadai kuwa mabadiliko haya yaliyozuliwa na ushairi huru ni njia ya kuweka hai ushairi, kama vile sanaa zingine, ilivyo lugha yenewe. K. Kahigi na Mulokozi, M, (1976) wanasema kuwa iwapo ushairi utadumishwa ni lazima kuzidi kuvumbua njia mpya za kuuendeleza. Walisisitiza kuwa daima huwa kuna njia bora zaidi kuliko nyingine katika kueleza ~~ukio~~ jipya. Hii ni hatua ya maendeleo katika lugha yenewe.

Kwa hiyo, katika sura hii tutaegemea kutalii mawazo yanayohusisha ushairi huru (huru) na hali ya kimabadiliko ya jamii; kwamba jamii hubadilika kiwakati, na vivyo tamaduni, mapokeo na

amali zake. Hapo tutatathmini jinsi uzukaji wa uzukaji wa ushairi huru ulivytukia kama badiliko la kijamii, kupiga daro ushairi wa kihafidhina.

2.2 USHAIRI WA KISWAHILI KABLA YA USHAIRI HURU

Ushairi wa Kiswahili ulikuwepo hata kabla ya majilio wa Waarabu na hati zao. Kwa hiyo imekuwa vigumu kukisia tarehe ya usuli wake. Wanavyoelekea kukubaliana waaandishi ni kuwa ‘tarehe ya ushairi wa Kiswahili, kama vile lugha yenyewe, ni Uswahilini’. Imedaiwa kuwa ushairi ulikiwepo katika fasihi simulizi ya Waswahili katika nyimbo zao kuhusu kazi na shighuli zingine za kijamii. Hukisiwa kuwa mizani za kivina zinazothaminiwa katika ushairi jadi wa Kiswahili aghalabu zilitokana na mipigo ya zana za kikazi. Kazungu (1982) anaandika kuwa:

Wasomi wanakubaliana kuwa asili ya ushairi wa Kiswahili ni nyimbo zilizoibuka na shughuli za kijamii, kitamaduni na kiuchumi. Wakati halisi ulipoanza haujulikani, (uk. iii)

Naye T. Allen (1971) anasema kuwa ulianza wakati Waswahili wenyewe walipoanza kuwepo. Ruo Kimani Ruo (1983) anayekubaliana na mawazo haya anasema kuwa ushairi wa Kiswahili ultokana na nyimbo za hali ya juu sana zilizofuata kanuni fulani.

Huu mwelekeo wa mkubaliano mionganoni mwa waandishi kuwa ushairi wa Kiswahili una asili yake kwenye nyimbo za kijamii unatushawishi kukubali kuwa' tarehe ya usuli wake haikadiriki. Hii ni kwa kuwa hatuwezi kujuua ni lini wimbo wa kwanza ulipoimbwa mionganoni mwao.

Kijumla, ushairi wa Kiswahili unahushishwa na wakazi wa maeneo ya kaskazini mwa pwani, hasa Amu na Mvita. Washairi hawa walikuwa ni walumbi katika lingo wakifungiana nyama kwa zamu –kabla ya ushairi kuandikwa. Baada ya majilio ya Waarabu kulitokea tafsiri nyingi kujumuisha katika ushairi wa Kiswahili pia. Nyingi zilikuwa tenzi za kidini na wasanifu wa milki na watawala mbambali.

Tunachoweza kukadiria ni tarehe ya haya mashairi yalioandikwa mwanzo, na sio wakati mashairi yalipochipuka uswahalini. Kupitia maandishi ya Kiarabu, tunapata tungo zilizo kongwe zaidi katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa haimaanishi kwamba wakati shairi liliponakiliwa kiamaandishi ndio lilipotungwa. Hii ni kwa sababu kabla ya kuandikwa mashairi yalikuwa sehemu ya fasihi simulizi, yakipitishwa kwa mdomo tu toka kizazi hadi kingine. Kwa mfano, ‘Utenzi wa Liyongo’ (M. Kijumwa) ambao uliandikwa mnamo 1913, unakadiriwa kuwa ulikuwepo karne nyingi za nyuma kiusimulizi.

Kwa mujibu wa Mazrui na Sharif (1976: 65) wanaonukuliwa na Kazungu (1982), umbo halisi la shairi la Kiswahili unaweza kukadiriwa kuanzia karne ya kumi na mbili. Wanaeleza kuwa kabla ya wakati huu ushairi wa Kiswahili haukuwa na umbo lolote maarufu bali uliathiriwa pakumbwa na arudhi za kiarabu hata kufikia usanifu wake wa kiutunzi. Kuathiriwa huku kunaweza kukisiwa kwa kuangalia baadhi ya istilahi zinazotumiwa katika ushairi wa Kiswahili, Kwa mfano neno ‘shairi’ lina asili ya kiarabu lenye maana ya ‘hisi katika moyo’.

Kwa mujibu wa waandishi wengi, tungo za kwanza katika ushairi wa Kiswahili zilikuwa aghalabu ni tenzi zilizotafsiriwa. Mionganoni mwake ni ‘Utenzi wa Tambuka’ (chuo cha herekali ~~uongo; Utungwa na Pate na Burudai~~ 1728 ~~kuhusu vita vya Syifa hawa ya wakilishi~~ –1728) ~~kuimhusu sultani~~ wa Pate, Fumo Kaiti Nabhani; ‘Hamziya’ (1749); ‘Al Inkishafi’ (1810 –1820), ‘Utenzi wa Vita vya Badri’, ‘Kasida ya Burudai’; ‘Takhmisi ya Liyongo’ (1913) n.k

Nyingi ya tenzi hizi zilikuwa aina za tungo ambazo zilikuwa na maudhui ya kidini, wasifu n.k ambazo zilieleza mambo mengi ya kihistoria. Fani yake aghalabu ilijumuisha beti zenye mishororo minne isiyogawika, na bila kibwagizo. Anavyoonelea Wamitila (2002):

Kimtindo zinafanana kwa kutumia formula za fasihi simulizi, formula sawa za utangulizi na mwisho wa utungaji, msuko na mgogoro wa msuko unaokaribiana, matimizi ya kilahaja (hasa Kiamu na Kipate), msamiati mpana wa Kiarabu na unyumbuaji maneno wa kiwango cha juu (uk. 96)

Anasema kuwa zilikuwa tingo ambazo zilitoa habari kwa urefu, kwa ufasaha na hivyo kuzua mvuto mkubwa.

Waandishi wengi humtambua Fumo Liyongo, anayekisiwa kuishi katika karne ya kumi na nne (k 11), kuwa ndiye msingi mkuu wa kuchungumzia historia ya ushairi wa Kiswahili. Yeye anatajwa kama mtunzi maarufu wa nyimbo nyingi zilizoimbwa kwenye ngoma za 'gungu' na 'mwao' zilizofuata mkondo wa kishairi mionganii mwa jamii za pwani. Mashairi yake hata hivyo hayaku hifadhiwa kimaandishi, ila kuna mifano ya tingo za Liyongo kama vile, 'Utenzi wa Mwana ninga'.

Hatimaye, maandishi mengi ya kishairi yajulikanayo ni yale ya Muyaka bin Haji (1776-1840).

Yeye alitunga na kuandika mashairi mengi kama aelezavyo M.H. Abdulazizi (1979):

Bila shaka Muyaka ndiye mtetezi mkuu wa hicho kitengo cha ushairi kiitwacho mashairi. Kazi yake huwakilisha hatua muhimu katika ukuaji wa umbo hili mashuhuri la Kishairi katika Kiswahili. (Utangulizi)

(Tafsiri yetu)

Tingo za Muyaka kama zinavyoorodheshwa na Abdulaziz (1979), pamoja na zile za wafuutilizi wake k.v. Ali Koti, Mohammed Kijumwa, na Hemedi Abdalla huchukuliwa kuwa zilizouwekea ushairi wa Kiswahili urasimi wake. Kutokana na mwelekeo wao wa kulipendelea umbo la Kitarbia, kifikia K.19 tarbia ilikuwa imeshatambuliwa kuwa ndiyo utungo wa kirasimi katika ushairi wa Kiswahili.

Baada ya kina Muyaka (Urasimi wa ushairi wa Kiswahili) kulijiri kipindi cha 'Utasa,' baina ya 1885- 1945. Katika kipindi hiki maandishi machache sana yalitokea kuhifadhiwa. Kezilahabi (Tuki, 1983) anasema kwamba:

Huu... ulikuwa wakati ambao mataifa ya Ulaya yalikuwa yakigawana Afrika, Vile vile wakati wa vita vyua dunia (uk.148)

Katika kipindi hiki, makini ya wasanii iliathiriwa na hali hii ya usumbusu na utatanishi juu ya hali na hatima ya mwfrika. Pwani, ambako ndiko kitovu cha Ushairi wa Kiswahili, ndiko kulikoathirika zaidi na majilio na shughuli za wageni.

Kimaandishi,

...ulikuwa wakati wa kubadilisha hati za maandishi..., (TUKI: k.h.j.)

kutoka Kiarabu hadi zile za Kirumi. Mambo haya yalisitisha ukuaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kwa muda, na hapo baadhi ya kanuni za utihzi wa mashairi zikaanza kupotea. Ni katika kipindi hiki pia ambapo maandishi ya kiriwaya (kinathari) yalianza.

Kimsingi, kipindi cha utasa kiliyumbisha ushairi wa Kiswahili na kuupoteza umahsusii wake katika baadhi ya fani, na hata maudhui yake kuchukua mkondo tofauti. Tungo za kutajika katika kipindi hiki ni kama vile, ‘Utenzi wa Mwanakupona na ‘Takhmis ya Liyongo’ (1913). Kilikuwa kipindi cha kuchanganyikiwa na jinsi ya kuyaendeleza maisha ya kijamii mionganoni mwa Waafrika.

Hatimaye kulizuka kipindi cha ‘urasimu mpya’ baina ya 1945 –1960. Baada ya vita kuu vya pili vya dunia, historia ya ushairi wa Kiswahili ilipata mwelekeo mpya. Kuanzia 1945 kulianzishwa juhudi mpya za kuzifuata kanuni za utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Hii ni kwa mujibu wa tungo za kina Shaaban Robert, Amri Abedi, Khamis Amani (Nyamaume), M. Mnyampala, M.M.Kihere, Abdi Matunga, Ahmed Nassir, Mdanzi Hamasa, Kibwana n.k. Hawa wanahuishwa na juhudi za kuufufua ushairi na kuurudishia sifa yake ya awali.

Mtindo ulioshika sana ni ule wa kitarbia. Hii ni kwa sababu ya uimbikaji wake kwa mahadhi iyozoeleka. Wao waliamini kuwa shairi la Kiswahili liliandikwa kwa kusudi la kuimbwa. Ni wakati huu ambapo Amri Abedi Kaluta alitunga kitabu kilichoordhesha sheria za utunzi wa mashairi ya Kiswahili ambacho walidai kuwa kilihitajika kuweka kiuongo kizuri na wakati uliopita . Hata hivyo, kwa nia ya kufufua baadhi ya anuwai za wakati uliopita, Shaaban Robert

alitokea kutumia mitindo mbali mbali, mingine ikionekana ngeni kabisa. Hiki kilikuwa kipindi cha urasimi mpya.

Miaka ya Sitini (1960) hadi sitini na saba (1967) ilikuwa ya kuyumbayumba katika ushairi wa Kiswahili. Hali hii ilisababishwa na nchi za Afrika Mashariki kupata uhuru wake na tataruki iliyofuata ya jinsi ya kujiendezea maswala yake. Ni wakati huu pia ambapo washairi wawili maarufu, Sheikh Shabaan Robert na Amri Abedi Kaluta waliaga dunia. Washairi wapya walikuwa wanaibuka ambao hawakutaka kubanwa na sera au kanuni yoyote ya kizamani. Hewa ya uhuru na mabadiliko ilienea pote na washairi hawakuachwa nje ya mkondo huu mpya wa mambo. Wao pia walikuwa na maswala mapya ya kuwasilisha kwa jamii kama njia ya kujinasibisha na huo mwamko mpya.

Kuanzia 1967 hata leo, washairi wenye mtazamo huu mpya walijitangaza hadharani na kutunga diwani kamilifu zinazoensi mkondo huo mpya. Mgogoro juu ya umbo hili la shairi la kiswahili ulianza na kuzidi kupamba moto. Hali hii ilindelea kufikia miaka ya themanini, ambapo ushairi huru ulikita baada ya makongamano na ulumbi mkali sana.

Kimsingi waandishi wanaelekea kukubaliana kwamba ushairi wa Kiswahili ni sehemu ya utamaduni wa jamii ya Waswahili. Ushairi huu umepitia mabadiliko mbali mbali kuambatana na tajriba na athari dhidi ya jamii yenyewe. Shairi, ilivyo fasihi yenyewe, ni zao la jamii. Hivyo, umbo la shairi la Kiswahili limekuzwa kuitia vipindi mbali mbali. Kwa mfano, shairi la Kiswahili limepitia hatua kama vile: kupata vina vya mwisho, hatimaye vya kati na mizani kabla ya kuufikia ushairi huru. Hivi ni kufuatia madai kuwa ushairi huu ulianzia kwenye nyimbo zisizo na vina wala mizani. Hata hivyo, wengine hulipuza dai hili kwa kauli kuwa shairi lingetwa shairi tu kwa kijidhihirisha kwa sifa bainifu.

Fauka ya hayo, tutaelezea hatua za mwanzo za ushairi wa Kiswahili kuwa nyimbo k.v. misemele, nyio, lelemama nachi n.k ambazo ziliimbwa mionganoni mwa wakazi wa mwambao wa pwani katika shughuli zao za kijamii. Hatimaye kulitokea ulumbi wa kishairi na tenzi.

Baadhi ya tenzi hizi zilifika kuandikwa, na zingine kutoka ugenini kutafsiriwa. Taratibu kukafikiwa urasimi wa kitarbia, na hatimaye tungo kiushi za kisasa (ushairi huru)

2.3 USULI NA MAENDELEO YA USHAIRI HURU KATIKA KISWAHILI

Ushairi huru haujakuwa tu tukio la kipekee lilioukumba' ushairi wa Kiswahili. Ni hali ilivyokuwa umeupitikia pia ushairi wa mataifa mengine ya ulimwengu. Wengi hudai kuwa ushairi huu mpya umeingizwa katika ushairi wa Kiswahili kupitia athari za kimagharibi. Kupitia athari za tajriba juu ya fasihi za kimagharibi, ukiushi dhidi ya arudhi za kijadi za ushairi wa Kiswahili ulianza.

W. Mwai, (1988) anasema kuwa ni tukio la ukuaji wa kiwango cha elimu. Anaandika kuwa ushairi huru:

...warudi nyuma hadi kipindi baada ya uhuru na mojawapo ya athari
kuu ni usambaaji wa elimu ya kimagharibi (uk. 30)

T. Arege, (1998) naye anasema kwamba huu ushairi katika Kiswahili;

... hasa ultokana na athari za wazungu walioisha jitoma katika bahari
ya ushairi huru, na pia usomaji wa kazi za kimagharibi miongoni mwa
watanzi wa Kiswahili. (uk. 22)

Imekwisha elezwa pengi kuwa wenyeji waliokuwa wamepata elimu ya Kimagharibi walianzisha chachu ya kutaka mabadiliko katika jamii. Hata baada ya mataifa yao kupata uhuru wa kisiaza wengi hawakuvutiwa na hali mambo yalivyoendelezwa na washika hatamu. Mbali na upana na upya wa maswala walijotungia, wao walijizatiti kutokea na miundo mipyä isiyofungwa na arudhi za kimapokeo. Jamii zilikuwa zinabadilika, nao pia walihitaji kuakisi mabadiliko hayo. Pamoja na kutaka mabadiliko ya hali ya kijamii, walihitaji mabadiliko pia katika fani yao A Mazrui (1988) anaeleza:

...ilhamu ya washairi hawa wapya imehusishwa na hali nyingine za mazingira, kwamba mdundo wa ilhamu yao unatokana na ngoma nyingine. (uk. ix)

Hali kama hii ilishuhudiwa katika mataifa ya Kimagharibi baada ya *'Mageuzi ya Kiviwanda'*.

Kwa mujibu wa maelezo yake, haya yalikuwa mabadiliko mengine ya kitamaduni, na hivyo yaliyohitaji mwitikio tofauti pia.

Kwa mfano huko Tanzania, mbali na kupata uhuru wa kisiasa, kulikuwa na Mapinduzi ya Unguja (1964) na Azimio la Arusha (1967); ambayo ni matukio makuu yaliyoipitikia jamii hiyo. Ni mabadiliko ya aina hiyo katika jamii yanayodhaniwa kuwa kichochezi cha mageuzi dhidi ya kanuni za kimapokeo.

Mbali na mkabala huo, kuna dai tofauti pia kuwa ushairi huru katika fasihi ya Kiswahili haukutokana na athari za mataifa ya nje bali ulikuwa urejelezi kwenye ushairi wa kale ulioibuka katika nyimbo, ambazo hazikuwa na vina wala mizani. E. Kezilahabi (Tuki: 1983) anapomnukuu Farsay, (1960) anatoa mfano wa wimbo unaokubalika kishairi japo haukuwa na vina wala urari wa mizani:

Hongera mwanangu wee hongera
Mwana jaha jamali kujamili uso wake
Utango na utambae uwe mwana wa baraka... (uk.144)

Anaeleza kuwa japo katika wimbo huu hakuna vina wala urari wa mizani, wimbo wenyewe humo katika hali ya kishairi zaidi kuliko mashairi mengine yaliyotokea katika gazeti la "Uhuru", huko Tanzania. Mawazo haya hukubaliana na kauli kuwa chanzo cha ushairi wa Kiswahili ni nyimbo zisizokuwa na taratibu maalum za kufuata vina wala mizani. Ni mkondo huu wa mawazo ambao unahusisha uasisi wa ushairi huru katika Kiswahili na urejelezi wa tingo kongwe za Uswahilini. Hivyo majaribio ya Sheikh Shaaban Robert ya Kuurudisha ushairi wa watunzi wa enzi zilizopita huonekana kuwa hatua ya kimsingi ya kuanzisha mbinu

hii ngeni katika enzi ya urasimi wa kitarbia. E. Kezilahabi (1976:2) akirejelea barua iliyoandikwa H.E. Lambert na Sheikh W. H. Whiteley, anasema:

Shaaban Robert bila Shaka ni nguzo muhimu katika fasihi ya kisasa...

Anaeleza kuwa 'beti hizi' za Shaaban zilikuwa chanzo cha kuufufua utunzi uliosahaulika. Yeye aliruka mipaka ya kutawaliwa na muundo wa aina moja tu, na hapo kuwaacha nyuma washairi "... wengine wa wakati huu..."(uk.1 k.h.j.) M.H. Abdulaziz (1979) anaandika:

Shaaban Robert haruhusu kubanwa kabisa na sheria za kikaida za 'mashairi'.

Katika majaribio yake kuhusiana na umbo amevunja nyingi za sheria zilizochukuliwa kuwa za kikaida na wafuasi wa mikondo ya kikale. (uk. 61)

(Tafsiri yetu)

Kauli kama hizi zimefanya baadhi ya wahakiki kudai kuwa Shaaban Robert ndiye mwanzilishi wa ushairi huru. Mawazo ya K. Kazungu (1982), anayemnukuu Abdulaziz(k.h.j) yana mwelekeo huo. W. Mwai (1988) anashikilia msimamo huo huo kwa kauli kwamba ushairi huu katika fasihi ya Kiswahili uliasisiwa na kina Shaaban Robert na Abdilatif Abdalla, ambao walianzisha aina fulani zake.

Madai haya aghalabu yaliongozwa na maeleo ya Abedi Kaluta (1962) katika utangulizi wa Kielezo cha Fasili anayetoa kauli kuwa, Shaaban:

Ametunga ya aina nyingi ... ya mashairi yenyе mistari mingi ambayo hajulikani kwa washairi wengi wa kisasa (miaka ya mapema ya 1960)... nami sioni ni kitu kwa sababu gani wengine walianza sisi tukafuata, nasi tusianze wajao wakafuata...(uk. xiii)

Shairi la Shaaban katika Kielezo cha Fasili kuuhusu ushairi wa kiarudhi wa urasimi mkongwe linadhihiri uchochezi wa Shaaban katika kutafuta mabadiliko:

Nashikilia ukale, ambapo hapana budi
Na huacha vile vile, iwapo haunifaidi....
Kwa pingu za kawaida, sitajifunga kusudi
Kila sheria kwa muda na wishapo hairudi

Pingu hazina faida, bali hupinga kuhidi
Wala hiyo siyo, kwa watu wa jitihadi (Uk.19)

Akichangia kuhusu kutopingika kwa ukiushi, Abedi Kaluta (k.h.j.) anaeleza:

Lakini kama mshairi amekusudia shairi lake lisomwe lisiimbwe hangekuwa na njia bora zaidi kuliko kuacha kulitoa katika taratibu ya nyimbo iliyozoewa... utakuta kuwa mashairi yasiyoshika desturi iliyoenea ... yamepambika kama furusi juu ya pete na kama pete vidoleni.

(1962: x vi)

Ni kwa sababu ya madai kama haya ambapo usuli wa ushairi huru katika Kiswahili hurejeshwa kwenye majaribio ya Shaaban ya kuufufua ushairi wa kale. Hapo Kezilahabi (1976) hudai kuwa hamu ya kurejelea mbinu mbali mbali zilizotumika na washairi wa zamani ilizua ushairi huu mpya.

Tunakubali kuwa ushairi wa Kiswahili ulikuwa umechukua awamu mpya. Kwetu tutaridhia kuuita mkondo huu mpya 'urasimu mpya' katika ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo, ni badiliko muhimu katika hatua za kuufikia ushairi huru. Badiliko moja hupishwa na ile lililotangulia.

2.3.1 HATUA ZA MAENDELEO YAKE

Kitsao (1982) anasema kuwa mashairi huru huenda labda yalianza kama tungo za kimajaribio tu yatokanayo na vuguvugu la wanamabadiliko katika ushairi wa Kiingereza, vuguvugu ambalo lilijaribu kujitenga na kaida za urari wa vina na mizani.

Pamoja na kuchukuliwa na baadhi ya watu kama ulioanza kiajali, ulihimiliwa na kuendelea. Waanzilishi hawa walitaka njia mpya za kuelezea mada ngeni, kwa njia huria zaidi. Aghalabu ulithaminiwa na waaplimu na wanafunzi wa vyuo vikuu waliokuwa wameishaingiliana na kuathiriwa na fasihi za kizungu.

Baada ya uasisi wake, ushairi huru ulishika kani katika miaka ya sabini (1970). Diwani nzima ya kwanza yenye mashairi huru ni Kichomi (Kezilahabi, 1973). Diwani hii ilifungua ukurasa mpya katika ushairi wa Kiswahili. Kezilahabi, anavyojieleza katika utangulizi wake alipania kughairi matumizi ya lugha ngeni, na kupendekeza matumizi ya lugha ya kawaida. Yeye, hali kadhalika aliungama kuwa yu mshairi huru. Hapo ametokea ta tungo zilizokaidi kabisa kaida za kimapokeo zilizoeleka. Hapo ndipo upinzani dhidi ya mkondo huu mpya ulipoanzia.

Utunzi wa aina hii ulipingwa sana na wanafidhina kupitia magazetini na redioni na pia kupitia chama cha 'UKUTA' (Ukuzaji wa Kiswahili na Ushairi Tanzania) ambapo vyombo hivi vyote vilisimamiwa na wana-mashairi jadi. Kwa sababu ya mgogoro huu, kwa muda mrefu, hakukutolewa diwani zingine za kishairi huru hadi mwishoni mwa miaka ya sabini. Washairi wengine k.v. Kahigi na Mulokizi walifuatilia mfano wa Kezilahabi.

Baada ya mgogoro na mjadala wa muda mrefu ushairi huru ulijitawalia nafasi yake katika ushairi wa Kiswahili. Hivi kufikia miaka ya tisini kazi kadha zinazofuata mkondo huu zilikuwa zimekwisha chapishwa. Mnamo 1988, A. Mazrui alichapisha Chembe cha Moyo baada ya K. Mutiso kutoa Mizani Yangu mnamo 1986. Katika chembe cha Moyo (1988) amesema kuwa haoni haja ya mgogoro kwani mapote yote pinzani yana nguvu na udhaifu wake. Yeye anatoa mwito mgogoro huo ukome muradi kila shairi litimize nia yake.

Katika Karibu Ndani (1988) Kezilahabi anatudhihirishia ushairi huru umeshinda na kukubalika kama aina ya ushairi wa Kiswahili. Katika shairi lake, 'Karibu Ndani' anaandika:

Washairi wa mapokeo, sasa wacheza la lasalama, katika mionzi hafifu, ya juu machweoni,... Mhimili wake ni mmoja, umeanza kukatika.... (uk. 34)

Imeelezwa kuwa Karibu Ndani.

Ni mwendelezo wa fani ya ushairi huria ulioleta mgogoro mkumbwa katika miaka ya sabini, (Utangulizi)

Hata hivyo, hata baada ya mgogoro wa kishairi kufisia, miaka ya tisini ya karne ya ishirini haikushuhudia maandishi mengi ya mkondo huo yaliyochapishwa, ila tu mfano ya shairi moja moja hapa na pale. Mwaka wa 1997, Kithaka wa Mberia ametokea na diwani yake: Mchezo wa Karata na hatimaye Bara Jingine (2001) ambazo mbali na kuwa zimefuata mkondo wa ushairi huru, zimetokea na matumizi ya mbinu ngeni zaidi katika ushairi wa Kiswahili.

Ametokea kutumia sitiari ya kimchoro ambayo haijatumika penginopo katika ushairi wa Kiswahili. Kazi hizi zake ndizo za karibuni zaidi kuchapishwa katika mkondo huu, na tutaichanganua fani na maudhui yake baadaye kwa kirefu.

Kimsingi, usuli na ukuaji wa anuwai hii mpya katika ushairi wa Kiswahili umeweza kujitetea kwa ukweli kwamba, sanaa ambayo ni sehemu ya utamaduni wa jamii haina budi kubadilika kufuatana na mabadiliko ya jamii yenye. M. Mohammed (1977) anasema kuwa mashairi:

Hayakukaa palepale katika ukale wake, yamebadilika kutokana na maendeleo ya mawazo ya mwanadamu. Basi kumetokea na kukua kwa bahari mbali mbali za ushairi katika hilo umbo lake. Kila hatua inapofikiwa huwa si budi itumike, haizuiliki (uk.3)

Anavyoeleza Mazrui, katika ukuaji wake mashairi huru yametokea kuwa ya aina mbili.

- (i) Kuna yale yasiyofuata mizani, vina vituo haya tunaweza kuyaita mashairi –huru’
- (ii) Kuna yale ambayo yanafuata mizani bila kufuata vina na vituo na hapa pengine jina la mashairi –vye’ lingefaa zaidi”

T. Arege (1998) anaorodhesha mikondo yake kuwa inayojumuisha; mashairi yanayofululiza kutoka mwanzio hadi mwisho bila migao ya beti; yafuatayo vina, hasa ya mwisho; yatumiayo michoro, na yenye mipangilio kibeti bila kujali mizani. Sisi tunayagawa kutatu;

- 1) yasiyofuata vina mizani wala beti
- 2) yanayotumia michoro
- 3) yaliyopangwa kibeti bila kujali vina, mizani wala utaratibu maalum wa arudhi.

2.4 VIGEZO VIKUU KATIKA USHAIRI HURU

Msisitizo juu ya vigezo tofauti na vile vilivyothaminiwa na wanamapokeo uliletteauzuaji wa jina la wanamabadiliko kurejelea watunzi wa mkondo wa ushairi huru. Wao, badala ya kusisitiza vigezo vya kikaida vya umbo la shairi k.v vina, mizani na utenganishaji wa beti, walisisitiza vitu tofauti.

K. Wamitila (2002) anaeleza kuwa ushairi huru, badala ya kutegemea mizani kuzua wizani wake,

... hutegemea mbinu nyingine kama mpangilio wa sentensi, unyumbuji maneno, mpangilio wake (graphic design), muundo wa beti n.k (uk. 96-97)

Wamitila anaeleza hapa kuwa badala ya kuumba mdundo wa shairi kuitia matumizi ya vina na mizani yenye mwitikiano fulani mshairi huru hupangilia vipashio vikubwa zaidi- maneno kupata mdundo huo. Maneno yanayoleta takriri hutumika kuibua umuziki katika tungo hizi. Pamoja na takriri ya sauti na maneno; hutumiwa pia mbinu ya usambamba ambapo maneno au vifungu fulani vya maneno hupangiliwa kwa ustadi fulani. Mpangilio wa aina hiyo huzua utamu wa kifonolojia katika usomaji wa maneno yaliyo katika shairi, na hivyo huunda wizani ya mashairi haya.

Usambamba wa kimawazo pia hutumika ambapo fahiwa fulani baada hatua fulani za ukuaji wa shairi. Beti huundwa kwa ustadi unaothamini mbinu hizi za usambamba na takriri.

Wazo au muundo uliotokea katika ubeti fulani hurudiwa na kukaririwa katika ubeti mwingie japo kwa leksemu tofauti.

Kuhusu muundo wa beti pia hutokea kuwa beti zingine, hufupika kuliko zingine zilizo katika shairi lile lile. Nia ya beti ndefu yumkini huwa ni kuonyesha muumano wa kisa bila kukatizwa na hisia tofauti huku beti zilizofupika zikinuiwa kuzua wizani unaofuatika upesi kimuziki. Hali kadhalika ushairi huru hutumia beti zenye mishororo mirefu au mifupi kuzua hisia mbalimbali za kiridhimu. Mipangilio hii pia huathiri maana wakati mwingine na ndiyo asili ya wizani unaounda umbuji wa kisanaa katika ushairi huru.

Anavyoeleza mmoja wa watunzi wake, E. Kezilahabi (1974), ushairi huru una sifa ya kuwana kutumia lugha sambazi, ya kawaida na inayotumika mionganoni mwa wengi. Anaeleza kuwa analotaka:

... kuleta katika ushairi wa Kiswahili ni utumiaji wa lugha ya kawaida, lugha itumiwayo na watu katika mazungumzo yao ya kawaida...(uk. ix)

Japo dai hili hupigwa na baadhi ya wataalamu, tunakubaliana na Kezilahabi kuwa ushairi huru hujaribu kujitenga na matumizi ya lahaja fulani tu, hasa za kipwani. Badala yake hupania matumizi ya lahaja ya Kiswahili sanifu ambayo si lahaja, asilia ya yejote. Nia hii hutazamwa kama hatua ya kupendelea utaifa kama anavyoeleza A. Mazrui (1988), na hivyo kuutoa ushairi katika mipaka ya utamaduni wa Kiswahili . Hudaiwa pia kuwa hatua hii pia ililenga kuundolea ushairi uzufu wake.

Kufuata mbinu za kinathari pia ni mionganoni mwa vigezo vya kimsingi vinavyoutambulisha ushairi huru. Ushairi huu hukwepa matumizi ya mipangilio ya kibeti ambapo kila ubeti huwa na idadi sawia ya mishororo. Badala yake, mashairi haya hujumuisha mishororo mirefu na mifupi kwa mchanganyiko usio na utaratibu maalum, sawa na sentensi zilizo katika maandishi ya kinathari.

Pia ushairi huru hauthamini takwa la ushairi wa kimapokeo kuwa ubeti uwe na utoshelezi fulani kimaana beti zitokeazo katika ushairi huru hulinganishika na aya katika maandishi ya kinathari ambazo bila kuwekwa pamoja hazijitoshelezi kimaana. Anavyoandika W. Mwai (1988) ‘kuukataa uhuru kamili wa ubeti ni baadhi za sifa za ushairi huru. Ushairi huru ulikwepa kanuni hiyo ya ujitoshelezi wa beti ambao ulifanya shairi kuonekana kama mkusanyiko wa mistari tu iliyozungwa pamoja bila sababu maalum wala umoja wa maudhui. Hapo ushairi huru husisitiza shairi liwe na umbo lenye muumano zaidi unaolishikamanisha kama kiungo kimoja, hasa kimaana. Kwake, matumizi ya mbinu za kimathari ya kufululiza katika shairi.

Hali kadhalika, ushairi huru hauna kaida ya kutumia kibwagizo katika tungo zake. Kibwagizo kilionekana kama njia ya kuhitimishia ubeti na hivyo kuupa ubeti uhuru dhidi ya ubeti zingine. Badala yake ushairi huru huhiari matumizi ya mbinu zingine kama vile za usambamba wa kisintaksia na kifonolojia au wa kimaana uliowekwa kwa kusudi maalum.

Watunzi wa kishairi huru wamebadilisha mtazamo wa kikale wa kuandikia mambo ya kidhahania, kuzifia na kuiburudisha umma tu. Wao wametawaliwa na uelewa wa maisha na kuyazungumzia kwa mkabala wa tajriba ya sasa katika jamii yao. Kwa njia hii mshairi huru huwa mtathmini wa hali ya sasa ya jamii, na hivyo akaonekana mwasi wakati mwingine. Huwa amejitolea mhanga kuukashifu na hatimaye kuusafisha uozo wa kijamii.

Matumizi ya alama nyingi za uakifishi katika mshororo mmoja pia ni zifa maarufu katika ushairi huru. Mshororo mmoja unaweza kuwa na urefu wa kutosha ubeti mzima. Hili hufanikishwa kwa matumizi ya vituo kadha vinuko n.k. katika mshororo mmoja. Mwai (k.h.j.) anasema kuwa hii ni hatua ya kuunganisha ushairi huru na mkondo wa ushairi wa kisasa wa mataifa ya Kimagharibi na huufanya ushairi kunasibika na nathari.

Ushairi huu huweza kutumia wahusika au nafsi za kiusimulizi wa nafsi ya kwanza, kwa kujizungumzia yeye mwenyewe. Pia usimulizi wa kinathari unaohushisha nafsi ya tatu hutumika pengi. Mtunzi pia huweza kutumia usimulizi horomo, usiohusika nafsi yoyote mahsusisi, ambayo ni mbinu ya kimaelezo. Ushairi huu hutokea hata kuchanganya mchanganyiko wa nafsi anuwai katika shairi moja. Kwa mfano, shairi la ‘Ngoi na Waimbaji’,

Bara jingine una mchanganyiko wa nafsi kwanza umoja na pia wingi. Kwa mfano ubeti wa kwanza na wa pili:

Ubeti I: Ngoi sijali, kwa ni jali...

Ubeti II: Hatujali, kamwe, hatujali... (uk. 51)

Nalo shairi la ‘Ngao’ (k.h.j.) linadhihirisha matumizi ya nafsi ya pili, umoja, na pia nafsi ya kwanza, wingi katika ubeti wa pili (uk. 59) na ule wa mwisho (uk. 60)

Pamoja na matumizi ya nafsi mbali mbali, ushairi huru una sifa iliyokolea ya matumizi ya mchanganyiko wa usemi halisi na ule wa taarifa. Hivi ni kwamba, katika shairi la kitaarifa hutokea hali za unukuzi wa moja kwa moja pia.

Mashairi ya mkondo huru huegemea zaidi matumizi ya vipengele vya kitaswira na picha. Hili huhalishwa na matumizi ya alama mbali mbali za kiuakifishi, maumbo anuwai ya ubeti zake, pamoja na uchoraji wa mandhari kwa unayeti mkubwa. Kwa mujibu wa Kezilahabi (1983) ushairi huru hutumia ufundi wa kulifanya wazo lionekane ‘kama shilingi iliyo majini, ambalo kulipata mtu hapeleki mkono wima tu, bali hubidi apige mbizi’.

Ushairi huru huonyesha uanuwai wa mipangilio katika utungaji wake. Kwa kususia maumbo mahsus ya kikaida, na kusisitiza upitishaji wa wazo tu, kwa njia anayopendelca mtunzi, ushairi huu umekuwa na mipangilio isiyokadirika. Maswala yanayozingatiwa zaidi huwa ni kama vile wiano wa kiwizani na si mpangilio, ambapo msisitizo huwa kwenye wazo la kimsingi tu.

Mbali na sifa za kimuundo, ushairi huru hudhibitiwa zaidi na maswala ya kihalisi ya maisha ya sasa. Watunzi wake aghalabu hupiga hatua ya kutaliki maswala ya kidhahania, na utabarudi tu. Wao hutokewa kujisaili pamoja na jamii yao. Kwa njia hii, wao hutokea kuikejeli hali iliyopo katika jamii kwa kuyamulika baadhi ya maswala yanayochafua haki na mahusiano. Pengi, wao huchukuliwa kuwa na mtazamo wa kiusai. Kimsingi, ushairi huu umetokea kusisitiza zaidi vigezo ambavyo hudhibiti maana na fahiwa zinazolengwa huku ukipuuza umaarufu wa umbo kama kitambulisho kikuu cha utungo wenyewe.

2.5 SWALA LA MGOGORO WA USHAIRI

Kuzuka kwa ushairi huru wa Kiswahili kulianzisha upinzani mkumbwa kutoka kwa wanamapokeo. Wapinzani hawa walionelea kuwa shairi la Kiswahili lazima lifuate taratibu na

kanuni fulani zisizobadilika. Wanamabadiliko hawakuona umuhimu wa sheria hizo katika kazi ya kisanaa, kama vile ushairi. Wao walihisi kwamba kila mmoja anafaa kuwa huru kuteua njia itakayomfaa kupitishia mawazo yake kishairi. Kwao, zile mbinu zilizoitwa sheria na wanamapokeo ni ufanano wa mashairi tu kiumbo ufanano ambaa hauna lazima ya kudumishwa. Ni mitazamo hii inayokinzana ambayo ilibusha mjadala mkali juu ya umbo la shairi la Kiswahili, mjadala ulioshia kuwa mgogoro mkubwa baina ya mapote mawili hayo.

Mgogoro wenyewe hasa ulifungamana na suala la umbo la shairi la Kiswahili. Yumkini kichochezi chake ni kijelezi cha wanamapokeo kuwa ‘ili shairi liitwe shairi ni lazima liwe na muundo fulani mabsusi. Wanamabadiliko waliuona huu kuwa utumwa unaozuia ubunifu ambaa ndio uti wa mgongo wa kazi yoyote ya kisanaa. Wao waliliona ushairi kuwa hai na hivyo usio budi kubadilika.

Huku wanamapokeo wakiuona ushairi kuwa mtalaa wenyewe kanuni na kaida zake elekezi, wanamabadiliko waliuona kama bahari wazi kwa yeote mwenye nia ya kuogelea. Mmojawapo wa hawa watunzi wapya, Kezilahabi (TUKI, 1983) anaandika kuwa:

... Kadiri msanii anavyozidi kufuata kwa dhati kanuni zilizowekwa tayari ndivyo anavyozidi kuwa ntumwa wa kanuni hizo na inafikia mahali zinamtawala na kusababisha uozo. (uk.146)

Anaeleza kuwa msanii hana satua dhidi ya uozo huo ila kuzivua kanuni hizo. Ni uvuaji wa kanuni hizo za kikaida uliosababisha mgogoro baina ya hawa wanamabadiliko na wanamapokeo. Huku wanamapokeo wakiuona uvuaji huu wa kanuni kuwa kupotoka mionganii mwa hawa washairi wapya, wao walionelea kuwa:

... ni kosa kuegemea kutatua matatizo ya sasa kwa kutumia shoka lile lililoachwa na mababu bila kufuata mbinu mpya.

(Kezilahabi, TUKI, 1983 – 144)

Wao waliona mabadiliko ya nyenzo kuwa njia ya maendeleo.

Wanamapinduzi wajiona kuwa wanaoishi katika enzi mpya na tofauti na jamii ya mbeleni walihisi kuwa walikuwa wanakabiliana na tajriba mpya, maswala mapya ya kijamii, ambayo valihitaji mbinu mpya pia kuyaelezea. Wao walienzi wazo kuwa, mfumo wa maisha na matukio ya kihistoria huathiri sana ushairi, na mbinu za kifasihi kwa jumla kwani kila kitu kimo katika mabadiliko. Kwa upande wao, wanamapokeo walishikilia kuwa asiyetaka kufuata sheria anafaa kueleza mawazo yake kwa njia nyingine tu bila kuuchafua ushairi –kwa miundo isiyo na msingi.

Kufuata kanuni zisizobadilika , walisema wanamabadiliko,, kuliwabana washairi wasiweze kueleza mawazo yao kikamilifu. Mazrui (1988) anaandika katika utangulizi wake kwamba;

... kwa sasabu ya kujishughulisha sana na kanuni za arudhi mshairi huwa hana wasaa mkubwa wa kuimwaga ilihamu yake vile imjiavyo katika kujenga fikra na mawazo ya mashairi yake. (uk. ix)

Kwa upande wao, wanamapokeo walidai kuwa:

... Washairi wa pote la mabadiliko wametuletea huu muundo ‘mpya’ kwa sababu hawajazimudu vyema mbinu za ushairi na kwa hivyo wakashindwa kutunga mashairi kwa mujibu wa mbinu hizo, (k.h.j: ix)

Msimamo wao ni kuwa mawazo yanafaa kujiingiza yenye we katika arudhi zile. Mayoka (1986) anasema kuwa mjadala:

... ulianzishwa na watafiti wa kigeni... Mmoja wa waanzilishi wa mtafaruku huu ni Lyndon Harries aliyewahi kudai kuwa mashairi ya Kiswahili yana asili ya mashairi ya Kiingereza ambayo hayana vina, ...

Na hatimaye kudai kuwa:

... washairi wa Kiswahili hawana desturi ya kuandika mashairi yasiyo na vina,
(uk. ix)

Kauli zake hizo zilichagiza ari ya wapinzani wa pande mbili hizo, kuanza kulumbana kuhusu unavyofaa kuwa ushairi wa Kiswahili. Kama kauli ya kijumla ya wanamapokeo, Mayoka anaeleza kuwa:

Kila utungo wa shairi umefungika upande wa mistari..., vina na mizani. Mashairi yote yaimbwaa, yanaweza pia kusomwa au kusemwa tu. Tungo zisizotimiza yote hayo si mashairi (k.h.j:x)

Wanamabadiliko nao walidai kuwa lililo muhimu ni kule kudhihirisha usanifu wa kupandisha maudhui kwa taswira na uteuzi wa lugha, au njia yoyote inayonata akilini.

Anavyoandika Njogu (1999) wanamapokeo waliuona ushairi huru kama:

...janga ambalo sharti lisiruhusiwe 'kuunajisi'ushairi wa Kiswahili;
...Mshairi ana jukumu la kuutetea... ushairi kama ulivyopokelewa (uk.119)

Kwa mujibu wa mawazo haya, ushairi usiofuata arudhi hauna thamani ya ushairi kamwe, na kuwa ili kuuhifadhia ushairi hadhi yake ni lazima kudumisha hali yake iliyopokelewa.

Kezilahabi (TUKI, 1983), ambaye mwanamapinduzi, anasema kwamba:

Mgongano kati ya wanamapokeo na wanamapinduzi katika kazi za kisanaa ni jambo lisiloweza kuepukika....Mitindo mipya hujaribiwa na falsafa mpya kuibuka kufuatana na mikondo mipya ya Kihistoria, fikra na mahitaji ya binadamu... Fasihi si maji mafu, ni hai (uk.144)

Kwa majibu wa kauli hii, inaashiriwa kwamba arudhi za ushairi, japo zilifaa kwa wakati wake, zilikuwa hazina budi kupishwa na ushairi kutambua mbinu zingine. Hili bila shaka lingewabughudhi walioziafiki lakini ni tukio lisiloepukika kusudi kuuhuisha ushairi kiwakati.

Wanamapokeo walihisi kuwa vina na mizani ni mali na amali ya kitamaduni ya Waswahili, walio wenyeji wa ushairi wa Kiswahili. D.P. B. Massamba (1976) aliandika:

Ushairi wa kimapokeo ndio ushairi wa Kiswahili kwa sababu chimbuko lake ni Uswahilini (uk:vi)

Madai haya yalilengwa kuhamisha tungo zingine zote zisizofuata kaida za kihuko. Nao wanamabadiliko walilumba kwamba sanaa si mali ya yeyote, ni milki ya jamii kwa jumla.

Wanamabadiliko walidai kuwa matumizi ya vina na mizani ni uigaji kwa ushairi wa ugenini hivyo wakakanusha kauli ya wanamapokeo kuwa ndizo uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Njogu (k.h.j.) anaandika:

Na kwa kuwa kila kitu cha asili ya Kiarabu kilikuwa ndicho kipimo cha ustaarabu.. walichukulia kuwa ni jambo lililokubalika kwa shairi liwe na urari wa vina na mizani. (uk. 119).

Wanabadiliko, kwa hiyo walieleza kuwa ushairi asilia wa Kiswahili ultokana na nyimbo ambazo hazikuwa na vina wala mizani. Kwa hivyo wanamabadiliko waliwakemea wanamapokeo kwa mtazamo wao uliokengeuka. Walijiona wao kuwa waaasilia zaidi na hapo kuwastihizai wanamapokeo kwa kuipuuza jadi ya Mwfrika.

Kwa mujibu wa Kezilahabi (TUKI, 1983);

Kitaaluma mjadala juu ya ushairi ulifikia upeo wake katika kongamano lililofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ... Mjadala huu uliendelezwa redioni na katika gazeti la 'Uhuru'. (uk. 145)

Kupitia mjadala huu, waandishi walinua kuelezana walichoelewa kuhusu ushairi wa Kiswahili, hasa kuhusu mbinu na misingi ya utunzi. Hapo wanamapinduzi walidai kuwa:

... wanamapokeo wanapozungumzia ushairi wanakuwa na maana finyu, na sisi maana pana. Hii ni kwa kuwa washairi wengi wa Kiswahili hawajakuwa na uhusiano na ushairi wa mataifa mengine (k.h.j.)

Hili ni thibitisho kuwa tajriba waliyopata wanamapinduzi kutokana na ushairi wa kwingineko ilikuwa kichocheo muhimu cha mgogoro huu. Kupitia vyombo vyahabari, wanamapokeo walipinga hali hii ya wanamabadiliko kuthamini tamaduni za kigeni na kuacha asili yao.

Katika kilele cha mjadala huu, wanamapokeo walikataa kata kata kuutambua ushairi huu mpya. Kwa, mfano, mhafidhina, Ruo (TUKI,1983) anaandika:

... inafahamika wazi kwamba ushairi wa Kiswahili umo katika hatari ya kuharibiwa au hata kuangamizwa na wachache waliozuka baina ya 1960 na 1975. Baadhi ya watunzi hao wanafahamu neno ushairi tu bali hawajui ni fani

gani au una asili ya namna gani na ni jinsi gani asili inavyofungamana na fani hii iliyo na tanzu kadhaa.

(uk. 140)

Kujibia dai hili wanamapokeo walijidai kuwa walio na mtazamo mpana kuuhusu ushairi kuliko wanamabadiliko wenyewe. Hili lilizidisha ulumbi juu ya ushairi wa Kiswahili.

Wenye msimamo wastani zaidi waliamba kuwa usasa ulikuwa ni mashairi lakini yasiyo ya Kiswahili, kwa mujibu wa Mazrui (k.h.j.). Msimamo horomo unaochukuliwa na C.N. Chacha (1992) ni kwamba:

... kule kutofahamu lugha pana ya kutumia katika utunzi wa mashairi kusichukuliwe kuwa ni udhuru unaotosheleza haja ya 'waatsi' ... wanapokiuka kanuni hizi za kawaida; ... kundi linaloafiki hoja kwamba fasihi yoyote ile kadiri inayokua na kupanuka lazima, ikubali mabadiliko... mambo huja yakaenda, (uk. 112)

Hapa Chacha anaangaza wazo kwamba ushairi hauna budi kubadilika, lakini mabadiliko wenyewe hayana budi kudumisha hadhi fulani ya tungo, hasa kwa jinsi lugha inavyotumiwa.

Akifuata mkondo huo huo, Abiud (1998) anaandika kwamba:¹

Jambo la kutambua ni kwamba kila pote lina madai ya kweli lakini... hoja za upande mmoja hazitoshi kuhusu umbo la ushairi wa Kiswahili. Jambo la muhimu kutambua ni kwamba fani huwa kiungo muhimu na ni lazima kuwepo katika mapote haya mawili... (uk. 48-49)

Huu ni msimamo unaotambua aina mbili hizi za mashairi, lakini unaotambua umuhimu wa kuwepo kwa ufundi fulani katika kulisana shairi. Wale waliohisi haja ya kuukomesha mgogoro huu walitokea na kauli horomo zaidi. Kwa mfano, Chacha (k.h.j) aliandika kuwa:

jamii ndiyo yenye jukumu la kupiga kelele juu ya mtindo ambao hauwanufaishi na wala sio kikundi tu cha wasomi 'wachoyo'... (uk.112)

Kauli hii inaafiki ukweli kwamba kitu kinachotegemea usanifu wa kiakili hakiwezi kumilikiwa na watu au kundi la wachache tu.

Wakati mgogoro huu ukifisia, A. Mazrui (k.h.j) alitoa kauli kuwa:

...kila tunapoutazama mzozo huu tunaona ya kuwa hauna msingi
wa maana, basi naukome (uk. xiv)

Mawazo haya ni kwa sababu hakuna kundi lililofaulu kuonyesha wazi wazi uhalali wao na papo hapo kutoa hoja zisizopingika kuonyesha uharamu wa lile lingine. Mapote yote yalikuwa na hoja zao thabiti na haikuhalisika kuzidi kuzozania maji yasiyofumbatika.

Kufikiri miaka ya tisini mgogoro huu ulikuwa umeisha kufisia na ushairi huru kuchukua nafasi yake katika ushairi wa Kiswahili . Hili linaonekana katika tungo za Kezilahabi k.v. ‘Karibu Ndani’ (1988: 34-39); ‘Moshi Ukizidi Pangoni’ (Uk.11); ‘Ngoma ya Kimya’ (uk.43) Katika miaka hiyo pia wahafidhina wengi walikuwa wameisha konga sana au hata kijifilia mbali.

2.6 ULINGANISHAJI KIHISTORIA WA USHAIRI HURU NA ULE WA KIMAPOKEO

Ulingenishaji baina ya ushairi wa kimapokeo na ushairi huru utatoa mwanga zaidi juu ya sababu za mgogoro uliowahi kuwepo baina washairi huru na wanamapokeo. Wakati wa mgogoro mapote yaliyojitenga yalitetea aina mbili tofauti za ushairi wa Kiswahili. Kwanza kabisa, wana mapote hayo walielekea kutumia istilahi ‘ushairi’ kwa maana tofauti. Njogu (k.h.j.) anasema kwamba wanamapokeo waliuona ushairi kama muundo maalum uliofungwa katika mipaka ya utamaduni wa Kiswahili.

Kwa upande mwingine, wanamapinduzi waliona shairi kama kipashio cha kisasa, na kulipa mtazamo mpana, mtazamo ambao pamoja na kusisitiza umuhimu wa lugha iliyopangiliwa kwa ufundi fulani, huegemea zaidi upitishaji wa mawazo kijazanda.

Kwa mtazamo wa kihistoria, ushairi wa kimapokeo pengi ulichukuliwa kuwa ushairi ulioonewa fahari na kutukuzwa na jamii kuwa wa kirasimu (k18) na hivyo kukadiriwa arudhi fulani. Urasimu huu hususan uliitwaza bahari ya kitarbia; mishororo minne katika kila ubeti,

pamoja na upatanifu wake wa vina na mizani. Kwa upande wa pili, ushairi wa kimapinduzi, ambao umeingia katika fasili ya Kiswahili katika karne ya ishirini, ni aina ya ushairi wenye tingo huria zaidi, usiofuata arudhi zinazothaminiwa kimapokeo.

Badala ya kushughulika na uwekaji wa vina na mizani, ulimwacha mtunzi huru kuyapangilia mawazo yake bila kubaniwa na kanuni zozote zilizopangiliwa kimbele. Ushairi huu huegemea upitishaji wa mawazo kuititia njia za kinathari na taswira. Kwake lililo muhimu si umbo la shairi bali ni ule upitishaji wa mawazo kwa njia ya yenyε kugusa hisia.

Huku wahafidhina wakiuona ushairi kuwa kipawa na milki ya wachache wenye ilihamu mahsusisi wanaofuata ushairi huu huuona kama mali ya umma inayoweza kubadilika na hali za kijamii. Hapo ushairi huru huchukuliwa kuwa wenye demokrasia ya kindani tofauti na ule wa kihafidhina unaoshikilia sheria sugu zisizoruhusu mabadiliko. Msimamo wa wanamapokeo ulikuwa kwamba vijana wasiobobea wakaruhusiwa kutunga watalilemaza na kulitia guni lile umbo halisi la shairi. Kezilahabi (1973) anadai kuwa;

Lugha inayopendelewa na watunzi wa mashairi huru ni ya kawaida, ya matumizi ya kila siku.

Kwao matumizi ya kikale au lahaja ni mapokeo yaliyokwisha pitwa na wakati. Kwa upande wake, ushairi wa kimapokeo husisitiza matumizi ya lugha isiyokuwą ya kawaida ili kuvyaza hisi. Kwa mujibu wa wafuasi wa ushairi huu, lugha rasmi ni dhaifu upande wa istiara, msamiati na mbinu zingine za kifasihi. Wao huiona kuwa kavu na inayokosa ufasaha unaohitajika katika utunzi wa mashairi. Labda hili ni swala la majadala kwani kuna baadhi ya watunzi wa kiarudhi wanaoonyesha ufasaha mkubwa.

Kuhusu umbø, ushairi jadi unashikilia lazima ya kuwa na umbo fulani mahsusisi. Unaafiki utungaji wa beti kamilifu zenyε idadi maalum ya mishororo inayodumisha idadi fulani ya mizani pamoja na vina vyenye urari, kutegemea bahari. Kwake hayo ndiyo uti wa mgongo wa shairi la Kiswahili linaloruhusu uimbikaji na ukumbukaji rahisi. Mashairi huru hayathamini

mawazo haya. Kwake husitizwa maudhui katika shairi kuliko umbo. Ushairi huru kukubali umbo lolote muradi wazo lipitishwe kwa usanifu fulani unaogusa hisia kwa kutumia mbinu kama vile za usambamba, takriri na taswira za kiumbo. Kwa njia hii, ushairi huru huweza kidhibiti mawazo yake na wa la si kwa kutumia umbo lolote maarufu.

Ushairi huru hudaiwa kuwa uliotoka kupanua kwa kutambua mabadiliko yanopitikia jamii. Mawazo yake yamepevuka zaidi huku yakizisaili hali zilizopo, kushughulika na siasa ya kisasa n.k. Hususan, ushairi huru hidhibiti maswala mazito zaidi na nyeti kuliko ushairi wa kijadi. Kwa upande wake, ushairi hafidhina ulihusika na maswala mepesi yanayohusika na kuiburudisha jamii, dini na wasifu; hasa maswala yaliyotculiwa kikaida.

Mbali na hali na umbo la mashairi yenye waandishi wa mashairi wamejigawa katika mapote kwa kuzingatia maeneo ya kijipografia. Ushairi huru umezuliwa katika Kiswahili hasa na vijana waliopata elimu ya Kimagharibi, na hasa ya vyuo vikuu. Wengi wao walikuwa wa kutoka bara. Ushairi hafidhina nao umepata watetezi wake mionganoni mwa wazee, hasa wa kutoka pwani. Hawa walijiona kuwa wachache wenye kipawa hicho.

Kwa mujibu wa Kezilahabi (TUKI,1983) huko Tanzania uanamapokeo ulitetewa na makundi ya walioshika hatamu za uandishi wa magazeti na vyama kuihusu lugha yenye
(k.v. UKUTA). Hawa waliwaona wanamabadiliko kuwa waliojaribisha:

... vipengele vya kizungu kutunga mshairi kwa njia za nathari... Mohammed (k.h.j)

Wanamapokeo hawakukubaliana na kauli hii. Wao walijiona kuwa watu binafsi walio na tajriba na ujuzi muhimu wa kisanaa, na walionua kuuteremsha ushairi uwafikie watu wa kawaida.

Hata hivyo, wakati huu ambapo mgororo umetulia, washairi wa makundi haya mawili wameanza kuona uwezekano wa mapote yote kuwepo katika ushairi ule ule. Baada ya mijadala mirefu wameona vipengele fulani vinavyowakutanisha. Kote hutambuliwa matumizi ya ligha

ya mkato inayoibua hisia mbali mbali, uteuzi wa maneno wenyewe malengo maalum, pamoja na matumizi ya picha na taswira katika kujenga maana zao. Matumizi ya beti pia husambaa kote. Hivi ni vigezo vinavyotambuliwa na ushairi wa mapote yote.

2.7 HITIMISHO

Katika sura hii tumeshughulika hasa na usuli na maendeleo ya ushairi huru katika fasihi ya Kiswahili. Tumeonyesha kuwa ushairi huu ni hatua mojawapo ya mabadiliko ya kijamiii. Ushairi wenyewe ulifikiwa baada ya mabadiliko mbali mbali katika ushairi wa Kiswahili.

Tumeonyesha baadhi ya tofauti zake na ushairi wa kihafidhina na kuangaza mvutano ulioibuka baina ya watunzi wa mapote yote mawili. Hili lilihusu hasa umbo la shairi la Kiswahili.

Hatimaye tumelinganisha baina ya mapote hayo mawili ya ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia vigezo vina~~y~~osisitizwa na pande zote. Japo ushairi huu mpya haukuoana na kaida zilizozoleka kimapokeo, tumetaja kuwa fani hii mpya imejipenyeza na kupata kutambuliwa kama aina nyingine huru ya ushairi katika ushairi wa Kiswahili. Hili liliikiwa kwa msimamo sugu uliofuatwa na wanamapokeo ambao walismama tisti kuonyesha kuwa ushairi huru si swala geni bali ni badiliko lilopitiwa na ushairi wa kwingineko pia.

SURA YA TATU

MATUMIZI YA MBINU ZA LUGHA KATIKA KUJENGA MAUDHUI

3.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutazichanganua na kuzihakiki diwani za Mchezo wa Karata na Bara Jingine kifani na maudhui. Tutachunguza hasa jinsi vipengele mbali mbali vya lugha viliviyotumika katika ukuzaji wa maudhui. Tutashughulika na maswala kama vile uteuzi wa vifungu vya kisarufi pamoja na tamathali za usemi. Vipengele vingine vya kifani tutavishughulikia katika sura inayofuata.

Itafaa kama tutatanguliza kwa kutoa fasili za istilahi ‘maudhui’ na ‘fani’. Kwa mujibu wa kamusi ya The longman Dictionary of Literary Terms (1985), maudhui humaanisha:

...wazo au mawazo makuu yanayoweza kupangiliwa ya kazi ya kifasihi,
yaani, kile ambacho kazi yenye we inahusu.

(Tafsiri yetu)

Mwenda Mbatia katika Kamusi ya Fasihi (2001) anasema kuwa maudhui ni:

...jumla ya mawazo, fikra dhamira na hisia...vinanyowasilishwa na kazi ya fasihi.

Anaeleza kuwa:

Kwa upande mmoja maudhui yanajibu swalii la nini kazi ya fasihi inazungumzia, kwa upande mwingine fani inajibu swalii la vipi maudhui yanawasilishwa.

Kwa mujibu wa fasili hizi, maudhui ni mawazo anayopitisha mwandishi katika kazi ya kifasihi kwa mpangilio fulani. Mtunzi bila shaka huwa na mambo ya kueleza katika kazi yake. Hiyo ndiyo sababu yake ya kuandika, nayo ndiyo huitwa maudhui.

Kuhusu fani, Kazungu (1982) anaeleza kuwa fani katika fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake. Anaeleza kuwa ni ufundi huu wa msanii ambao huweza kuijenga au kuibomoa kazi ya kifasihi, ikavutia au ikachusha. Jinsi alivyovitumia vipengele vya fani husaidia uelewa na mvuto katika upitishaji wa maudhui. Nayo kamusi ya Oxford Advanced Learner's Dictionary inasema kuwa fani ni:

Umbo la nje la kitu au mtu, mpangilio mahsus wa kitu au muundo wa kitu, jinsi kitu kinavyoonekana au kukaa, muundo wa kawaida na mpangilio wa kitu katika zile tungo za kimuziki au zinazoandikwa, kinyume na maudhui yake.

(Tafsiri yetu)

Maelezo haya yanatuashiria kuwa fani ni ufundi wa kuyapangilia yaliyomo. Ni kule kuyaweka maudhui katika sura fulani ya kuonekana, na si yaliyomo yenye. M. Msokile (1993) naye anaandika kwamba:

Fani ni umbo, ufundi, au muundo wa kazi ya sanaa. Mambo kama lugha itumikayo, mtindo, muundo, mandhari na kadhalika.

Huyu anataja vipengele vinavyojenga fani ya kazi ya kifasihi na kuonyesha kuwa mbali na lugha, fani ni ufundi mzima wa kuisana kazi ya kisanaa. Mbatia (k.h.j.) anakubaliana na mawazo haya anaposema kuwa fani ni:

Jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubeba ujumbe na maana mahsus.

Kwa hiyo, tunachukulia fani kuwa jumla ya mbinu zote za kisanaa zinazotumiwa na mtunzi katika kuiunda kazi yake. Mbinu hizi husaidia kuwasilishia malengo yake kwa umbo mahsus na kwa mvuto unaopendeza. Maudhui ya kisanii hayabadiliki bali mbinu huteuliwa kimtindo na msanii mwenyewe.

Katika sura hii hatutashughulikia mbinu zote za kifani bali mbinu za kilugha tu kwa kuchunguza jinsi zinavyoingiliana na maudhui mbali mbali. J.S. Mdee (1986) anaandika kuwa:

Lugha ni chombo kilichoundwa na wanadai mu kwa ajili ya matumizi yao.

Kwa hiyo tutatathmini humu matumizi ya lugha kama njia ya msanii wa fasihi ya kuyaelezea mawazo yake kwa jamii. Tutachunguza matumizi ya vipengele vyake mbali mbali kama chombo cha kubebba maudhui.

Inavyolewaka ni kuwa suala la lugha lina uzito mkuu katika ujenzi wa fani kwani vipengele vyake ndivyo hubeba maana. Vipengele vingine vya kifani havina uwezo wa kujielezea mbali hutegemea jinsi ya upangiliaji wa maana inayobebwa na lugha.

Kimsingi, lugha ya kishairi huwa ya mkato, bunifu, hisishi na yenye uhuru mwingi dhidi ya kanuni za kisarufi. Lugha hii uhitaji uteuzi mwafaka wa miundo ya kisarufi pamoja na matumizi haifu ya tamathali mbali mbali za kiusemi.

Tumenuia kuonyesha humu mshikamano wa vipengele vya lugha na maudhui. Tunataka kuonyesha jinsi fani na maudhui ni vitu viwili visivyoweza kutenganishika. Lugha hulengwa kuitisha maudhui ambayo ni muhali kujengwa bila matumizi yake. E.V. Roberts (1994) anasema kuwa:

Mashairi hujengwa kwa maneno, yaundayo mbinu mbali mbali za kifani (uk. 576)
(Tafsiri yetu)

Anaeleza kuwa mashairi huwasilisha mawazo kwa njia iliyopambwa kwa lugha ya mkato. Hii ni kuonyesha kuwa mawazo yajengayo maudhui hupitishwa kuitia lugha kama chombo chake.

Katika kuzihakiki diwani hizi tumegawa maudhui yake katika mafungu manne makuu:

1. Maudhui ya siasa
2. Mazingira
3. Utamaduni
4. Dhuluma ya kimapenzi

Katika kuangalia jinsi maudhui haya yalivyojengwa na msanii, tutaongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Umuundo na ile Kisosholojia.

3.2: SIASA

Maudhui kuu katika diwani hizi ni yale ya kisiasa. Kithaka Mberia ametokea kuyatathmini na kuyakejeli maisha ya jamii yake hasa baada ya miongo miwili ya uhuru wa kisiasa barani. Jamii ya wakati huu ilishuhudia kutengwa katika makundi mawili; kundi la watawala dhalimu na umma uliohasirika. Anaonyesha kuvunjwa kwa ndoto za jamii za hali kubadilika baada ya uhuru na kukariri kuwa mabadiliko waliyoparamia yalikuwa 'mazigazi' tu. Katika kuitashtiti hali ya sasa, ametunga mashairi kadha yenze kiimbo kinachokashifu hali hii potovu. Mbinu mbali mbali za lugha zimetumiwa kujengea taswira inayoumulika uongozi mbaya wa kisiasa.

Takriban mashairi yote yaliyo katika Mchezo wa Karata yanakuza maudhui haya. Sehemu kubwa zaidi pia ya Bara Jingine inamiliwi na maudhui haya. Mifano yake ni kama vile; 'Machozi ya Damu' (uk. 1); 'Jumapili ya Damu' (uk.6), 'Kikaoni Addis Ababa'(uk.2); 'Kamba na Jabali' (uk.3) , 'Bara Jingine' (uk.10) ; 'Obasanjo' (uk.17), 'Mruko wa Nyuki' (uk.20). Haya ni baadhi ya mashairi tutayotumia katika kuyaelezea maudhui ya kisiasa katika uhakiki wetu. Tutataja mifano kutoka penginopo pia kulinganishia na hii yetu. Maudhui haya yameendelezwa vizuri sana kwa matumizi ya mbinu mbali mbali za lugha. Uteuzi wa maneno na wa kimuundo umechangia pakubwa.

Kwa mfano, kuna matumizi ya 'ndoto' kuonyesha matarajio ya raia pindi waliponyakua uhuru wa kisiasa. Neno hilo limetumika katika mahairi kama : 'Ndoto' (uk.1.MwK), 'Msumari Moyoni' (1997: 4) 'Hatutaaga Ndoto' (2001: 4), 'Bara Jingine' (2001: 10) n.k.

Uteuzi wa neno lenyewe pia unaweza kuonyesha kuwa matarajio ya hali kubadilika ni jambo la kidhahania tu. Ni taashira ya ugumu wa mambo kubadilika. Kwa mfano, katika shairi 'Ndoto'(k.h.j.) mtunzi anataja "ndoto" inayotisha utulivu katika jamii. Anasema:

Mara nyngine

Naota ndoto

Ndoto tishi kama

Udikteta

Naona majambazi wenyе bendera
Wakitutwanga vichwa na rungu
Huku nyimbo hewani
Zikisifia, zikitukuza
Rangi ya usiku (uk.1)

Hapa mtunzi anainasibisha hali iliyo katika jamii yake na hiyo ya 'udikteta' unaotukuzwa.

Kupitia huku kutukuzwa kwa udikteta anaashiria ugumu wa hali kubadilika.

Neno 'ndoto' pia limetumiwa kutumainisha. Ni maono dhidi ya hali hii mbaya. Linaashiria kubadilika kwa hali iliyopo katika jamii. Kwa mfano, katika shairi 'Bara Jingine' (k.h.j) mtunzi anaandika:

Ndoto yangu
Ni tamu
Kama asali
Ndoto ya bara jipya
Bara ambapo
Bunge
Halitakuwa ukumbi
Wa genge la nzige

Kuna pia msamiati uliotumiwa kitaashira kuwakebehi viongozi waovu wanaonyanya raia. Huu unawanasibisha na viumbе tishi, wabaya, na wawezao kuangamiza. Kunatajwa: "Miungu" (wa kinamo), "mazimwi", "mamba", "mbu", "nzige".

Kwa mfano katika shairi 'Jumapili ya Damu' (2001) anaadika:

.... Nayo mizinga hatari
Inatega mbingu
Huu mtiririko
Ni safari ya marejeo
Anarejea mungu- wa-kinamo
Kwenye ulingo (uk.8)

Hali hii ya ubaya na hatari ya hawa viongozi pia inajitokeza katika shairi; 'Bara Jingine' (k.h.j) asemapo:

.... Katika ikulu
Hakutapinda mamba
Bali kuketi binadamu
Watu wenge damu (uk.11-12)

Msamati wa aina hii unatuashiria, na kukejeli, hali ya viongozi kuwa wadhulumu dhidi ya raia wao.

Mbali na maneno pweke kuna pia matumizi ya miundo ya kinahau kuelezea hali iliyopo. Kwa mfano, katika kuonyesha hali ya kujisikitikia miongoni mwa raia, mtunzi anasema katika 'Machozi ya Damu' (2001) kuwa "majuto ni mjukuu" (UK.1). Katika kutumainisha dhidi ya hali hii anaandika katika 'Kamba na Jabali' (2001) kuwa:

Papo kwa papo
Kamba ya wadhulumiwa
Hakata jabali gumu
Ambalo miungu – wa –kinamo
Hutumia kuzibia njia
Ya binadamu (Uk.3)

Aghalabu beti anazotumia ni ndefu sana, beti ambazo pengi zinaundwa kwa mshororo mmoja tu. Hili linaonyesha muumano wa suala linalozungumziwa, siasa. Mashairi yote yanadumisha maudhui moja tu hadi mwisho. Kwa mfano, katika Mchezo wa Karata, shairi 'Swali kwa Yangeyange' (uk. 41-42) ni refu sana na lenye ubeti mmoja tu'. Shairi 'Hatutaaga Ndoto' katika Bara Jingine linafuata umbo hilo pia (Uk.4-5)

Kwengineko kuna hali ya kutenga beti fupi fupi baina ya zile ndefu kwa nia ya kuchopeka kauli zenyezito kisiasa. Mfano kama huo unaonekana katika shairi 'Kamba na Jabali' (2001: 3:) ambapo sehemu inayogusia uwezakano wa kuwashinda viongozi waovu inatengwa kwa

kuingizwa ndani zaidi. Mtunzi ametenga mishororo miwili tu kuwa ubeti baina ya beti ndefu katika shairi ‘Mchezo wa Karata’. Mishororo hiyo inasema:

Tunatupa karata...

Wanatupa karata....(uk. 19)

Mbali na uteuzi wa miundo ya maneno na beti, lugha ya kitamathali imetumiwa kujengea maudhui hii. Lugha hii imelengwa kujenga taswira madhubuti kuhusu siasa ya wakati wa utunzi wa mwandishi. Baadhi ya tamathali hizo ni kama vile:

3.2.1 Tashbiha

Tashbiha hutumiwa kutolea picha fulani kwa njia ya ulinganishaji. Hujumuisha utumiaji wa viungo fulani ili kuzua mwelekeo fulani wa kimaana, badala ya kutumia vielezi au vivumishi tu. Huibua hisia nzito zaidi.

Tashbiha nyingi zimetumiwa nazo zinafananishia tabia, na kukejeli utawala au watawala watukufu pamoja na raia hohehahe. Kwa mfano katika Mchezo wa Karata, shairi “Viwavi na Nzige’ kuna tashbiha kwamba:

Kicheko chako jamala

Kulipamba mandhari

Mithili cha mtoto mchanga

Mapajani mwa mzazi (uk. 36)

Tashbiha hii haikutumika hapa kama njia ya kulinganishia tu. Tunaweza kuona hali ya kitaswira inyozuka katika mfano wenyewe. Tunaundiwa taswira ya mtoto aliyepakatwa na mama yake. Zote mbili zinasaidia katika kuzua fahiwa iliyonuiwa. Mbinu hizi zimeleengwa kulinganisha jinsi watawala wanavyofaidi jasho la raia wanaowafanya yote, sawa na mtoto aliyepakatwa na mamake.

Mbinu zingine zinazochangiana na tashbiha hii katika kuonyesha dhuluma ya kisiasa ni usambamba unaojitokeza hasa baina ya ubeti wa tatu na wa nne. Katika ubeti wa tatu, kunatajwa kikosi cha viwavi wanaoshiriki karamu. Nao ubeti wa nne unazungumzia ‘nzige’ waliojipweteka kwenye mazulia mekundu shereheni. Neno ‘nzige’ pia limetumiwa kisitiari kuwamulika viongozi walafi. Mbinu hizi zinachangiana vyema na tashbiha tuliyoidokeza mbeleni katika kuyakuza maudhui ya kisiasa. Uteuzi wa msamiati “nzige” “mtoto” anayepakatwa umelenga kutoa maana ya utegemezi. Tashbiha “mithili ya mtoto mchanga” imelenga athari hiyo hiyo pia.

Akisifia kitendo cha Obasanjo cha kukubali kung’atuka uongozini, kinyume na walivyo viongozi wengine barani, mtunzi anamsifu kwa tashbiha kuwa:

Kitendo chako

Kilikuwa na ladha

Kama matone ya asali (2001: 17)

Tashbiha hii imelengwa kutafakarisha kuwahusu viongozi walio na tabia kinyume na yake, kwani wengine wangekuwa kama yeye, tabia yake haingesifiwa vile. Kusaidiana na tashbiha hii katika kukariri uovu wa viongozi walio kinyume na Obasanjo, mtunzi ameteua msamiati hisishi kama vile: “mwewe”, “mauti”, “Izraeli”, na “cheche ya fataki”.

Mbali na mfano huu, tashbiha zimetumiwa pengi aghalabu kulinganishia hali ya uongozi wa sasa. Kwa mfano, katika ‘Hatutaaga Ndoto’ (2001), mtunzi ameandika:

...Kichaa cha ufisadi

Kimesambaa kote

Mithili viini vya kichocho (uk. 4)

Tukiangalia mifano hii miwili tunaona jinsi inavyochangiana kuonyesha mkinzano wa tabia za aina mbili za viongozi. Inaleta matumizi ya mbinu ya kinyume.

Mbinu hiyo pia imesaidiana na matumizi ya msamiati kama vile: "sumu", "ufisadi", "vita" na "mamba" katika kuibua kiimbo na maana iliyolengwa kwa uwazi zaidi. Matumuzi ya tashbiha katika shairi hilo ni mengi pia.

Matumizi ya mbinu hii yamefana sana katika kuikuza maudhui haya. Tumeona kuwa mbinu hii imechangiana sana na mbinu nyingine katika ukuzaji wake wa maudhui ya siasa.

3.2.2 Tashihisi

Kuna matumizi mengi ya uhuishi wa viumbe mbali mbali. Pengi, viumbe hawa wamelengwa kufananishwa na viongozi na utawala wao unonyanyasa raia. Nia yake hasa ni kufumba mambo fulani nyeti.

Viumbe hawa wametokea kuongeleshwa na kuulizwa maswali fulani ya balagha. Kwa mfano, katika Bara Jingine, shairi 'Hatima ya Mbu' (uk.19), mbu anatangaziwa kuisha kwa utawala wake. Huku ni kuwapiga vijembe viongozi waovu, wasiotakiwa.

Katika Mchezo wa Karata, shairi 'Utandabui Muuaji' (uk.31) kuna maswali yanayoelekezwa kwa 'Utandabui' ambayo ni tashhisi inayokwepa mkabala wa ana kwa ana na viongozi wanaosutwa. Kwa mfano, mtunzi anauliza:

Kwangu mezani
Nisipotafuna
Nitatafunu wapi? (ub.2:31)

Tunaona kwamba mbali na matumizi ya tashhisi kuna swali la balagha pia katika fani hii. Mbinu hizi zinasaidiana kuitisha ujumbe kwa hisia nzito zaidi na hapo kuifikirisha hadhira. Hali kama hiyo, inaonekana pia katika 'Swali kwa Konokono' (1997: 33)

Katika shairi 'Msimu wa Mazigagazi' (1997: 23) mshairi ametumia tashhisi kuisawiri hali mbaya ya wakati wa ukoloni, na pia ile ya wakati huu. Anaandika:

Adhuhuri ya juzi

Huku kaa la kiu

Limetukalia kooni...(uk. 23)

Anaonyesha hali ya wakati ule na kisha kufahamisha kuwa hali hiyo haikubadilika kwa:

.... Ukweli umeinua uso

Na kubainika machoni

Mzagao tuliuona

Haukuwa maji

Bali mazigazi! (k.h.j)

Mbali na kuisawiri hali hiyo kwa njia hisishi ya kitashihisi, tunaon pia hali ya ujengaji wa taswira ya hali mbaya anayolenga mtunzi ya kuumia na kudanganyika kwa raia. Kuna taswira ya ‘kaa kukalia kooni’, na ‘uso kuona kuona hali ya mazigazi’. Kwa mshikamano mmoja, mbinu hizi zinachangiana kuitisha wazo la mtunzi kwa unyeti mahususi.

Anapoupa ‘ukweli’ sifa ya kuinua uso kama vile binadamu, ananuia kutaja kuwa ni ukweli ulio wazi kuwa hali ni vile vile tu, haijabadilika.

Tashihisi humu ina uwezo mkubwa na inampa fursa msomaji, na wale wanaopigwa vijembe, kujilinganisha na kiumbe anayehuishwa. Mbinu hii imefaulu kwani maswala ya kisiasa ni nyeti na hubidi yazungumziwe kwa tahadhari fulani. Mtunzi ameyasawiri vyema kwa matumizi ya mbinu hii. Ameyatoa maswali na dhihaka zake kwa kuvitumia viumbe vingine. Vivyo amevitumia viumbe vile kutolea picha ya jinsi hali ilivyo duni kwa uongozi wenye mushkeli. Ameonyesha pia jinsi bara lingekuwa bora kama mkondo wa kisiasa ungebadilishwa, kuitia kwa tamathali hii.

Hata hivyo, ili kufaulu katika dhima yake ya kuhisisha kitashtiti, mbinu hii imesaidiana na mbinu zingine anuwai. Kwa mfano, katika shairi ‘Utandabui Muuaji’ (k.h.j) kuna matumizi ya maswali ya balagha na pia beti fupi fupi ambazo zinaundwa kwa maswali hayo yanayosisimua tafakuri. Katika ‘Msimu wa Mazigazi’ mtunzi ametumia pia mbinu ya sitiari kukoleza uovu wa

viongozi anaowapiga tashtiti. Anawalinganisha na "meno ya vikwata" na pia "ndimi za mipupu". Mbinu hizi zinachangiana katika kuumba maudhui yaliyolengwa.

3.2.3 Sitiari

Hii ni mbinu ya ulinganishaji usio wazi ambapo sifa ya kitu huhamishiwa kwa kingine bila ya kuwepo na viungio. Husaidia kujenga picha ya ulinganisho wa sifa za vitajwa kwa kukiita kitu kimoja kuwa ni kile kingine. Maelezo yake huwa yenye nguvu na yanayogusa hisia kuliko lugha ya kawaida. Mbinu hii imetumika katika diwani hizi na ikasaidia katika ukuzaji wa maudhui yake yakiwemo yale ya kisiasa. Katika 'Bara Jingine' kuna:

Bunge
Halitakuwa ukumbi
Wa genge la nzige
"Usalama wa taifa"
Hautakuwa ngozi
Ya kulinda mamba wa ikulu... (uk. 10)

Imetokea pia katika 'Viwavi na Nzige' na 'Msimu wa Mazigazi' kama tulivyoeleza hapo juu. Katika mfano wetu hapo juu (2001), mbinu hiyo imechangiana na zingine katika kujenga maudhui ya kisiasa. Akiwakejeli viongozi waovu pengi anatumia mbinu ya usambamba, ambapo vifungu fulani hurudiwarudiwa. Amewarejelea viongozi kuwa "genge la nzige", "mamba wa ikulu" n.k. Katika kuonyesha matumaini ya kesho wakati viongozi hawa watakaposhindwa, mtunzi ametumia tashbiha mbali mbali kuangazia hali itakavyokuwa kwa mfano, anataja ndoto "**tamu kama asali**". Mbinu hizi zinachangiana ili kuweza kufanikisha ukuzaji wa maudhui yenye ya siasa.

Japo mbinu ya sitiari ni maarufu mionganoni mwa watunzi wengi, Mberia hakutokea kuitumia sana katika ukuzaji wa maudhui haya. Kwa mfano, A. Nassir (1982) ameitumia vyema sana mbinu hii katika shairi lake 'Simba Mwenda Pweke' anapodai kuwa:

Ndimi samba ndume, ndimi mwelevu wa nyina
Niwazingae wasemi, wa huja wakadangana
Ndimi mkingama ndimi, zisipate la kunena...(uk. 4)

Yeye anajilinganisha na simba bila kutumia viungio.

Hata hivyo maudhui haya yamekuzwa pia kwa matumizi ya sitiari ya mchoro. Sitiari hii hujitokeza katika kiwango cha umbo la utungo. Aina hii ya sitiari tutaishughulikia katika sura ya nne.

3.2.4 Taashira

Taashira hutumiwa kujengea taswira kwa kutumia 'picha' au maumbo yanayoweza kuhamishika hadi mazingira tofauti. Kitu kimoja kinachotajwa huwa ni kiashiria cha kitu kingine ambacho mtunzi hakuchagua kikitaja moja kwa moja. Aghalabu hutajwa vitu vilivyozeleka, kwa sifa zake, katika mazingira-husika kusudi kufanikisha uelewa. Katika diwani hii imetumika pengi katika kufanikisha ujenzi wa maudhui ya siasa. Imelengwa kufumba baadhi ya hoja. Kwa mfano, katika Mchezo wa Karata, neno "boga" (uk.2) limetumiwa kwa maana ya urithi au mali ya taifa huku "fujo tumboni" (uk. 7) likiashiria enzi ya mateso.

Tunavyoona katika shairi 'Boga' (uk.2) mshairi anatetea үsawa katika kugawana mali ya umma. Boga ambalo "si urithi wako si urithi wangu" (uk. 2-3) ni mirathi ambayo huhodhiwa na taifa au mataifa yetu ambayo tunafaa kugawana bila kubaguana. Katika shairi hili pia, mtunzi ametumia sitiari ya kimchoro katika kujenga taswira anayolenga. Tunaona aina ya mchoro wa duara uliogawika katikati, na^hii ni sitiari ya usawa unaofaa kuweko katika jamii. Mbinu hii inasaidiana na taashira inayojengwa kwa maneno katika kuyajenga maudhui.

Kama vile tashhisi matumizi ya mbinu hii ni kwa nia ya kuepuka kuwakabili walengwa ana kwa ana, kwa sababu ya unyeti wa suala lenyewe, la kisiasa.

Shairi ‘Mruko wa Nyuki’ (2001:20) ni taashira ya jinsi mataifa ya Kiafrika yalivyovutwa kuandama mikondo miwili tofauti ya kiuchumi; ule wa ukomunisti (ujamaa) na ule wa ubepari. Hatimaye ukomunisti ulisambaratika na kuuacha ulimwengu kudhibitiwa na ubepari ambao ni mfumo wenye uwezo mkubwa, na unaoudhibiti ulimwengu leo. Taashira yake inapigwa mwengo na matumizi ya sitiari ya kimchoro inayooenyesha picha ya mkondo uliofuatwa na nyuki. Kuna pia matumizi ya mbinu ya usambamba katika kuthibiti maudhui. Kuna urudiaji wa vifumbu kama vile “machovu, machovu...”, “ukusanyaji, ukusanyaji...”, “mabawa, mabawa...”, “mwendo, mwendo...”. Mbinu hizi zote zinachangiana katika ukuzaji wa maudhui.

3.2.5 Maswali ya Balagha

Hapa msisitizo wa ujumbe hufanywa kwa kuuliza swali ambalo halihitaji kujibiwa au ambalo jawabu lake linajulikana wazi wazi. Mbinu hii, kama vile zingine za kitamathali, huwajibika kusisitiza wazo ambalo mtunzi hakutaka kulielezea tu, au kulitaja moja kwa moja.

Baadhi ya maswali yanayolenga maudhui ya kisiasa humu yamelenga kuwakebchi viongozi waovu au kuwapiga daro watawaliwa waliozubaa na kuikubali hali kama ilivyo sasa. Katika Mchezo wa Karata, “Maswali kwa Mdudu’ (uk.51), maswali yote mawili yamelengwa kuwachagiza raia wanaonyanyaswa na utawala mwovu ambao wanazidi kuuunga mkono.

Swali la pili linauliza:

Basi utaacha lini haya mazoea
Ya kuhimili chama cha nzige? (uk. 51)

Chama kinachohimiliwa hapa huwakilisha chama halisi cha kisiasa au kundi la viongozi wanaokandamiza. Katika ‘Tajiri wa Lulu’ (1997: 16), tajiri anaulizwa jinsi alivyofikia kupata mali nyingi bila ya kuchoka kuitafuta. Aaulizwa:

Lulu haiwi ukingoni mwa njia
Wewe uogopaye maji ya chumvi...
Wewe ukwepaye maji ya matope...
Lulu makasha –makasha
Umekuwaje mmiliki? (uk. 16)

Swali hili linawapa changamoto watawala matajiri wanaowanyanya raia.

Tunaona pia katika ubeti huu kuwa mshairi anatuangazia picha ya uzembe wa mhusika kwa maelezo yake ya kitaashira. Taashira yenyewe inasaidiana na swali linaloulizwa mwishoni katika kufikirisha zaidi kuhusu hali ya viongozi inayozugumziwa. Hapa balagha na taashira zinakuza swala la siasa ya unyanyasaji linaloshughulikiwa.

Baadhi ya mashairi yaliyo katika Bara Jingine yanachukua mkondo wa swali katika kichwa chake na hivyo kuleta athari hiyo hiyo. Kuna; ‘Swali kwa Konokono’ (uk.33) na ‘Swali kwa Yangeyange’ (uk.41)

Mbinu hii imetumika kuibua hisia nzito nzito, na kuichochea akili ya msomaji. Maswali haya yamelengwa, kwa njia isiyo ya moja moja, kuchagiza utekelezaji wa kisiasa.

Maswali ya balagha yanachangiana pakubwa na mbinu za ulinganishaji kama vile tashbiha na sitiari (k.h.j). Mbinu ya usambamba pia inachangia sana na lengo la balagha kwa mfano katika ‘Bara Jingine’ (uk. 10) kuna urudiaji wa kauli “bara ambapo” wakati mtunzi anaponua kuonyesha bara anayowazia, ya kesho.

3.2.6 Takriri

Katika kuleta uzito katika mapigo ya kifonojia na kisemantiki, takriri huzua hali fulani za urudiaji wa sauti, maneno au visfungu. Hili huleta msisitizo fulani katika mazingira-husika.

Kauli zenyе uzito kisiasа zimepewa nguvu ya kuvuta makini ya hadhira kwa kutumia aina fulani za mbinu hii. Kwa mfano, mbinu hii imetumika katika shairi ‘Mruko wa Nyuki’ (2001:20) ambapo maneno yenе uzito kihisia yanatajwa na kurudiwa papo hapо, ilivyo katika mbinu ya pindu. Kuna takriri ya maneno kama vile: “machovu”, “ukusanyaji”, “ndoto”, “mwendo”, “kitambo”, “panda”. Sehemu ya pili inayorudia neno-husika inatoa maelezo fulani kuonyesha athari ya neno lenyewe katika mazingira hayo. Kwa mfano, kuna:

“mabawa, mabawa ya safari, safari ya tiba” (uk.21); “njia panda”, “panda tatizi”, “baada ya kitambo, kitambo cha jasho” (uk.22)

Aghalabu urudiaji huo unaelemea maneо yenе kutanguliza ujumbe wa kimsingi na nyeti katika shairi. Urudiaji wa aina hii pia unaumba hali ya usambamba wa kisauti na kimawazo pia. Mbinu hizi zinachangiana vizuri katika kuzuana na pia katika kuyakuza maudhui kwa urudiaji unaotafakarisha.

Takriri ya sauti inaonekana katika ‘Bara Jingine’ (2001) ambapo kina ‘mu’ mwishoni mwa mishororo mitatu ya mwisho kinakaririwa.

Bali kuketi binadamu
Watу wenyе damu
Na fahamu (uk.12)

Hili linaleta utamu katika masikizi. Hali kadhalika ujumbe unaowasilishwa ungeleta ‘utamu’ kwenye maisha ya wanaonyanyaswa. Kwa hiyo, takriri hiyo imelengwa kuwa ya kitaashira. Inavuta makini masikizini na hapо kuweza kusimua dhati ya kuzingatia kwa makini faida inayoweza kutokana na kitendo. Usambamba unaorudia kueleza kulihusu bara kwa: “bara ambapo...” unasaидia katika kuleta athari hii pia.

Katika Mchezo wa Karata, takriri ya kisauti inatokea waziwazi katika shairi ‘Amba’ (uk.5) ambapo sauti

“-amba” imerudiwa katika kila mshororo. Kwa njia ya vijembe na mzaha wa kitakriri, wazo nzito la kwamba wabambe wanaonyanyasa umma hawana budi kutimuliwa wajijutie linapitishwa. Hii ni mbinu inayofanikiwa katika kulipitisha hili swala nyeti la kisiasa, kwa kusaidiana na maelezo ya kimafumbo ya mawazo ya mtunzi kuhusiana na kali iliyopo. Kwa mfano, mamba anayezugumziwa anarejelea kiongozi fulani mkatili.

Katika shairi ‘Siku Chungu’ (1997:14) kuna takriri ya sauti, vitenzi na nomino kadha wa kadha kote katika shairi. Hii ni njia ya ucheshi inayotumiwa kusawiria hali ilivyo, na jinsi inavyosinya. Mfano kama huo uko katika ‘Mgunga Shambani’ (1997) matumizi ya mbinu hii katika mashairi mahsusini yenyе maudhui ya kisiasa ni mengi sana, na imefana katika kusisitiza mawazo fulani fulani mazito na nyeti.

Mbali na utukiaji wa takriri katika mashairi mahsusini, mbinu hii imesambazwa kote mionganini mwa mashairi yenyе maudhui haya. Vifungu na maneno fulani yenyе uzito mwangi kitaswira yamerudiwa baina ya mashairi tofauti. Kwa mfano katika Mchezo wa Karata neno ‘ndoto’ linaloashiria matarajio ya jamii limetumika katika ukurasa 39,47,58,18 n.k. ‘Miungu’, kuashiria viongozi bahili limetokea katika ukurasa 30,55; “ekundu” kwa maana ya ovu limo katika ukurasa 56,58 n.k. ‘Nzige’ kwa maana ya viongozi wanafiki limo katika kurasa za 24,33,35,40,51 n.k. Katika Bara Jingine kuna:

‘Miungu’ katika kurasa za 1,3,8,10 n.k; ‘ndoto’ katika kurasa za 4,10,12,13,21 n.k ‘damu’ (taashira ya usumbufu barani) katika kurasa za 1,2,7,8 n.k.

Msamati unaokaririwa unatupa picha ya hali ya kisiasa wakati wa utunzi. Huu nao ni ujengaji wa taswira inayosaidiana na takriri katika kushadidia wazo la kimsingi kuhusu siasa ya wakati unaozugumziwa.

3.2.7 Msisitizo Bayani

Hii ni mbinu ambapo mafungu fulani hutumiwa kupitishia ujumbe kwa njia ya ufupi na yenyemvuto. Mbinu hii hutumia mkumbo wa vitushi au nomino badala ya kutoa maelezo mafupi. Kiunzi hiki cha maneno huwa hisishi na huweza kusisitiza wazo zito, kwa sifa yake ya kitaswira. Kwa mfano, katika Mchezo wa Karata: ‘Nyuki, Ndege na Nyegere’ kuna:

.... Kwa nuru nyusoni

Tabasamu machoni

Na ndoto nyoyoni (uk.10)

Huu ni msisitizo wa jinsi kundi la wahasiriwa (aghatalabu Waafrika) walivyodanganyika upesi na wageni wenye hila. Matumizi ya kifingu “lughya yenyeye sukari” pia ni udamisi unaosaidia kuonyesha kudanganyika kwa wahasiriwa kuitia maneno matamu ya wageni.

Msisitizo wa aina hii unahimiliwa na matumizi ya tashihisi katika:

Huzuni ikajenga maskani

Kwenye nyoyo zao... (uk. 11)

Dondoo hili nalo linaonyesha matokeo ya kule kudanganyika kwa wenyeji

Kwa pamoja mbinu hizi zinatumiwa kumsisitizia msomaji' juu ya kudanganyika kwa mtu mweusi na hatima ya tukio hilo. Hii ni safu mojawapo ya ujenzi wa maudhui ya kisiasa.

Katika ‘Msumari Moyoni’ pia kuna:

...na macho yaonayo

Masikio yasikiayo

Na hisia zihisizo...

Nikiota

Na kuimba

Na kutaraji (uk. 4)

Misisitizo kama huu unawapa changamoto wenyeji kutafakari walivyozaa tu na kungojea maisha yawaeleke tu. Mpangilio wa shairi lenyewe pia, ambalo linatenga vifungu mbali mbali

kwa nia ya kuvipwekesha vionekane kuwa beti tenge na zenyenye mpangilio anuwai, unachangia msisitizo huu (uk. 4).

Tunaona mifano kama hiyo pia katika Bara Jingine kwenye mashairi kama vile. 'Bara Jingine' kunako.

...wakulima wataimba nyimbo

Washairi

Watakariri mashairi...(uk.13)

Na katika 'Jumapili ya Damu' kuna:

Watu wanatereruka

Damu inatiririka

Uhai unaporomoka

Tunaona humu kwamba, mbali na msisitizo bayani, kuna hali ya usambamba na takriri za sauti ambazo zinalenga kusisitiza kasi ya matukio ya siku ile. Kimsingi, swala linalolelezwa ni upinzani dhidi ya serikali

Mbinu hii ni sifa maarufu inayojitokeza katika kazi za marehemu Sheikh Shaaban Robert aliyeitumia kotekote kwa ufundi na usanifu wa hali ya juu sana, katika riwaya na pia mashairi yake. Kwa mfano katika diwani ya Utubora Mkulima (1968) Shabaan anatongoa:

Adabu ni dhahabu,

Na johari ya moyo,

Na mstaarabu,

Ni mwenye kuwa nayo,

Na mbele ya aibu,

Kitu hiki ni ngao (uk. 56)

Hapa anasisistiza kuhusu thamani ya 'adabu'.

Kwa jumla, maudhui ya kisiasa imejengwa kwa matumizi mwafaka ya vipengele vya lugha katika diwani hizi kwa uteuzi unaoafiki, wa maneno, vifungu pamoja na tamathali mbali mbali za semi. Usawiri wa maudhui yenye umeonyesha hali ya kuhuzunisha kwa jinsi watawala

wanavyowanyanya raia. Yeye anaimulika jamii yake kwa jinsi alivyouteua msamiati na maudhui kutoka mazingirani mwake.

Hata hivyo mtunzi haonyeshi kuitalii kwa ujumla wake siasa ya wakati alipotunga kwani mashairi mengi yanadhibitiwa na swala la dhuluma na unafiki wa washika hatamu tu. Mtunzi angetamba kwenye maswala mengine kama vile uchaguzi, vyombo vyaa dola n.k.

3.3: MAZINGIRA

Kuna mashairi yanayobeba maudhui ya uthamini na utetezi wa mali asili. Tungo hizi zinaangaza juu ya hatari ya kuyaharibu mazingira yetu, huku zikionyesha manufaa yanayotokana na mazingira. Zinakashifu uharibifu dhidi ya miti, mito, anga zetu, mabwawa n.k. Baadhi ya mashairi yamepewa vichwa vyaa majina kama vile ya bwawa, mito na miti fulani mahsusii, na kuihuisha kusudi kuipa hadhi kuu ya kuthaminika.

Vipengele anuwai vyaa lugha vimetumiwa katika kuikuza maudhui haya. Hivi ni pamoja na uteuzi mwafaka wa msamiati unaooana vyema na muktadha wa kimazingira. Yametumia pia tamathali mbali mbali zinazosaidia katika kujenga maudhui yenewe.

Mashairi ya aina hii yanaanza ukurasa wa 53 hadi mwishoni mwa kitabu, (2001).

Uteuzi wa msamiati unaojitokeza katika mengi ya mashairi haya unaafiki mandhari ya kienyeji ya mazingira ya Kiafrika. Kuna msamiati unaohusiana na maumbile ya kimazingira, pamoja na ulio na kiimbo cha malalamiko na utetezi. Miogoni mwake kuna ule unaotisha na kukatisha tamaa kufuatia uharibifu unaofanywa dhidi ya mazingira yetu.

Katika baadhi ya mashairi kunatajwa mifugo k.v. "kuku", "ng'ombe", "kondoo", "mbuzi"; ilivyo katika shairi: 'Jinamizi' (uk.55) na 'Nyeri' (uk.70). Mtunzi anaonyesha faida ya mifugo hawa, na hivyo kuhimiza haja ya kuwashifadhi. Huku ni kuhimiza umuhimu wa kuendeleza kilimo. Aidha uteuzi huo unatambulisha msamiati kama vile: "kijani kibichi", "tanzu",

"wakulima", "majani-chai", "kahawa", "mahindi", "shamba", "mbegu", "mimea", "migomba". n.k. Msamati huu unatuashiria shughuli ya ukulima ambayo inaweza kusaidia katika uhifadhi wa mazingira. Hapa tunaona kuathirika kwa mtunzi na mazingira yake ya kijamii.

3.3.1 Tashihisi

Ili kuonyesha thamani ya mali asili, pengi amali hizi zimezungumziwa na kuonyeshwa kama kwamba ni binadamu. Miti, bwawa au mito inapoongeleshwa au kuachwa kujisemea, mtunzi amelenga kuteka makini na hisia za msomaji. Kwa mfano katika shairi 'Matone ya Mvua' (2001:73), matone ya mvua yanaongeleshwa moja kwa moja kama vile ni watu kushadidia thamani yake. Mtunzi anasema:

Enyi wageni wa thamani
Msiondoke kwa haraka
Kaeni, muwe ngome ya chuma...

Ili kupiga mwengo thamani ya matone hayo, kuna matumizi ya kauli zinazoyatukuza. Kauli hizo ni kama vile: "mmekomboa mimea", "mmeufuua miali jamala", "joto laini la furaha", "matumaini yanametameta" n.k. Mbinu hizi zinachangia kwa pamoja ukuzaji wa maudhui ya mazingira.

Pia 'Bwala la Ithanje' (2001:69) linaongeleshwa na kuhuzunikiwa kwa hali yake mbovu:

Pole ,bwawa la Ithanje
Pole pole afya yako inafifia...
Wanakukamulia sumu kinywani.

Kuna pia matumizi ya tashbiha:

Vinakuhambulia mwili
Kama vikosi hatari... (uk. 69)

Tashbiha hii inasisitiza pia hali mbaya inyolikumba bwawa hili.

Miti mbali mbali pia inaongeleshwa kama vile ni binadamu. Katika 'Mkalitusi' (2001: 67) tunaona:

Na kwa mkono imara
Kuyakamata maradhi
Na kuyatupa kaburini

Hapa thamani yake inasifiwa kama kwamba juhudi yake ni sawa na ya binadamu halisi. Mto Nairobi umepewa sifa ya kuongea kujitetea kama vile ni binadamu. Unasema:

Dhiki iliyoje
Tunaishi mtaa mmoja
Na majirani ambao
Asante yao
Ni mateke(uk. 63)

Malalamiko yake haya yamelengwa kuwahisisha wale wanaoshika jukumu la kuuweka nadhifu na safi. Kuna pia matumizi ya msisitizo bayani katika ubeti wa pili, ambapo mtunzi anaandika:

Kwa mafuta
Kwa makopo
Kwa talimbo... (uk. 63)

Huu ni msisitizo wa kuonyesha vichafuzi nya mto. Mbinu zote zinalenga kiimbo cha kulalamikia tabia isiyopendeza dhidi ya mto. Kuna pia matumizi ya msamiati kama vile: "wananitesa", "wananikaba koo", "wananiangamiza", ambao unasaidia pia katika kujenga kiimbo cha malalamiko dhidi ya dhuluma unayofanyiwa mto.

Mbinu hizi zina mchango wa pamoja katika kuonyesha haja ya kuchukua hatua ya kuokoa mto, na hivyo mazingira.

Huu uhuishaji wa maumbile ya kiasili unayapa nafasi kubwa ya kugusa hisia na hapo kuvuna matokeo ya mbadiliko wa tabia. Ni njia bora ya kuwasilishia mawazo mazito kuliko ile ya usimulizi uliozoeleka wa sauti tofauti kutetea uhifadhi wa mazingira.

Hata hivyo ingefaa zaidi kama mtunzi angeguzia swala la ni kwa nini tendo hili la uchafuzi linatokea. Angezungumzia swala kama lile la ongezeko la watu jijini ili kuyaoanisha mawazo ya shairi lake na jamii.

3.3.2 Taswira

Hii ni mbinu ya kuzua picha akilini kwa maelezo yanayochora mandhari fulani ya kihalsia.

Picha zinazoundwa kwa nguvu ya maneno yaliyopangiliwa vizuri humwathiri mlengwa.

Kwa mfano, katika ‘Ngao’ (2001: 59) tunaumbiwa picha ya kutuwezesha kutafakari uharibifu dhidi ya Ozoni kwa:

Kemikali jeuri
Zinatafuna ozoni
Kama majeshi ya mbwa
Yalivyovamia paa
La komba moyo (uk. 59)

Mshairi hapa ana lengo la kutuhisisha jinsi Ozoni inavyoharibiwa upesi na tabia ya mwanadamu, pamoja na kuwa mtandao huo ni muhimu sana kwa uhai wetu.

Matumizi ya msamiati hisishi pia yanasaidia katika uibuaji wa picha halisi inayolengwa. Mtunzi anatumia maneno kama vile: “zinatafuna”, “uchungu”, “uzuzi”, “makombora”, “kutushambulia” nk. Matumizi ya sitiari pia yanachangia katika kuonyesha umuhimu wa Ozoni. Ozoni inanasibishwa na: “ngao ya uhai” na “handaki ipara”.

Hapo tunaweza kuona jinsi mbimu hizi zinavyochangiana katika kujenga picha halisi ya hali ilivyo kuihusu Ozoni, na vivyo mazingira.

Kuhusu kukauka kwa mto ‘Thagicu’ mtunzi anatuundia taswira ya jinsi tukio hilo lilivyo baya na la kuhuzunisha. Anaandika:

Macho yangu
Yanapoona hayo mabonde ambayo

Yamejaa mchanga mweupe

Akili yangu

Huona vidonda virefu ambavyo

Vimejaa usaha

Moto wa uchungu (uk. 61)

Matumizi ya usambamba pia yanasaidia katika kukoleza hisia za mtunzi kuhusu matokeo ya upujuaji wa mazingira. Kuna usambamba baina ya ubeti wa kwanza na wa tatu, wa pili na nne. Kauli hisishi kama vile: “nakuhurumia!”, “Hudondokwa na machozi”, “Huona vidonda virefu”, “Ninaona vipele vyaya surua” pia yanahimili hisia za mtunzi kuhusu hali ya mto wenyewe.

Mbinu hizi zinasaidiana katika kuyaweka wazi maudhui, kupitia mfano huu wa mto ‘Thagicu’. Kwa pamoja, zimelenga kumsisimua binadamu juu ya hatari iliyopo katika kuyaponza mazingira yake kwa kumuundia picha ‘halisi’ akilini mwake. Huku kuhisisha kitaswira kunayajenga kwa ufasaha zaidi maudhui yenyewe.

Taswira ni mbinu yenyeye uwezo sana katika kugusa hisia kama ikipangiliwa vyema, kwa uteuzi wa msamiati hisivu zaidi. Matumizi dhahiri zaidi yanapatikana katika diwani ya Karibu Ndani (1988) katika shairi ‘Nondo’. Akieleza kuhusu usiku wa mauko ya nondo mtunzi anasema:

Juu ya meza kuna msitu

Wa vitabu vyaya manabii

Ni usiku. Taa inawaka

Mwanga (uk. 13)

3.3.3 Usambamba

Mbinu hii imetokea kupitia urudiaji wa baadhi ya miundo na mawazo mazito kwa urudiaji wake katika shairi lile lile. Katika ‘Thagicu’ (uk. 61), kwa kutaka kuonyesha hatari ya kupujuka kwa mazingira, mbinu hii imetumika. Baina ya ubeti wa pili na wa nne kuna:

Macho yangu

Yanapoona haya mabonde

Huona vidonda virefu...

.....
Ninapoona Koonyo na siili

Hundondokwa na machozi

.....
Ninapoona hayo mawe

Ninaona vipele vyasurua

Kuna mwendelezo wa fahiwa ya unyeti ule ule na hivyo kuzua usambamba unaoshadidia hali ya huzuni iliyopo katika tukio hilo. Mbinu hii inasaidiana sana na taswira zinazojengwa kama tulivyocleza hapo juu. Katika shairi ‘Mkalitusi’ (Uk. 67) pia kuna usambamba baina ya beti zake tano za mwanzo. Kuna urudiaji wa kauli “moyo wangu”:-“unashangilia” (ub.1); “unaridhika” (ub.2); “unakushukuru” (ub.3) “unasema asante”. (ub.4); “unakupigia makofi”. (ub.5).

Urudiaji huu unaleta hali ya kuendeleza hisia zile zile za kufurahia manufaa ya “mkalitusi” na hapo kukoleza wazo kuwa mkalitusi una manufaa makuu. Udhamini unaokabidhiwa “malitusi” pia unajotokeza kupitia matumizi ya uhuishi unaopewa mti wenyewe. Katika shairi nzima, mtunzi anauongelesha mti huu kama kwamba ni binadamu.

Ufuatishaji wa mtiririko ule ule unaozua usambamba unaonekana katika shairi ‘Mimi, Mto Nairobi’ (uk.63) ambapo mshairi anawatambulisha wachafuzi wake. Hili ni katika ubeti wa kwanza na ule wa pili. Tashihisi inatumika pia katika shairi hili kwa kufanya mto kuongea. Hapo mbinu hizi zinachangiana katika ujengaji wa maudhui.

3.3.4 Msisitizo Bayani

Ili kuhisisha kuhusu swala la mazingira, kuna matumizi ya mafungu fulani fulani yenyε uzito nkuu kimaana. Kwa Mfano, katika 'Okidi, Piga Ukelele' (2001) kunatokea kiunzi cha maneno yasiyoelezwa zaidi:

Si halali
Si haki
Ni maonevu
Ni dhuluma
Ni haramu...(uk.65)

Kauli hizi zinatilia nguvu swala kuwa uharabu dhidi ya mali asili haufai, ni haramu. Matumizi ya swalι la balagha (ub. 3) yanasaidia pia katika kufanya thabitι kauli za utetezi anazoendeleza. Swalι hili lina athari ya kufikirisha zaidi.

Katika 'Mimi, Mto Nairobi' (2001) katika kueleza vichafuzi vya maji ya mto Nairobi mtunzi amesomba pamoja kauli zisizotolewa maeleo:

Kwa mafuta
Kwa makopo
Kwa tairi
Kwa talimbo ...(uk.63)

Maudhui haya yamejengwa pia kwa lugha inayothamini sana mali asili ambayo inaangaliwa kama kiini cha uhai wa mwanadamu. Hili linathibitika katika "Bwawa la Ithanje"(uk. 69) ambalo linaambiwa:

Mpigo wa moyo wangu
Unakuunga mkono
Katika ndoto yako
Ya kuutetea uzima
Na uhai wa familia nzima...(uk.69)

Katika kushughulikia mazingira, mtunzi amefuata mkondo mahususi sana. Kwa mfano, anapozungumzia mti anataja aina fulani mahususi ya mti. Vivyo pia na mito na bwawa. Mbinu

za lugha zilizotumiwa, kwa hiyo, zililengwa na kuhusishwa na vitu mahususi na si kwa ujumla wake. Upekee huu unavutia dhati katika kutambua hali ya mazingara.

3.4 UTAMADUNI

Baadhi ya mashairi katika Bara Jingine, yanaonyesha nafasi na manufaa ya kuuendeleza utamaduni wetu. Yanadharau tabia ya kuandama yale ya kigeni na kuutupilia uasilia. Maudhui haya yamekuzwa kwa kuangaza thamani ya kile cha kiasili. Inatwaza utamaduni pamoja na mbini zake za kupambana na maisha huku ikiangaza hasara itokanayo na kuandama ugeni.

Mashairi haya yameteua msamiati na mafungu mahsusisi yanayothamini asili na mapokeo. Kuna matumizi ya mafungu kama vile: “mwashi mahiri” (uk. 45), “tiba” (uk. 47), “jabali” (uk. 47), “nyonza” (uk 51); ambayo yanarejelea asili yetu, kama nguzo thabiti. Kwa mfano, katika ‘Mwashi Mahiri’ mshairi anakiona kile asilia kuwa kijenzi maarufu cha hali na maisha yetu.

Anaandika:

.... Wewe mwashi mahiri
ujengaye miili thabiti
Ikawa kama mgome ya mawe...(uk.46)

Katika kuonyesha kuwa uasilia wetu unakabiliwa na tisho fulani, kuna matumizi ya vifungu kama vile: “kujinusuru” (uk. 44) katika shairi ‘Wanabiashara Barabarani’, “muuaji” (uk. 45), “pigana” (uk.45), “usasa unaoua” (uk 45), “kulindwa” (uk. 46), “mashambulizi” (uk. 46) katika shairi ‘Mwashi Mahiri’, “maradhi” (uk. 48) katika ‘Tiba’ na “utemeaji mate” (uk. 52) katika ‘Ni Sumu kwa Watoto’.

Katika kujaribu kuisisimua hadhira, mtunzi ametumia msamiati huu ambao una nguvu ya kuwatanabahisha juu ya uviziaji unaofanywa dhidi ya utamaduni wetu. Kuna msamiati pia unaogusia mali na amali zetu za kiasili ambazo ni bora na stadi. Baadhi yake ni: “mtama”, “wimbi”, “mawele”, “muhogo”, “viazi”, “wanga”, “viazi vikuu”, “twiga”, “nduma”, “pori”,

“simba”, “heroe”. Hizi zinalinganishwa na kope za kigeni k.v. “yenii”, “krona”, “dochimaka”, “lira”, “fauni” n.k. Katika kusifu amali za kiasili mtunzi anaandika katika ‘Tiba’:

Unapokula muhogo
Au viazi, ndizi au wanga
Unaimarika misuli
Hivi kwamba, bingwa
Unapokumbatia maradhi
Unayavunja vunja mifupa....(uk. 47-48)

Huku akiuponza usasa anasema, katika ‘Ni Sumu kwa Watoto’:

Ni sumu sumu hatari....
Mazoea yako tenganishi
Ya kunywa ‘moja baridi’ ... (uk. 49)

Hatimaye katika ‘Ngoi wa Waimbaji’ mtunzi anasema:

Tunajali taifa kugeuzwa pipa
La kupokea uoza wa ulimwengu
Ili nchi ivune dola na fauni ... (uk 52)

Mbali na uteuzi na upangiliaji wa vifungu vyta maneno, maudhui haya yamepigwa jeki na upangiliaji wa shairi zima la ‘Mwashi Mahiri’ (uk 45). Shairi hili badala ya kupanga beti kwa njia ya kawaida limetokea kukuza taswira kupitia mchoro. Titi linalosifiwa limeumbwa kimchoro kufanya thabiti maelezo ya maneno.

Tamathali mbali mbali zimetumiwa pia. Zimetumika kueleza kwa mguso fulani haja ya kuthamini na kuuheshimu uasilia. Baadhi yake ni kama vile:

3.4.1 Takriri

Mbinu ya takriri imetumiwa ama kukariria umaarufu wa kile cha kiasili au pia kukariri uharabu wa kile cha kigeni. Kwa mfano, katika ‘Mwashi Mahiri’ (uk. 45) kuna takriri ya kauli “Pigana titi pigana”. Kauli hii inautia shime uasilia. Hii ni taashira ya kumpa daro msomaji azidi

kuwana kuenzi kile cha kiasili kama vile maziwa ya chupani (kutoka dukani) kuna takriri ya: "Ni sumu, sumu..." , katika, shairi 'Ni Sumu kwa Watoto' (uk. 49). Kuonyesha jinsi uparamiaji wa mambo ya kuletwa na wageni unavyoweza kuwa hatari kwa maisha na uhai wetu. Yumkini hili ni kwa sababu ya mtunzi kuadhiriwa na maisha ya kienyeji katika jamii ya kijadi. Anaopinga usasa.

Katika shairi 'Ngoi na Waimbaji' (uk.51), fungu "Sijali, kwa nini nijali..." ambapo fanani anakariri kuwa hajali wanajamii wakifurahia vile vya kiasili k.v:

... Johari za ardhi na anga...
...Vito vya maji na pori...
... mbio za nduma mawindoni.... (uk.51)

Hili ni kwa mujibu wa kuwatia shime wanajamii wazidi kujipumbaza kwa vilivyo vya kiasili badala ya kungangania vya kigeni. Yeye anachukizwa na

...Watoto wa kike
Wakikanda miili ufukweni
Ili nchi ivune lira na dochimaki....(uk.52)

Katika msisitizo wake juu ya umuhimu wa kile cha kiasili, mbinu hii ya takriri inasaidiana na usambamba unaojitezea baina ya beti za wahusika waliomo. "Ngoi" anarejelea mawazo yenyе mshabaha mkubwa kutoka ubeti hadi mwingine huku "waimbaji" wakikariri ubeti ule ule katika kumwitikia.

3.4.2 Uhuishi

Utamaduni au vitu vya kiasili vimepewa hadhi kwa kuhuishwa. Anakipa hadhi kile ambacho ni cha kiasili kusudi kuvuta makini ya wasomaji. Titi katika 'Mwashi Mahiri' (2001) linaongeleshwa kama kwamba ni mtu. Tena linapewa sifa ya kuwa 'mwashi' awavyo mwanadamu. Haya ni kwa nia ya kutaka kuutwaza uwezo wake ulingane na ule wa mwanadamu. Chupa pia inapewa sifa hiyo. Asemapo:

Chupa!

Muuaji vijijini!

Mwenye njama za wivu (uk. 45)

Ana maana ya kuonyesha uwezo mkubwa wa vile vya kigeni katika kuhasiri.

Uhuishi hapa umenata vizuri katika kuhimili maudhui.

Tunapolichunguza shairi hili, tunaona kuwa mbali na matumizi ya tashihisi, mtunzi anakoleza maudhui yake kwa matumizi ya sitiari ya kimchoro. Kuna pia matumizi ya usambamba na takrini zinazosheheni urudiaji wa kauli kama vile “pigana, titi, pigana”. Mbinu hizi zinachangiana sana katika kuyakuza maudhui kwa kuwa zote zinaleta athari fulani ya kimsisitizo.

3.4.3 Usambamba

Mbinu hii imetumika kwa ufuatishaji wa mafungu yanayokariri ujumbe unaoshabihiana katika mashairi. Mbinu hii imeyatawala mashairi haya kusudi kukariri uthabiti wa utamaduni.

Katika shairi ‘Mwashi Mahiri’(uk. 45), ubeti wa nne na ule wa tano ni mwendelezo wa wazo linaloshabihiana la kulihimiza titi kupigana dhidi ya usasa, matumizi ya chupa.

Ubeti wa nne:

Pigana titi pigana

Pigana dhidi ya ulafi

Wa wanabiashara wajanja

Pigana dhidi ya uchafu

Ubeti wa tano:

Pigana titi pigana

Pigana na wale ambaao

Hukuchukulia kuwa pambo...(uk. 45-46)

Usambamba hapa unasiaidiana na mbinu ya sitiari ya kimchoro katika kuyateka makini ya msomaji kusudi alimakinikie kwa dhati swala linaloendelezwa. Ziwa la mama huthaminika zaidi kwa mujibu wa mapokeo ya jamii ya mwandishi.

Shairi 'Tiba' pia linaonyesha matumizi ya mbinu hii baina ya ubeti wa pili na wa tatu. Beti hizi zinakariri wazo la kumenyana ili kujihami dhidi ya mabaya.

Ubeti wa pili

Jikakamue wewe tiba

Pigana kote Afrika....

Unaangusha chini adui

Ubeti wa tatu

Pambana, wewe jasiri

Hudumia mashambani...

Unapokumbatia maradhi

Unayavunjavunja mifupa....(uk. 47)

Katika kulihimili wazo hili, mbali na usambamba kuna pia matumizi ya tashihisi ambapo "mchanganyiko wa maji, chumvi na sukari" unaongeleshwa kama kwamba ni mwanadamu. Mchango wa mbinu hizi mbili ni muhimu katika ukuzaji wa mjaudhui yenye.

Katika shairi 'Ngoi na Waimbaji' kuna usambamba unaodhihirika waziwazi. Beti za ngoi zina mshabaha mkubwa kwa kukariri maelezo yale yale, kuhusu asiyoyajali, huku waimbaji wakizidi kuitikia kwa kauli ile ile isiyobadilika:

Hatujali, kamwe hatujali

Bora mzinga wa utalii urinwapo

Umma ugawiwe vizuri asali (ubeti 2,4:51)

Beti za 'Ngoi' zote zinaanzia kwa "Sijali, kwa nini njali..." na kisha kuendelea kueleza amali mwafaka zinazomvutia, za kiasili. Humu mtunzi anakisifu' kile cha kiasili. Mbinu hii ya usambamba inasaidiana na uteuzi wa msamiati kutoka mazingira ya kienyeji ya mtunzi. Kuna

matumizi ya kauli kama vile: "mzinga", "asali", "twiga", "duma", "viazi vikuu". Msamiati huu umetumiwa kuangaza zaidi kuhusu kile cha kitamaduni katika jamii ya mtunzi.

3.4.4 Sitiari

Matumizi ya sitiari kukuzia maudhui ya uasilia yameshamiri pengi. Kwa kutaka tuhisi uwezo wa amali za asili yetu, mtunzi ameitumia tamathali hii kama kifananishio chenye uzito mkubwa. Katika 'Tiba' (uk 47) mtunzi ameunasibisha "mchanganyiko wa maji, chumvi na sukari" na vitu kadha. Anaandika:

... jikakamue, wewe Tiba...

Pambana, wewe jasiri (uk. 47)

Huu ni ulinganishaji unaolengwa kuzivumisha amali za kiasili na hivyo kumiwathiri msomaji.

Mbinu ya usambamba pia imesaidiana na sitiari katika shairi hili kwa kukuza mawazo yenye kushabihiana katika beti mbali mbali. Hapo mbinu hizi za kifani zinachangiana katika kuyakuza maudhui yenye. Kuna pia uteuzi wa msamiati wa mazingirani mwa mtunzi. Msamiati huo ni kama vile: "mtama", "wimbi", "mawele", "mhogo", "viazi" n.k. Msamiati huu unahimili pia swala la kuuthamini utamaduni.

Kuna pia matumizi ya sitiari za kimchoro ambayo itashughulikiwa kwa kina katika sura inayofuata.

Kwa jumla, mashairi yanayobeba maudhui haya ni machache lakini yaliyosheheni vipengele anuwai vya lugha, ambavyo vinabaini na kuiweka wazi maudhui yenye. Ujenzi wa maudhui yenye umekita kwenye ukariri wa sifa za amali za kiasili, na papo hapo kuonyesha hatari za kuandama vipyta vya ugenini. Maudhui haya yamejengwa kwa ulinganisho baina ya amali za pande hizo mbili.

Hata hivyo, jambo la kutiliwa makini ni kwamba mtunzi ana msimamo wa kukashifu chochote cha kutoka ugenini na kutukuza chochote cha kiasili. Mkabala huu unatilia shaka dhati yake katika kuichunguza jamii ya wakati wake ambayo imeyathamini mabadiliko ya hali za kimapokeo na kukubali maendeleo ya kisasa. Hapo amekwepa hali halisi ya jamii yake.

3.5 DHULUMA YA KIMAPENZI

Maudhui haya yamekuzwa kuitia usawiri wa wasichana wachanga wanaopotoshwa na maisha kuitia kwa wanaume wanafiki. Ovu hili linakuzwa kufikia pale tunapoonyeshwa msichana kuhangaika punde mwenziwe akisha muacha katika hali mbaya ya uja-uzito au maradhi. Hiyo ndiyo hatima ya mahusiano yanayokuzwa humu. Majuto na kuhangaika kwa wasichana hawa ndicho kilele kinachotumiwa kutuashiria ubaya wa tendo hili. Maudhui haya yameshughulikiwa katika mashairi matano tu katika Bara Jingine ya ‘Giza Mbele’ (uk.26); ‘Pamela’ (uk.29); ‘Flora na Wenzake’ (uk.33); ‘Mimi, Monika’ (uk.37), na ‘Nakumbuka Ulivyokuwa’ (uk.76).

Vipengele vya lugha vimesaidia sana katika uendelezaji wa maudhui haya. Kwanza, uteuzi wa msamiati wake unatufikisha kwenye mawazo ya kutanabahi na kutafakari hali ya kuhuzunisha ya tabia yenye. Mtunzi ameteua msamiati unaotuangazia uchanga na uzuzu wa wanawake wanaoshirikishwa katika tabia hii ya uzinzi. Matumizi ya msamiati kama huu yanatuashiria kuwa kushirikishwa kwa kundi hili katika mahaba ni dhuluma kubwa dhidi yao. Wahasiriwa hawa ni wachanga na wasioelewa maana ya kushiriki mapenzi. Kiwango cha umri na ufahamu wao kinatuelekeza kutilia shaka hiari yao katika kushiriki katika ngono.

Kuna pia uteuzi unaoonyesha hukumu na ukuu wa wanaume dhidi ya hao wasichana. Unatuonyesha pia jinsi wanaume hawa walivyo dhalimu na walivyokosa utu.

Msamiati huu unasaidia kuisisimua hadhira ihisi kuwa tabia yenyewe haina budi kuepukwa. Hii ni hatua muhimu katika kujenga maudhui yenyewe. Misano ya msamiati unaoangaza upotovu unaopingwa ni kama vile: "wanafunzi", "windo", "mja-mzito-mtoto" (uk. 26: 'Giza Mbele') na "mwalimu mkuu, Uoza", "mburukenge", "nyegere", "bweha" (uk. 33: 'Flora na Wenzake'). Tunaona kuwa baadhi ya huu msamiati unatokana na mazingira ya mtunzi na hivyo kuonyesha jinsi alivyoathiriwa na hali iliyopo katika jamii yake, kimtindo na kimaudhui pia.

Kupitia kwa msamiati huu mtunzi anadokeza juu ya uovu wa tendo lenyewe pamoja na hasara inayonasibishwa nalo. Msamiati huu unagusa hisia na kufikirisha zaidi kuhusu mahusiano ya aina ile. Mahusiano ya aina hii, baina ya wasichana wachanga na wazee walokomaa ni jambo linalopingana na mila na mapokeo ya Kiafrika. Kwa hiyo mtunzi anaiangaza jamii yake ya kienyeji katika maudhui haya.

Mtunzi pia ametumia tamathali mbalimbali katika kuyasana maudhui yake. Baadhi yake ni kama zifuatazo:

3.5.1 Tashbiha

Tamathali hii imetumika pengi hasa kuwalinganishia washiriki na viumbe vingine wanavyoshabihiana navyo kitabia. Kwa mfano, katika 'Giza Mbele' kuna:

Benzi jekundu

Limetulia tuli

Likisubiri **kama** chatu (uk. 26)

Hii inadokeza kuhusu ubaya na hatari ya wanaume wanaowahangaisha wasichana wadogo. Kwanza kabisa, "benzi" linalinganishwa na nyoka mbaya sana, "chatu" anayeweza kummeza mwaniadamu mzima mzima. Ulinganishaji huu unamulika hatua fulani za kimaendeleo ya kisasa ambazo ndizo visababishi vyta baadhi ya maovu tunayoyashudia siku hizi. Wazo hili

linathaminiwa na hali iliyopo katika jamii yetu ya sasa. Maovu mengi ya kijamii yanaandamana na maendeleo ya kisasa.

Kuna pia “mkono mkongwe **kama** karne” (uk. 27) katuonyesha picha ya alivyo mzee mwanamme aliyemchukua msichana wa darasa la nane. Tunavyoshuhudia katika jamii ya kisasa, wasichana wachanga wanaangukia mapenzi ya wanaume wazee kwa kuandama malengo tofauti; utajiri au pesa. Hili ni ovu lililokolea katika jamii ya sasa, na ile ya mtunzi.

Kuhusu uchafuzi aliofanyiwa Pamela na wabakaji wake, mtunzi ametumia tashbiha:

Huku maisha yako
Yamechafuliwa
Kama nguo nadhifu
Ilivyovamiwa na mwani....(uk.30)

Dondoo hili linatuangazia pia jinsi maisha ya wasichana kama kundi la jamii linalodhulumiwa, wanavyoishilia kuharibiwa maisha na wanaume wenye uchu wa mapenzi.

Mbali na matumizi ya tashbiha kuangazia uovu wa tabia yenyewe, kuna pia matumizi ya msamati mzito na wenye kuibua hisia zinazotafakarisha kuihusu tabia hii. Kwa mfano mtunzi anataja: “mbwa mwitu”, “funo-mpweke”, “mateke”, “mwanguko”, “mkasa”, “yamechafuliwa”, n.k. Huu ni mwendelezo wa ukuzaji wa maudhui haya, ya dhuluma ya kimpenzi.

3.5.2 Tashhisi

Ili kuonyesha uzito unaohusishwa na vitu, au tabia fulani, mshairi amevipatia vitu hivyo sifa ya kutenda kama binadamu. Katika ‘Giza Mbele’ tunaonyeshwa jinsi msichana alivyokuwa katika hali mbaya baada ya kushiriki mapenzi na *mzee wa Benzi*. Tunaambiwa “maswali yanamchoma akili” (uk. 27), kuonyesha jinsi alivyoishi kujijutia baadaye.

Katika ‘Flora na Wenzake’ kuna: “Jua lachomoza uso likitabasamu” (uk. 33) Jua linalotabasamu ni taashira ya uchanga wa wasichana wenyewe. Imelengwa kuibua hisia tunapotichuliwa jinsi wanavyohangaishwa na Mwalimu- Mkuu, Uoza. Uchanga wa wasichana hapa unalinganishwa na kuchomoza kwa jua. Hali kadhalika:

Amri nyekundu
“Ingia ofisini”
inatupa dhoruba
inayomgonga mtoto...(uk. 34),

ni mfano wa tashhisi ambayo inatwaza amri ya Mwalimu –Mkuu ikaonekana kama binadamu.

Pamoja na tashihisi, katika dondo lenyewe, tunaweza kuona matumizi ya litifati (nukuu) ambapo kuingia ofisin mwa mwalimu mkuu kunatoa taswira ya mwanzo wa matatizo ya wasichana. Hii ni kwa kuwa ofisi yenyewe inatoa huduma tofauti, ufunzaji wa “utu uzima”. Mkumbo wa mbinu hizi kwa pamoja unatoa hali ya kitaashira kuonyesha jamii ya sasa, ya mtunzi, ilivyovuruga mambo. Walio na vyeo wanavitumia vyeo vyao katika kuwaangaisha walio chini yao.

Monika katika ‘Mimi, Monika’ (uk. 38) anataja: “Mauti yamenisimamia kidete”, ili kutupatia picha ya jinsi alivyoharibikiwa baada ya kupashwa ugonjwa na tabia yake ya kimalaya. Kuonyesha majuto yake, Monika anasema:

Naisikia sauti yangu
Ikilalamika kwa machovu (uk. 39)

Kulalamika kwa sauti yake kumelengwa kutuangazia juu ya ukuu wa majuto yanayowafikia wale wanaojiingiza katika maisha haya ya kikahaba. Yumkini mtunzi anataka kuonyesha, kupitia kwa malalamiko ya Monika, kuwa tabia yenyewe haifai japo inaendelea katika jamii. Msukumo unaoletea tabia yenyewe aghalabu huwa ni matatizo ya kijamii, japo mtunzi hakuliangazia hili. Hapo tunatoa kauli kwamba mtunzi angeonyesha msukumo unaovyaza tabia kama hii inayodhihirika katika tungo zake.

3.5.3 Taswira

Hali ya mambo inakolezwa kwa uchoraji wa picha ya mandhari anuwai ya yanayozungumziwa. Msomaji anafanywa kuiona akilini mwake picha na mkao wa mazingira fulani ya matukio kusudi kuhimili fahiwa inayopitishwa.

Kuhusu alivyokuwa Monika wakati akiingizwa katika ukahaba tunaelezwa:

Tambarare kifuani

Bila viatu miguuni (uk. 39)

Dondoo hili linajenga taswira inayotuelekeza kuona jinsi alivyopotoshwa akiwa mchanga na pia hali yake mbaya ya kupungukiwa. Hapa tunaona kuwa kuna nguvu mbili changilizi katika upotovu wa mhusika, kutojua na pia hali duni ya maisha. Hivyo tunavutwa kuona kuwa hii ni dhuluma dhidi yake, kwa kuzingatia kuwa yeye anasukumwa kwenye ukahaba na nguvu asizonasatua dhidi yake. Hivi ni vichochezi vikuu katika jamii ya sasa ambayo inaelekea kushindwa kudhibiti tabia potovu ya ukahaba.

Picha ya uharibifu wake inakolezwa pia na maeleo kuwa:

Kama mlango wa umma

Nimeguswa na viganja milioni

Kama jumba la mikutano

Nimetembelewa na halaiki ya watu (uk. 37)

Pamoja na kuundiwa taswira juu ya mhusika huyu, kuna pia hali ya usambamba katika dondoo lenyewe. Urudiaji wa “kama...” unasaidia katikauzuaji wa piche inayolengwa na mwandishi.

Katika ‘Giza Mbele’ (uk. 26), tunaundiwa piche ya hali ya anga na wakati wa siku msichana alipochukuliwa na mzee wa Benzi. Tunatajiwa:

Mawingu nyuma ya vilima

Yanawaka moto mwekundu

Na kuipa anga

Sura ya damu

Hii ni taswira ya mandhari ya wakati maovu kama haya hutekelezwa. Ni mambo maovu yafanywayo wakati wa giza. Kwa hiyo ni hatari kuyashiriki, kama inavyoashiriwa na matumizi ya kijazanda ya neno 'damu'.

Usimulizi mwingi hapa ni wa lugha inayomnasa akili msomaji ahuzunishwe na kitendo hiki, kupitia matumizi ya vipengele anuwai vya lugha.

Maudhui haya japo hayakuendelezwa katika mashairi mengi yametokea kuangazwa vyema hasa na usawiri wa makundi mawili yaliyobaidika katika mambo mengi, wanaume wazee na wasichana wachanga. Matumizi ya lugha inayowasawiri kuwa mbali mbali kihulka inakoleza uzito wa maudhui yenye. Hali kadhalika, matokeo, na sifa mbaya za tendo lenyewe, yameangazwa vyema pia kupitia matumizi ya lugha.

Hata hivyo, tungo nyingi tulizoziona kuhusu maudhui haya hazidhihirishi wazi wazi kichochezi cha tabia yenye. Hili huwa ni muhimu iwapo maudhui yenye yataoanika na jamii halisi. Mtunzi hakuonyesha mshawasha wa tabia anazozia ^{utawandani}inisha. Hali kadhalika, mtunzi anaonekana kuegemea upotoshaji na dhuluma ya upande mmoja tu. Kuna pia hali ya wanawake wazee kuwaangaisha wavulana wachanga. Ili kuangaza picha halisi ya jamii, ilifaa mtunzi aangaze pande zote mbili.

3.6 HITIMISHO

Katika sura hii tumeainisha maudhui manne yanayojitokeza katika diwani hizi. Imebainika kuwa diwani ya Mchezo wa Karata imetawaliwa na maudhui mamoja tu, maudhui ya siasa. Tumeweza kuainisha maudhui ya siasa, mazingira, uasilia na dhuluma ya kimpenzi katika Bara Jingine. Vipengele mbali mbali vya lugha vimejitokeza kuyapitisha na kuyahimili maudhui haya.

Kwa kiimbo kikali sana na uziada wa chukizo, mtunzi amejitokeza kuteta dhidi ya dhuluma katika jamii. Uteuzi wake wa maneno na vifungu mbali mbali umedhihirisha hili. Ametumia tamathali anuwai kuyapa mawazo yake mguso unaofaa, na pia kuumba baadhi ya ujumbe nyeti.

Kwa kutaka kukoleza ujumbe wake mtunzi amejitokeza na maudhui machache tu. Hili lililetea hali ya kuteua msamiati usio sambazi sana. Ametumia msamiati unaoshabihiana sana katika karibu mashairi yote. Msamiati mwangi umeteuliwa kutoka mazingira ya kiasili tu. Hata maudhui ya kisiasa, kwa kiasi kikubwa yamejengwa na matumizi ya kauli zinazopigia taswira ya mazingira ya kiasili. Uteuzi wake umefaulu katika kuhimili ujumbe kuwa ubwana, unafiki, uharibifu wa mazingira hauwezi kudumu iwapo maisha yataendelea. Pengi mtunzi anataja “ndoto” yake ya hali kugeuka.

Tumeona kuwa diwani ya Mchezo wa Karata ina maudhui mamoja tu. Hii si kwamba ni dhaifu bali ni fanifu katika kusawiri maudhui aliyolenga mtunzi, kwa wakati huo. Kila shairi japo kuhusu maudhui yale yale, lina mkabala wa kipekee na unaokubalika na kulitambulisha kivake. Jazanda na taswira zinazojitokeza katika mashairi mbali mbali zinajisimamia. Hata hivyo inajuzu tuseme hapa kuwa mtunzi ameyakwepa matukio mengi yaliyomo katika jamii yake. Tunaona usinyu uliyopo katika kuyazingatia maudhui yake. Yeye amekita tu kwenye mhemko wa kuwapinga walio mamlakani. Hili linaonekana hasa katika maudhui yake ya kisiasa ambayo ndio yamechukua nafasi kubwa katika diwani zake.

Kwa jumla, uteuzi wa msamiati pamoja na ule wa uteuzi wa maudhui pia unaegemea jamii ya mtunzi. Pengi anatetea haja ya uumbaji wa mazingira bora ya kuishi. Msamiati mzito umesaidia katika ujenzi wa kiimbo kikali cha utetezi. Aghalabu lugha iliyotumika ni ya kiwango rasmi isiyoingiliwa na misimbo au sajili za kimitaa wala lahaja.

SURA YA NNE

SITIARI ZA KIMCHORO NA VIPENGELE VINGINE VYA KIFANI

4.1 UTANGULIZI

katika sura hii tutathmini jinsi vipengele vya ziada ya lugha vinavyotumiwa katika ujenzi wa maudhui yanayojitokeza katika diwani za Mchezo wa Karata na Bara Jingine. Tutachunguza jinsi vipengele hivyo vinavyojengeka pamoja na athari zinayoleta katika kuyapambanua maudhui.

Vipengele tutakavyoshughulikia ni: sitiari za kimchoro, mandhari na toni. Tutajaribu kuchanganua jinsi vinavyojitokeza katika muktaba wa kishairi. Tutatoa mifano ya usawiri wake katika mashairi mbali mbali, hasa kwa kuegemea maudhui kadha yanayokuzwa na mwandishi. Hatimaye tutatoa hitimisho letu kuhusu uwajibikaji wa vipengele hivi katika tungo zilizomo.

4.2 SITIARI ZA KIMCHORO

kwa hali ya kuwa ushairi huru huwasilisha mchanganyiko usiobagua wa mbinu zake za upangiliaji. watunzi wanazidi kuzua mbinu mpya za kuzipangilia tungo zao. Kwa kiwango kikubwa, maumbo haya yametokea kutawala ushairi wa kisasa katika pembe nyingi za ulimwengu. Watetezi wake wamekariri kuwa ushairi huu una ruwaza zake na kuwa hauna chochote cha kushtukiza. Ilivyo, washairi hawa bado hukubali haja ya kuumba aina mpya za kuoanisha umbo na yaliyomo. Uziada wake ni kuwa, kaida yake hutaka kuwe na maumbo mengi zilivyo mada. Kwa sababu ya uhuru mwingi uliopo, kwa hivyo, kaida na mipaka iliyopo huwa ni ya kujizulia.

Kama hatua ya kimaendeleo ushairi unaofuata mkondo huru ulifiki hatua ya kuunganisha maandishi na picha, kukawa 'mashairi – picha'. Kwa mujibu wa N. Abiud (1998):

Mashairi picha yameundwa kutokana na muungano wa aina mbili za sanaa: sanaa ya uchoraji... na usanifu wa kiufasaha (uk.50)

hapa mtunzi huyaweka mawazo yake katika picha fulani ya kuonekana na ambayo ina thamani yake ya kisanaa. Huzua aina ya mchoro kuitia upangiliaji wake wa maneno, mchoro ambao huchangia faiwa zianazojengwa.

E.V. Roberts (k.h.j) anasema kuwa ushairi wa aina hii si wa hivi karibuni na kuwa:

Wachina wameutumia kwa maelfu ya miaka na kuna mifano inayopatikana leo kutoka Ugiriki ya kale (uk.736 – 737)

(Tafsiri yetu)

Anaendelea kueleza kwamba ushairi huu katika mapokeo ya Waingereza, unaweza kuwekwa tarehe yake katika karne ya kumi na saba. Huu ni wakati ambapo washairi mahiri waliyapamba mashairi katika maumbo ya miraba, duara, pembe tatu, nyota n.k Tungo hizi zenyenye maumbo zilithaminjwa sana kuwa za kirazini zaidi.

Hata hivyo nyingi hazikuonyesha uhusiano wowote wa kutajika baina ya 'umbo' na 'fahiwa' ya shairi lenyewe. Ni chache sana zilizoonyesha sifa ya kusaidiana baina ya umbo hilo la kuonekana na maana.

Mashairi ya aina hii yalifilia na yamepata kufufuliwa tena baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Hapo ndipo ushairi wa kuonekana (visual) uliporejea tena kwenye ulingo wa kifasihi. Awamu iliyofigiwa kupitia hii vuguvugu mpya iliitwa 'ushairi wa ki-umbo' (concrete). Ushairi huu ulitegemea mbinu za uwasilishaji k.v mpangilio wa kuonekana wa maneno, mistari na nafasi zilioachwa wazi kuliko msisitizo kwa yaliyomo. Ushairi huu ulionekana kuwa uliowakilisha muungano baina ya maandishi na upakaji rangi au mtindo wa kimchoro.

Anavyoeleza Roberts (k.h.j), kwake msisitizo juu ya umbo ndio huwa nyenzo na madhumuni kuu ya uumbaji. Lakini tunataka kueleza kuwa umbo haliwezi kuwa muhimu kuliko wazo linalobebwa. Umbo huwepo kwa ajili ya kupitisha maudhui na sio kinyume. Kwa hiyo, sitiari za kimchoro, kama ufundi wa kuyaunda mashairi zinasa kuchukuliwa kama nyenzo tu, na wala madhumuni.

Tunapochanganua muundo wa shairi tunamulika ruwaza za mpangilio wake kama sehemu ya fani yake. Kuna madai kuwa hili husaidia katika ung'amuaji wa maana ingawa madai haya hupingwa kwa kauli kwamba maana ya ndani ya utungo haiwezi kuonekana kwa macho, mbali hutokana na ung'amuzi wa kiakili unaotokana na usomaji makinifu.

Mawazo ya E.E. Cummings (Diyanni, R:1994) kuhusu madai haya ni kwamba tunachoona tayari kinawasilisha ujumbe kupidia upangiliaji wake, na hivyo kuna muungano kati ya umbo na yaliyomo, muundo na wazo. Kwa hiyo msisitizo wa kiuoni (wa kile tunaachoona) ni muhimu katika ushairi, kwani huathiri na kuelekeza usomaji wetu.

E.V. Roberts (k.h.j.) anasema kuwa:

Katika kusoma ushairi wa picha na ule wa kiumbo hufuatwa wiano baina ya picha na maneno (uk.759)

(Tafsiri yetu)

Alieleza kuwa umbo la shairi hutiliwa maanani kwa sababu maumbo haya huashiria maana kutegemea urefu mbali mbali wa mistari, matumizi ya nafasi ya karatasi n.k. Mawazo haya huenzi kauli kwamba muundo ni kigezo cha maana; si kitu huru bali huwajibika pamoja na elementi zingine za kishairi kuunda maana. Inachukuliwa kuwa muundo wa shairi, umbo lake ni sehemu ya lile shairi tunalolisoma; sehemu ya maana yake. Kwa mujibu wa mawazo kama haya, Abiud (k.h.j.) anaandika:

Picha inachangia maana kwa sababu yajenga taswira ya maono ambayo husaidia hadhira kuelewa vizuri kile mtu anachozungumzia (uk.50)

Na sababu ya madai kama haya utumiaji wa michoro au picha katika kuyapa sura mashairi zekuja kujulikana kama aina fulani ya sitiari. Huchukuliwa kuwa mbinu ya unasibishaji naapo maana hudokezwa na michoro wa kuonekana wa shairi. Hapo mbinu hii imeitwa sitiari ya kimchoro.

Hii aina ya taswira ambayo haijengwi kwa maneno tu, bali kwa picha au umbo halojitokeza kwa mujibu wa mpangilio wa tungo. Thamani yake huonekana kuwa mhimili muhimu zilivyo picha na michoro mingine katika vitabu vya kiakademia.

Limsingi, mvuto wa lile umbo linaloonekana huwa muhimu sana katika kuunda msimamo wa mengwa wa kazi yoyote ya kisanii. Usununu na hisia zake huathiriwa mwanzoni kabisa na zocha inayojitokeza. Aghalabu hili huathiri maamuzi na uelewa wa tungo yenewe. Kwa hiyo naumbo hayo ya kimchoro ni mojawapo ya fani ambayo mtunzi anaitumia kufanikishia naudhui. Ni mbinu inayosaidiana na zile zingine katika kuibua maana. Kama vile sitiari ya meneno hulifaa shairi katika kuashiria maana fulani, basi na sitiari ya kimchoro hutumika ivyo. Sitiari yoyote huwa na athari ya kuzua taswira yenyen urejelezi fulani wa maana. Maana hizi ndizo vijenzi vya maudhui.

Katika diwani za Mchezo wa Karata na Bara Jingine kuna mashairi yasiyopungua matano yanayofuata mbinu hii. Yumkini haya ndiyo mashairi ya kwanza katika ushairi wa Kiswahili kuonyesha sifa hii. Umbo la kila mojawapo lina mvuto wa pekee kwa macho ya msomaji. Kwa nafano, shairi ‘Mwashi Mahiri’ (2001:45) limeonyesha umbo la maziwa ya mwanamke.

Baada ya kulisoma tunapata kuona himizo kwa ‘titi’ azidi kupiga dhidi ya uchafu uwezao baletwa na ‘Muuaji’, chupa. Kwa mujibu wa umbo la shairi lenyewe tunaweza kukisia kuwa binadamu ndiye anayelengwa na shairi lenyewe anyonye titi asilia, la mama, na sio kutegemea maziwa ya chupa ambayo yanaweza kuwa yaliyochafuliwa. Ujumbe huu unahimiliwa na mchoro au umbo tunaloona la shairi lenyewe. Shairi hili linahimili maudhui ya utamaduni kwa njia hiyo ya kuzua mchoro huo ambao ni kama kifaa cha kusisitizia.

shiri ‘Boga’, Mchezo wa Karata, linaonyeshwa kimchoro na mduara kamili unaojipanga
miaka kurasa mbili za kitabu. Mduara huo umegawanywa kuwili na kurasa mbili hizo kila
zego likiwa na idadi ya maneno ishirini na nane. Kwa mujibu wa maelezo yake, msemaji
rawania wagawane ‘boga’ lao kwa sehemu mbili zilizo sawa. Kwa hiyo upangiliaji wa
maneno ya shairi lenyewe unapiga mwengo mawazo ya msemaji. Kugawika kuwili ni taashira
a kutopendelea uroho. Tunapong’amua lengo la shairi kwa mujibu wa maisha halisi, kuna
sisitizo wa kugawana sawia mali ya umma au mirathi ya taifa. Mchoro huo basi unasaidia
katika upitishaji wa wazo hilo, na hivyo katika lengo kuu la kudumisha usawa.

Shairi “Mruko wa Nyuki” (2001:20) ni refu sana na pia linaanza kwa upangiliaji wa maneno
katikati mwa ukurasa wa kitabu toka juu hadi chini. Hatimaye kuna hali ya mtanziko ambapo
maneno mengine yanaelekea kulia na mengine kushoto mwa ukurasa. Kisha safu ya kulia ya
maneno ndiyo inayoendelezwa tu, ya kushoto inakatika. Maelezo; yaliyomo katika shairi yana
mwelekeo kama huo.

Urefu wa shairi unaweza kuashiria wingi wa miaka. Tunang’amua kuwa shairi hili linaweza
kuashiria miaka ya mataifa ya ulimwengu kudhibitiwa na nguvu mbili za kiuchumi: ubepari na
usoshalisti. Hatimaye tunaonyeshwa kusambaratika kwa usoshalisti na kutawala ubepari.
Hapo tunasadiki kuwa mchoro ni taashira ya mwendo huo kwa jinsi maneo yenewe
yalivyopangiliwa. ‘Mruko wa Nyuki’ kabla ya kugawana tariki umeashiriwa na mapito ya
katikati mwa ukurasa, kwamba mataifa ya kiafrika yalifuata mkondo horomo usioegemea wala
ubepari au usoshalisti.

Mchoro huu unafaa sana katika uelezaji wa jinsi mtanziko wa mataifa ya kilimwengu
ulivyotokea wakati kabla na hata baada ya enzi ya ubishi baina ya mifumo hiyo miwili. Shairi
‘Nyumba’ (1997:17) linaonyesha mpangilio unaouumba nyumba ya kienyeji ambayo uvumbuzi
wa taashira yake unaweza kumaanisha nchi yetu sisi wenyeji wa Kiafrika. Nyumba
iliyoashiriwa bila shaka ni hadhira ya kihuku. Maelezo ya shairi yanadhihirini hili kwa:

Udongo kimano tuliorithi kutoka mama...

Nyumba ni mahali pa kujisetiri, na vivyo ndivyo nchi yetu, tulimozaliwa na mama zetu. Neno **nyumba** na mchoro ni jazanda inayoashiria maskani, hasa "taifa letu". Jinsi walioijenga **nyumba** walivyo na haki ya kuingia ndani yake, na ndivyo raia waliorithi au kung'ang'ania **nuru** wa nchi yao walivyo na haki kuishi humo. Shairi 'Dau Haliendi' (1997:32) pia linafuata **Kondo huo huo, wa kisitiari.**

Tuma tulivyoeleza mwanzoni basi, sitiari hii inachukua dhima ya unasibishaji kimchoro. **M**ichoro inayodokezwa na umbo ni mhimili muhimu wa maana na ujumbe zitokanazo na **zaelezo**. Michoro inayotumiwa inafasirika pia. Kwa mfano, jinsi neno nyumba ni jazanda ya **z** sitiari inayowakilisha nchi, na mchoro wake ni vivyo.

Kwa hiyo tunauchukulia mchoro kuwa mbinu ya kifani na inayoingiliana na maudhui pia. Hii **z** kwa kuwa maneno yanayozungumzia vitajwa au wahusika, yanazungumzia vitajwa **vile vile** **unavyoundiwa** katika mchoro. Hayazungumzii vitu vingine tofauti na mbali kabisa na **yanavyooneka** kimchoro. Ni mchoro ule ule tunaouona kwenye picha ambao unazungumziwa **na maneno kisitiari.**

Hapo hatuwezi kutupilia umuhimu wa michoro katika ujenzi wa maana. Mchoro **utakapowekwa** katika muktadha unaofaa wa kimazingira na kiwakati utaleta maana muhimu pia. Umuhimu wake usiponzwe kwa kuwa mchoro wenyewe hausemi kila kitu. Hakuna mbinu **yoyote** inayojitosha katika sanaa. Zote hutegemeana na kuchangiana ili kukamilisha maana. **K**wa mfano, maneno yaliyoteuliwa yatakuwa na maana mahususi tu iwapo yatapangiliwa **ipasavyo** kwa njia fulani, kiwakati na kutegemea muktadha pia. Sivyo yatakosa umuhimu **wake.**

Kukosa kuipata maana razini katika mchoro si udhaifu, bali ni kwamba mchoro wenyewe **huhitaji** kukamilishiwa maana kwa ung'amuzi wa mbinu zingine, k.v. mandhari. Mbinu moja

haiwezi kutoa maana kamili ya utungo mzima. Mbinu husaidiana. Mchoro husaidiana na binu zingine katika kujenga maudhui ya shairi.

4.3 MANDHARI

Kwa mujibu wa Mbatia (2001), Kamusi ya Fasihi, mandhari:

Inarejelea sura mahsus i inayojitokeza na mapambo na vifaa ... sura iliyodhamiriwa kuiga mazingira halisi yanoyozungumziwa ... sura ya mahali...

Nao Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa:

.... Ni mahali au makazi maalum yaliyojengwa na mtunzi, na mnamatukia matukio mbali mbali ya kazi ya fasihi. Ni mazingira ya wahusika pamwe na matukio, na inahusu mahali wanamokaa wahusika, na kuingiliana; mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika hao... (uk.45)

Kwa mujibu wa fasiri hizi tunachukulia mandhari kuwa hali inayozunguka matukio ya kazi ya kifasihi ambapo huwa ni mwigo wa mazingira ya kihalisa. Ni elementi inayotufichulia wapi na lini ya matukio.

Mandhari daima huathiri mkondo wa maudhui na dhamira kuu kwani hutupa msingi wa kuyatathminia (maudhui) kiwakati na/au mazingira ya utukizi, kwa misingi ya uhalisia. Yaani, kwa kuegemea uhalisikaji wake, mandhari husaidia katika usafanuzi wa maana.

Mbali na hivyo, mandhari huweza kutumika kama sitiari ya hali fulani inayomhusu mhusika au inayohusu tukio fulani. Yanaweza pia kutumika kama kihisisishi, ambapo huelezwa kwa namna inayoleta hisia fulani kwa msomaji, hisia imwelekezayo apande au kuchukia jambo au kitu fulani.

Mandhari hudhihirika kwa namna mbili: hali ilivyo kijiografia (kimazingira) na kihistoria (kiwakati). Udhahirikaji wake huu huelekezwa na katika uteuzi wa vipengele vingine vavojenga fani, kama vile msamiati, wahusika n.k.

Hivyo kwa jumla mandhari hutuelekeza kuviamini vipengele vingine vilivyoteuliwa ambapo mbali na kutupa taswira ya hali husika, hisia zetu huguswa na aina ya toni inayosawiriwa kwayo. Mandhari basi ni kielekezi cha uteuzi mwingine unaofanywa katika kuisana kazi yenye, hasa wa lugha na wahusika. Hutumika kama nguzo ya kuoanishia vipengele hivyo na maswala ya kiwakati na mazingira.

Muhimu ni kwamba, iwapo mandhari itafana na uteuzi wake uwe kidhifu, utatoa picha inayolengwa, kwa mujibu wa mawazo yaliyolengwa. Hili hufanya mandhari kuwa kipengele kikuu cha fani. Ni kipengele kinachoathiri maana na kutupa taswira ya hali-husika. Kwa hiyo ulazimishaji wa mandhari husababisha ukinzani na mawazo yaliyonuiwa na hivyo kufeli katika jukumu lake.

Pengi mtunzi hakuwa na tatizo la kuteua mandhari yake. Hii ni kwa kuwa maudhui yake ni machache tu, na hasa yanayokuza maswala ya kimsingi sana katika jamii. Kwa jumla maudhui yanayoundwa yanakuza falsafa ya utetezi.

Mandhari ya kisiasa imeteuliwa na kukuzwa kuititia masimulizi ya hali halisi pamoja na matumizi ya ujazanda na taswira anuwai. Mtunzi, katika kuiandaa mandhari haya anapigia mwengo hali halisi zilizo katika mazingira ya kienyeji barani.

Katika mandhari haya anamulika siasa ya Afrika kwa kuwazungumzia viongozi halisi k.v Obasanjo (2001: 17), P.W. Botha, (2001:2), Bokassa na Amin (2001:8) ambapo anawasifu au kuwakejeli kusudi kuwapa funzo wenzao.

Kwa kutumia mbinu ya kijazanda na taswira pevu, mtunzi, anaitalii mandhari haya kwa uhuishi anaofanyia ‘Boga’ (1997:2); ‘Nyumba’ (1997:17); ‘Konokono’ (1997:33);

Yangeyange’ (1997:41). Anavitumia vitu hivi ambavyo vinapatikana pote katika mazingira ya mtunzi ya mtunzi kuipambia mandhari yake kusudi ionekane vizuri na jamii yenewe.

Mandhari haya kwa njia hiyo inachangia vizuri katika ukusaji wa maudhui ya kisiasa. Kwa mfano, katika shairi mboga (1997:2), hadhira inachorewa picha ya tunda hilo linalopatikana mazingirani mwao. Mchoro wa boga umeonyeshwa huku umegawanywa sehemu mbili zinazotoshana kusudi kuonyesha haja ya kutekeleza usawa. Maelezo yaliyomo pia yanahimili wazo hili. Mdudu konokono anaongeleshwa na kuulizwa maswali kama kwamba yu binadamu. Kwa hakika, maswali hayo yanalengwa viongozi waroho barani. Konokono anaulizwa:

Niambie ewe konokono

Ungeligeuka mtu mithili sisi

Ukapaa hadi kitikitimu

Ungelichukua tabia ya nzige

Ukala na watoto wako

Bila kujali umati

Upigao miayo chini ya ngazi?... (uk.33)

Kiumbo hiki cha kutoridhishwa na hali ilivyo, na kinachoendelezwa na kuuliza maswali, kinaonekana pia katika ‘Swali kwa Yangeyange’ (1997: 41) na pia katika ‘Maswali kwa Mdudu’ (1997: 51).

Kimsingi mandhari ya kisiasa imelengwa kufahamisha watawala kuwa inawabidi kutekeleza haki; na vile vile kukebehi tabia zao zisizovutia. Huu ni ujengaji wa maudhui yenewe ya kisiasa. Hata hivyo, hali ya kuwa mtunzi hakuizungumzia siasa ya jamii kwa upana wake, inaonyesha upujuaji wa thamani ya mandhari hayo. Mtunzi ameifunga mandhari hiyo kwenye maswala finyu tu, hasa ya unyanyasaji na unafiki. Kwa jumla mandhari haya haikutaliwa vya kutosha katika diwani hizi.

Mtunzi, hali kadhalika, amekita maudhui hii kwenye uwanda wa kiwakati kuanzia hasa kipindi baada ya uhuru barani. Viongozi wanaotajwa ni wa enzi hii. Hili pia linaonekana katika shairi

'Jumapili ya Damu' (2001:6); lizungumziale jaribio la mapinduzi nchini Kenya mnamo Agosti 2,1982.

Katika kukuza maudhui ya kitamaduni, mtunzi amejenga mandhari inayoonyesha mtanziko reina ya thamani za kienyeji na zile za kigeni. Hali inayotawala maudhui haya yanaonyesha winganishaji wa thamani hizi mbili. Humu, vile vya kiasili vinatengwa na vile vya kigeni, ambavyo mtunzi haonekani kuvithamini. Katika shairi 'Ngoi na Waimbaji' (2001:51) mwandishi anaonyesha umuhimu wa kile cha kiasili huku akitweza vile vya kigeni. Anaonyesha usawiri wa mandhari ya mtanziko huo kwa mishororo k.v:

Sijali, kwa nini nijali
Wenye nyoyo na mbawa za kumandari
Wakifurahia vilele vya theluji...
Wakifurahia vito vya maji na pori....
Viboko vaizi vikuu vinavyotembea
Simba watawala mwitu
Heroe darizi za maziwa....(uk.51)

Kisha:

Najali sana najali
Najali watoto wa kike
Wakikanda miili ufukweni
Ili nchi ivune miili yeni na krona....
Tunajali taifa kugeuzwa pipa
La kupokea uoza wa ulimwengu
Ili nchi ivune dola na fauni. (uk.53)

Hapa mwandishi anaonyesha hali ya kuthamini kile chao, cha kienyeji. Haya mandhari yanatumiwa kuhimilia maudhui ya uasilia. Mashairi mengine yanayokita kwenye mandhari haya ni kama vile 'Mwashi Mahiri' (2001:45) na 'Tiba' (2001:47). Mandhari haya pia imehimiliwa kwa msamiati unaoashiria uasilia wa kienyeji na msamiati wa kigeni pia. Mfano: asali, viazi vikuu; nyeni, dola, lira n.k

Maoni yetu hapa ni kwamba maswala yanayoendelezwa katika mandhari haya yangesawazishwa kwa kiwango fulani. Mtunzi, mbali na kutukuza kile cha kiasili tu, angetokea kuonyesha jinsi usasa unavyozidi kunata katika jamii. Angeonyesha pia udhaifu ambao tayari unajitokeza katika utamaduni wa jamii yake, huku akiangaza unakofaa usasa na thamani mpya za kigeni. Aghalabu angeonyesha ulinganishaji usiolenga kuendekeza utamaduni mkongwe tu.

Kuna pia mandhari ya uharabu dhidi ya mazingira ambayo yanawasiri tabia ya ufujaji wa mali asili. Mandhari haya inajengwa kwa mujibu wa utetezi wa mazingira, na mali asili, ambayo yanapujuliwa aghalabu na tabia ya mwanadamu ya kutojali thamani yake. Vihasiriwa hapa vinapewa nafasi ya kujitetea kwa vinywa vyao ambapo miti, mito, mabwawa n.k. vinahuishwa na mtunzi.

Shairi ‘Mimi, Mto Nairobi’ (2001:63) linaonyesha mandhari haya kwa kusawiri jinsi mto huu unavyodhulumiwa na jirani zake. Mto unalalamika:

Ubeti 2

Wenda –wazimu!
Wananiangamizi
Mimi ambaye
Kwa moyo mkunjufu
Niliwakaribisha....(uk. 63)

Mandhari haya pia yanatokea katika mashairi k.v ‘Thagicu’ (2001:61), ‘Okidi, Piga Ukelele’ (2001:64), ‘Mikoma’ (2001:66).

Mandhari ya aina hii yanahimiliwa kwa utajaji wa miti fulani, mabwawa, mito, n.k. Pamoja nayo, kuna pia msamiati mkali unaoashiria tabia ya uharibifu na maonevu kama vile; “shambulia”, “Vami” (“Mbiu ya Mgambo” :uk.41); “dhara”, “muuaji”, (“Mwashi Mahiri”:45),

"wanikaba koo", "wananiziba pumzi", "wananinyonga", "wananiangamiza" ('Mimi, Mto Nairobi':63), "makaburi", "wanashambuliwa kwa mapanga", "maangamizi" ('Mikoma' uk.66)

Mandhari haya yanasaidia sana katika ujenzi wa maudhui ya utamaduni kwani vipengele vinavyoijenga havitalikiani na hali ya kienyeji ya jamii ya mtunzi. Japo kuna mashairi machache yanayokita kwenye mandhari haya, matumizi ya mandhari yenewe hayakupwaya.

Mandhari ya jamii iliyopuja maadili ya kijamii inajitokeza pia katika tungo hizi. Taasubi ya kiume inayoleta dhuluma dhidi ya wasichana wachanga inajenga mandhari haya. Tunaona hali ya uingiliaji na udungaji mimba wasichana wachanga na wanaume tusioona wakiadhibiwa na jamii.

Katika 'Pamela' (2001:29) tunaandaliwa mandhari haya kwa kuangaziwa jinsi Pamela alivyonajisiwa na genge la wanaume waliolewa 'pombe na moshi leweshi'. Mwalimu-mkuu katika 'Flora na wenzake' (2001: 33) anasawiriwa kuwa mtu aliyeoza na mviziaji mfano wa mburukenge; na nduli kama vile 'risasi' kutoka kwa mtutu, anayewalenga wasichana wasiopevuka. Katika 'Giza Mbele' (2001:26) Ukosaji huu wa maadili unaonyeshwa kwa:

Mkono mkongwe kama karne....

Taratibu unaaza mwendo...

Hadi maeneo ya mbali,

Katika akili ya moto

Wasiwasi unatanda...(uk.27)

Katika ' Flora na Wenzake' (2001:33) hali hii inaangazwa na:

Vidole bila adabu

Na ngozi changa

Zinakutana ghafla

Na kuchanganyika

Chini ya sare ya shule... (uk.34)

Katika shairi hili tunaobna pia hali ya ukosaji maadili kupitia kwa mwalimu "Uoza" ambaye kuondoka kwake nyumbani ni kama "kufyatuka kwa risasi" dhidi ya wasichana wa shule.

Mandhari haya ya upujuaji wa maadili inahimiliwa pia na matumizi ya watusika wanaokifupi hali hiyo. Hawa ni kama vile 'Mzee wa benzi', Pamela, askari, mzee mwenye upara kwa upande mmoja na wasichana wachanga kwa upande mwingine. Usafanuzi wa watusika hawa na matendo yao pia unatumia msamati unasaadia sana katika usawiri wa mandhari haya. Hii mandhari inafana sana katika ujenzi wa maudhui ya 'dhuluma ya kimpenzi' dhidi ya wasichana.

Hata hivyo, pengi mtunzi hakuikuza kazi yake kuonyesha mshawasha wa baadhi ya matendo. Angezamia zaidi kuonyesha hali za kijamii zinazowavuta watusika kwenye matendo yao maovu. Hili lingethamini zaidi msingi wa mandhari zinazojengwa

4.4 TONI

Toni katika kazi ya kifasihi hulenga usununu na msimamo wą mwandishi unaodhiihirika katika kiimbo cha sauti yake au uteuzi wa vipengele mbali mbali vya kimaelezo katika kazi yenye.

Roberts (k.h.j.) anaeleza kuwa toni ni:

... mbinu ambayo kwayo washairi hudhibiti msimamo na hisia ... (uk. 654)

(Tafsiri yetu)

Myers (k.h.j.) anaandika kuwa ni:

... msimamo unaoweza kutambuliwa wa mwandishi kuhusu
hadhira yake.... usununu wa kazi ya kifasihi.

Tunaona hapa kwamba waandishi hawa wanegemea kusisitiza msimamo na usununu unaoidhiihirikia hadhira kutoka kwa mtunzi.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa toni imefungamana kwa kiasi kikubwa na maswala anayozungumzia mshairi. Hivi ni kwamba sauti ya utoaji wake huathiri dhamira yake kwa

kiwango kikubwa. Kwa hivyo, toni hujengwa na kufanikishwa na matumizi ya kunga anuwai za kifani k.v muundo wa kazi, uteuzi, taswira, chuku n.k. Uteuzi wa msamiati mzito na mkali, kwa mfano, huweza kuonyesha upinzani, utetezi au tahadhari. Haya yote huathiri ukuzaji wa maudhui kwa jinsi yanavyowafikia waliolengwa.

Toni inayojitokeza katika diwani hizi ni kali inayolenga kukuza sauti ya utetezi. Mtunzi amesawiri mandhari ya kimazingira na uasilia unaopujuliwa pamoja na unyanyasaji wa kisiasa. Katika kukosoa hali hizi, imebidi atue kwa makini sana vipengele vya kifani vinavyoisawiri na kukebehi hali hiyo.

Uteuzi wa msamiati, mipangilio pamoja na mandhari ya tungo zenyewe ni mambo ambayo yametuashiria barabara usununu na msimamo wa mtunzi kuhusiana na hali ilivyo. Misimamo hii inajitokeza kupitia toni zenyе mshabaha ki malengo katika mashairi tofauti tofauti.

Mengi ya mashairi yanajumuisha msamiati unoibua hisia na kusimua. Mandhari yaliyoteuliwa ni ya kihalisi na ya karibu na msomaji. Matumizi ya msamiati wenye nguvu katika mandhari haya ya kihalisi ni suala linalozua toni hisivu inayomwathiri msomaji kwa jinsi atakavyopokea ujumbe uliolengwa.

Tutachunguza toni katika mashairi tutakayoteua katika kila maudhui huku tukiilinganisha na inayotoka katika mashairi mengine yanayokuza maudhui hayo hayo.

Katika ukuzaji wa maudhui ya kisiasa shairi 'Bara Jingine' (2001:10) linaashiria toni ya matumaini katika hali kugeuka kutoka kwenye uozo ilimojizamisha bara. Msimalizi, japo anaeleza hali mbaya iliyopo barani, anaeleza juu ya ndoto yake yenyе kutumainisha. Pamoja na kutumainisha, mshairi anaeleza kwa kiimbo chenyе masikitiko juu ya hali duni iliyopo barani. Anazungumzia matendo maovu yaliyokithiri barani kama vile ulafi, ufisadi, utengano, n.k; maafa ambayo yanaendelezwa na viongozi waovu.

Hatimaye, kwa jumla tunaweza kutambua kuwa hamu ya mwandishi ni kuonyesha uwezekano wa hali hi kugeuka. Hili ni kuitia ukariri wake wa 'ndoto' yake. Kuna pia mwendelezo wa mawazo kwa kauli ya ukanushi dhidi ya matendo maovu yanayooodheshwa. Shairi 'Bara Jingine' limesheheni kauli k.v.

Bara ambapo

Bunge

Halitakuwa....

"Usalama wa taifa"

hautakuwa...

Ulafi

Na ufisadi

Hazitanyesha kutoka juu...

Katika Ikulu

Hakutapinda mamba...(uk. 10-11)

Hatimaye anaeleza kwa kauli yakinifu mambo mapya na mema ambayo yatalidhibiti bara, pindi ndoto yake itakapotimia. Anaeleza kuwa:

Kama chozi

Juu ya ua...

Ndoto yangu

Imetua na kutulia

Juu ya bara jipya

Bara ambapo...

Tekinolojia ya habari

Haitabakia juu angani...

Wakulima

Wataimba nyimbo...

Kusifia ukunjufu(uk.11-13)

Mishororo hii inaonyesha kuwa msimamo na matamano ya mtunzi ni kwamba hali mbaya iliyopo itabadilika. Hili linawekwa wazi na uteuzi wake wa kauli kama tulivyoonyesha hapo juu. Kwamba ana msimamo unaolenga hali ya kugeuka ni swala linalotuangazia kuwa kuna

hali ya unyanyasaji katika jamii. Hivyo, mandhari haya yanahimili mwendelezo wa maudhui ya kisiasa.

Toni ya aina hii pia inadhihirika katika mashairi k.v. ‘Amba’ (1997:15); ‘Papa’ (1997:45); ‘Kamba na jabali’ (2001:3); ‘Hatutaaga ndoto’ (2001:4). Ukariri wa neno “ndoto” katika mashairi mengi pia unaendeleza toni hii.

Yote haya ni kuunda toni ya kutumainisha dhidi ya hali iliyopo, na husaidia katika uendelezaji wa maudhui ya kisiasa.

Kuna pia toni ya kukejeli ambapo mashairi mengi yanaonyesha hali ya mtunzi kutopendezwa na hali iliyopo ya mambo, hasa uongozi mbaya na uharibifu wa mazingira. Toni hii inadhihirika hasa katika mashairi yanayouliza maswali ya balagha. Kwa mfano, maswali kama hayo yanatokea katika: ‘Maswali kwa Mdudu’ (1997:51), ‘Kikaoni Addis Ababa’ (2001:2); ‘Swali kwa Yangeyange’ (1997:41) ‘Swali kwa Konokono’ (1997:33). Katika ‘Swali kwa Yangeyange’ (k.h.j.) mshairi anasema:

Ungelifikia hicho kidato
Ungelimea pembe kama kifaru
Ukanyanya kwa kutonga...? (uk.41)

Maswali kama haya yanatashtitia hali ya watawala waovu na hivyo kuuweka wazi msimamo wa mwandishi. Huu ni mwendelezo wa maudhui ya kisiasa kupitia huo uchochezi wa kiimbo chenyewe.

Kuhusu mengi ya mashairi yanayokuza maudhui ya ‘dhuluma ya kimapenzi’ mtunzi anabaini toni ya kuchukizwa na kukashifu. Anayakuza maudhui haya kwa msimamo wazi kuwa tendo hilo si zuri na linakera.

Katika shairi ‘Pamela’ (2001:29) mtunzi anateua msamiati mkali unaoibua hisia kwa kusudi la kuonyesha kutoyutiwa kwa tendo hilo. Anawafananisha wavamizi wa Pamela na ‘mbwa –

mwitu'. Katika 'Flora na Wenzake' (2001:33) anamfananisha mwalimu mkuu (anayewavizia wasichana) na Mburukenge, risasi. Katika 'Giza Mbele' (2001:27) gari la mnasaji (lile benzi la mzee) linalinganishwa na 'Chatu'. Pia kauli kama vile "mja -mzito-mtoto", "kutojua akilini" zinasisimua hadhira na kuonyesha jinsi tendo lenyewe linavyomgusa mtunzi. Anaashiria shutuma dhidi ya tendo lenyewe.

Maudhui ya mazingira yanaendelezwa kwa toni yenye kuonyesha huzuni, masikitiko na malalamiko. Toni ya huzuni inatokea pale mtunzi anapotueleza hali ya kusikitisha ya mto 'Thagicu' ambapo anasema:

Macho yangu
Yanapoona hayo mabonde ambayo
Yamejaa mchanga mweupe
Akili yangu
Huona vidonda virefu....(2001:61)

Kiimbo hicho kinaendelezwa katika 'Mimi', Mto Nairobi, ambapo kuna masimulizi ya mto unavyoteswa na majirani zake. Unasema:

Wakazi wa jiji
Wananikaba koo
Wananiziba pumzi
Wananinyonga ... (uk. 63)

Msamiati wake pia unasikitisha na kuonyesha huzuni anayotaka kuibua mtunzi, na aliyo nayo.

Hali kama hiyo pia inatokea katika shairi 'Bwawa la Ithanje' (2001:69) kwa:

La! Usife! Ithanje Usife!
Kwani kifo chako
Hakitakuwa chako pekee
Kitakuwa cha familia kubwa... (uk. 69)

Matumizi ya nidaa (!) yanaonyesha mchomo wa moyo, na hivyo huzuni aliyonao mtunzi. Pengi masimulizi ya wahusika hawa yanaibua toni ya malalamiko. Kiimbo hiki kinahimili utetezi wa mazingira, na huu ni mwendelezo wa maudhui yenye, ya mazingira.

Toni ya kuvihimiza inatawala mashairi yanayogusia uasilia. Mengi yake yamesheheni utiaji shime kwa wahusika wanaoyaendeleza maudhui. Mtunzi mara nyingi anawatetea, kuwasifu au kuwachochea wadumishe mapambano. Katika ‘Mwashi Mahiri’ (2001:46), mtunzi analichochea titi lizidi kupigana na hapo hapo kulitolea sifa nzuri nzuri. Analambia titi:

Pigana, Titi pigana!...

Pigana wewe mwashi mahiri

Ujengaye miili thabiti...(uk.46)

Katika shairi ‘Tiba’ anavihimili vivyo hivyo vilivyo vyakienyeji vidumu katika mapambano kote barani. Anasema:

Jikakamue, wewe Tiba

Pigana kote Afrika

Usichoke, wewe jabari ambaye

Unaangusha chini adui (uk. 47)

Matumizi ya mbinu ya tashhisi pia yanahimili sana toni ya mwandishi kwani ni ishara ya kuvithamini sana anavyovihuisha. Kwa kuvihimiza vilivyo vyakienyeji vidumu katika mapambano maudhui hii ya uasilia, kwa mwelekeo wa kuuthamini uasilia wenywewe.

Aghalabu, uteuzi wa msamiati unafanikisha sana ubainishaji wa toni ya mwandishi. Mbinu ya tashhisi pia inatumika pengi na inashadidia msimamo wa mwandishi kuyahuusu maswala pamoja na wahusika wanaoyajenga maudhui yake.

Hata hivyo mtunzi ana uziada wa kukuza msimamo hasi kuhusu vitu au mambo mengi katika jamii yake. Pengi usununu wake unaonyesha kwa malalamiko na kuteta dhidi ya hali iliyopo. Ingefaa zaidi kuchanganya msimamo wa aina hii na kiimbo chenye upole zaidi kilicholengwa kuikosoa jamii.

Pamoja na hayo mbinu ya kipekee ya kutumia picha au sitiari ya kimchoro ni mashuhuri humu, katika kutolea usununu na hisia za mtunzi. Mbinu ya kiuoni inakuza na kushadidia maana na

thamani ya kinachozungumziwa. Hili huonyesha udhati anaohusisha na maswala anayosughulikia mwandishi.

4.5 HITIMISHO

Katika sura hii tumechunguza vipengele mbali mbali vya kifani ziada ya vile vya kilugha na mchango wake katika ukuzaji wa maudhui. Tumeainisha mchango wa sitiari ya kimchoro, mandhari na toni. Tumeonyesha jinsi vipengele hivi vinavyokamilishana na mbinu za kilugha katika uendelezaji wa maudhui.

Imedhihirika kuwa hakuna mbinu moja inayoweza kuleta fahiwa kamilifu bila kutegemea zile nyingine. Kwa mfano, tumetambua kuwa sitiari ya kimchoro huwakilisha hatua ya kimsingi ya ung'amuaji wa maana, na hii ni taashira ya kiuono ya yale yanayoelezwa kwa maneno

Sitiari hii hupiga mwengo yale yanayoelezwa kwa maneno japo aghalabu humulika fahiwa ya kijuu juu tu. Hufanikiwa vizuri zaidi inapooanishwa vyema na muktadha wa kiusimulizi. **Mbinu zote hizi hutegemeana sana.**

Imebainika kuwa, kwa kiasi kikubwa, mbinu zote hizi huzitegemea zile za kilugha ndiposa ziweze kujengeka. Nazo huhimili sana msingi wa kujenga maudhui. Hivi ni vipengele ambavyo hujumuisha mseto wa mbinu nyingine. Ni tukio la uteuzi, upangiliaji na mwingiliano wa mbinu na vipengele vingine.

Hata hivyo, tumeona kuwa uendelezaji finyu wa maudhui huweza kupujua ufanifu wa mbinu zenyewe. Iwapo maudhui hayatatamba uwanda mzima unaodhibitiwa na mbinu hizi uteuzi wake basi utapwaya. Hali hii imedhihirika katika baadhi ya maudhui kama vile ya siasa, utamaduni na pia dhuluma ya kimpenzi.

Jumla ya vipengele hivi vinaonyesha uhalisi mkuu katika ukuzwaji wake kwani uteuzi wake una mshabaha mkubwa na hali ya mambo barani. Kwa hiyo vyote vinaoana vyema katika kutekeleza wajibu mmoja wa kuyakuza maudhui, ambayo pia yanailenga jamii ya kihuku.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 HITIMISHO

Katika tasnifu hii tumechunguza mwingiliano wa fani na maudhui katika diwani za Kithaka wa Mberia za Mchezo wa Karata na Bara Jingine. Kwa kuegemea nadharia ya Umuundo na kisosholojia tumeonyesha umuhimu wa vipengele vya kifani pamoja na athari za kimazingira katika kujenga fahiwa katika kazi za kifasihi.

Katika sura ya pili tumetalii historia ya uzukaji wa ushairi huru katika ushairi wa Kiswahili. Hapa tumeviainisha vipengele vikuu kama njia ya kusisitiza utalikiano wake na kaida zilizofuatwa na ushairi wa kimapokeo. Tumeonyesha jinsi mabadiliko ya kijamii, hasa baada ya uhuru wa kisiasa yalivyochochea uibukaji wa mtindo huu mpya wa kuyaandika mashairi. Tumbainisha kuwa mgeuko wa hali ya kisiasa ulizua awamu mpya ya ufikiriaji mionganini mwa jamii, hali ambayo pia iliwaathiri washairi. Kuzuka kwa maswala mapya ya kushughulikiwa na watanzi pia kulichagizauzuaji wa mbinu mpya za kuyawasilishia mawazo mapya. Imedhihirika pia kuwa mwingiliano na elimu ya kimaghari bu ulikuwa na taathira katika watanzi hawa wapya.

Kauli za baadhi ya waandishi zimetuelekeza kwenye maamuzi kuwa mkabala fulani wa kimawazo huwa daima una njia bora zaidi ya kuuwakilisha. Dhamira mbali mbali huwa na mbinu tofauti tofauti za kuzifikia. Kwa mfano, ushairi huu mpya uliolenga maswala yenye unyeti wa kisiasa pamoja na ukosoaji wa jamii ulihitaji pia taratibu mpya za kuufanikisha. Kila kiimbo huwa na fani yake mwafaka ya kukiwasilishia. Tumeona kuwa katika kuwasilishia kiimbo cha kupigia tashtiti upotevu wa jamii yake, Mberia amepiga hatua za kuteua mbinu mpya za kifani. Hili linatosheleza hamu ya makisio yetu kuwa uteuzi wa vipengele vya kifani una mchango mkubwa katika kuyaunda maudhui yaliyolengwa. Kwa mfano, tumeona jinsi vipengele kama vile uteuzi wa kimandhari na pia sitiari za kimchoro unavyochangia

udhihirishaji wa maudhui. Amevitumia kama nyenzo hisishi zaidi kuyaendeleza maswala nyeti ya kisiasa na pia kupigia tashtiti upotevu kwa jumla.

Katika kuyaainisha maudhui katika sura ya tatu kwa jinsi yalivyojengwa na vipengele veya kifani, tumeona kuwa yana msingi wake katika jamii ya wakati wake. Uteuzi wa vipengele veya kifani pia una mshabaha mkubwa na mandhari ya kijamii. Haukutalikiana pia na mandhari ya kiasili. Mbinu za kifani zimejenga ufasaha wake wa kiunasibishi kutoka mazingira ya mwandishi. Kwa mfano, uteuzi wa msamiatu wake umewiana na hali halisi inayoshuhudiwa katika jamii ya mtunzi. Hali hii inazikutanisha vyema nadharia zetu za kihakiki. Hii ni kwa kuangalia jinsi uteuzi wa maudhui pamoja na vipengele veya kifani unavyowiana na mazingira ya kijamii.

Kuhusu sitiari za kimchoro, imebainika katika sura ya nne kuwa matumizi ya 'picha' yanatoa mwelekeo muhimu katika ufasili wa maana. Tumeona kuwa tunachokiona katika mchoro hakiwezi kutenganishwa na yale yanayoelezwa kuititia maneno ya mtunzi. Imebainika kuwa matumizi ya mbinu hii katika ushairi wa Mberia ni tofauti na ule ushairi wa kimaumbo uliodhibiti tungo za Ulaya katika karne ya kumi na saba ambaao uliyaumba mashairi yake katika maumbo ya kimraba, duara, nyota, nk. Maumbo hayo yutmkini hayakuwa na uhusiano wowote na yaliyomo. Umichoro uliomo katika diwanı hizi ni tofauti, una usitiari ndani yake. Mbinu hii imetokea kwa uwazi zaidi katika mashairi ya 'Boga' (1997:2); 'Nyumba' (1997:17) na 'Mwashi Mahiri' (2001:45). Inasaidia sana, kwa kusaidiana na mbinu nyingine, katika kujenga taswira amazonuia mtunzi.

Kwa jumla, mambo mawili ya kimsingi yanajitokeza katika diwani hizi. Kwanza, zote zinafuata mkondo wa ushairi huru uliopiga hatua ya kipekee. Pamoja na kutofuata arudhi za kikale, mtunzi amezua mbinu ngeni ya kuyaandika mashairi huru. Hii ni ya sitiari ya kimchoro, ambayo ni mchango mpya katika ushairi wa Kiswahili. Huu si upotoshi mbali ni hatua ya kimaendeleo. Utukizi wa mashairi huru si kioja bali ni hoja katika ukuaji wa ushairi. Unakuza

matumizi ya hisi nyingine katika kuyatalii mashairi, hisi ya maono mbali na usomaji tu. Japo matumizi yake yanaashiria kuathiriwa kwa mtunzi na usomaji wa ushairi wa kwingineko, huu si udhaifu. Nadharia ya kisosholojia hutambua kuathirika kwa mwandishi na mazingira yake, yawe ya kihalisi au ya kielimu. Nayo nadharia ya Umuundo inathamini uzuaji wa maana kutokana na mchango wa miundo na upangiliaji wa kazi. Kwa hiyo, kauli kuwa umichoro unaathiri uelewa ina mashiko.

Hali kadhalika, imebainika kuwa mtunzi ameteua aghalabu pmaudhui ya kiutetezi tu, ambayo yamejengwa kwa uteuzi uliojikita kwenye mazingira yake halisi. Hana maswala ya kidhahania. Anajishughulisha na hali halisi katika jamii yake ambapo anayaendeleza maswala yake kwa kiimbo kikali cha manung'uniko na utetezi. Hata hivyo, ye ye ameufinyaza mkabala wake kwenye maswala machache tu ambayo huenda ndiyo yaliyomchachiza. Hakuishughulikia hali ya jamii kwa ujumla wake. Kwa mfano, hakutamba kwenye maswala kama vile ya kielimu, biashara au vita. Amelishughulikia kwa ufinyu sana swala la unyumba au mapenzi. Analozamia zaidi ni swala la siasa tu, ambapo ameshughulikia kwa kina vipengele fulani vyake. Haya ndiyo maudhui yanayotawala diwani nzima ya Mchezo wa Karata.

Kwa hali ya kuwa hatukunuia kutathmini upeo na kina cha maudhui, wala fani, tumeridhika kuwa uteuzi wa maudhui machache yanayojitokeza umeonyesha mshikamano mkuu na fani yake. Uteuzi wa vipengele vyote hivi una mshabaha na mazingira halisi ya jamii ya mtunzi.

5.2 MAPENDEKEZO

Katika utafiti wetu, tumelenga hasa kuchunguza mwingiliano wa vipengele vyta kifasihi vinavyojitokeza. Hatukupiga mbizi kutathmini kina na ufanifu wa kila kimojawapo katika upekee wake. Tahakiki za baadaye zinaweza kushughulikia kina na kiwango cha fani au maudhui bila ya kutathmini viwango vyta maingiliano yake. Utafiti mahsus ikuhusu fani au maudhui unaweza kufanya pia kwa kuegemea misingi tofauti ya kinadharia.

Hali kadhalika, tahakiki za baadaye zinaweza kuzitathmini diwani hizi kwa kuzilinganisha na kazi za watunzi wengine na hapo kutoa hukumu kuhusu usanifu wake kwa misingi ya kishairi huru.

Lingekuwa jambo la busara pia kuzitathmini diwani hizi mbili kiulinganishi. Tunapendekeza uchanganuzi wa aina hiyo ufanywe ili kuweka wazi mshabaha na kuhitilafiana kwake. Hii itakuwa njia mwafaka ya kupimia falsafa na mtindo wa huyu mshairi mpya.

Aidha tunapendekeza utafiti wenye kina zaidi ufanyiwe mbinu yake mpya ya 'umichoro' kusudi kutoa mahitimisho makinifu kuhusu nafasi yake katika ushairi wa Kiswahili kwa siku zijazo.

Kwa sababu ya muda mfupi tuliokuwa nao pamoja na ukosefu wa tahakiki zenye kina kuhusu kazi zake, hatungeweza kufanya ziada ya tulilofanya.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M.H. (1979) Muyaka: 19th centrury swahili popular poetry, Nairobi, KLB.
- Abedi, A.K. (1954) Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri, Nairobi. KLB
- Abiud, N.N. (1998) Utetezi wa Haki za Wanyonge Katika Diwani ya Mchezo wa Karata (1997)', Tasnifu ya B.Ed.
- Arege, T.I.M (1998) 'Ushairi Huru wa Kiswahili: Mchango Wa Euphrase Kezilahabi', Tasnifu ya Uzamili – Haijachapishwa.
- Cohen, J.M (1960) Poetry of Resistance. London, Hutchinson & Co.Ltd.
- Cuddon, J.A. (1979) A Dictionary of Literary Terms. London, Andre Deustch Ltd.
- Culler, J. (1975) Structuralist Poetics: Structuralism Linguistics and the study of literature, Newyork, Cornell University Press.
- Diyyani, R (1994) Literature: Reading, Fiction, Poetry, Drama & The Essay, Newyork, McGraw- Hill, Inc.
- Fekete, J (1977) The Critical Twilight, London, Routledge and Kegan Paul Limited
- Fowler, R (1975) Style and Structure in Literature, Oxford, Basil Blackwell
- Gachukia, E.W. (1980) 'Cultural Conflict in East African Literature', Ph.D Thesis- Unpublished.
- Gill, R. (1985) Mastering English Literature, London, Mac Millan Press Ltd.
- Gromov, M.D. (2001) Mazungumzo ya Fasihi, Moscow, Humanite Publishing.

- Harries, L. (1962) Swahili Poetry. Oxford, Clarendon Press.
- Hawkes, T. (1977) Structuralism of Poetics, London, Methuen and Co. Limited.
- Hornby, A.S. (1989) Oxford Advanced Learners' Dictionary, Newyork, Oxford Univ. Press.
- Inyani, S.K. (2002) Utafiti wa Kiswahili, Nairobi, Downtown Printing Works Ltd.
- Johnson, F. (1973) A Standard English –Swahili Dictionary, Nairobi, UOP.
- Kahigi, K. na Mulokozi, M. (1976) Malenga wa Bara, Nairobi, EALB.
- _____ (1979) Kunga za Ushairi na Diwani Yetu, Dar es Salaam, Tanzania Publishing House.
- Kazungu, E.K (1982) 'Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Texts', Masters Thesis – Unpublished
- Kezilahabi, E. (1974) Kichomi, Nairobi, Heinemann.
- _____ (1976) Ushairi wa Shaaban Robert, Nairobi, EALB
- _____ (1988) Karibu Ndani, Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press.
- Kitsao, J. (1982) 'An Investigation of Themes in Swahili Literature & Application of Stylostatistics to Chosen Texts', Ph.D Thesis – Unpublished
- Knappert, J. (1972) An Anthology of Swahili Love Poetry, California, Berkeley Uni. of California Press.
- Lambert, H.E. (1971) Diwani ya Lambert, Nairobi, EALB
- Levin, S.R. (1969) Linguistic Structure in Poetry, The Hague, Mouton and Co.

Printers.

- Makkai, A (ed.1976) Towards a Theory of Context in Linguistics and Literature.
Paris, Mouton and Co. N.B. Publishers.
- Masoko, D. na mdee, J.S. (1984) Mulika (16) Dar es Salaam, TUKI
- Massamba, D.P.B (1976) Diwani ya Massamba, Middlesex, Thomas Nelson & Sons Ltd.
- Mayoka, J..M. (1986) Mgororo wa Ushairi na Diwani ya Mavoka, Dar es Salaam, TPH
- Mazrui, A (1988) Chembe cha Moyo, Nairobi, EAEP.
- Mbatia, A.M. (1999) 'The Origin and Development of the Swahili Thesis Novel in Tanzania', Ph.D. Thesis – Unpublished
- _____ (2001) Kamusi ya Fasihi, Nairobi, standard TextBooks Graphic & Publishing
- Mberia, K. (1997) Mchezo wa Karata, Nairobi, Marimba Publishing Company
- _____ (2001) Bara Jingine Nairobi, Marimba Publishing Company
- Mdee, J.S. (1986) Kiswahili Muundo wa Matumizi yake, Nairobi, Intecontinental Publishers Ltd.
- Mnyampala, M.E. (1965) Waadhi wa Ushairi, Nairobi, EALB
- _____ (1971) Diwani ya Mnyampala, Nairobi, EALB
- Mohamed, S.A.M (1995) Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthlia, na Hadithi Fupi, Nairobi, EAEP.
- Mohammed, M. (1977) Malenga wa Mrima, Dar es Salaam, Oxford University Press.
- Msokile, M. (1993) Misingi ya Uhakiki wa Fasihi, Nairobi EAEP

- Musau, P. (1985) 'Euphrase Kezilahabi: Mwandishi Aliyekata Tamaa'. Tasnifu ya Uzamili - Haijapishwa.
- Musyoka, F. M. (1996) 'Uhakiki wa Fani Katika Tamthilia za Jay Kitsao', Tasnifu ya Uzamili – Haijachapishwa
- Mutiso, K. (1986) Mizani Yangu, Nairobi, KLB
- Mwai, W. (1982) 'New Trends in Ushairi', Masters Thesis – Unpublished
- Myers, J. (1989) The Longman Dictionary of Poetic Terms, Newyork, Longman.
- Nassir, A. (1982) Taa ya Umalenga, Nairobi, KLB
- Newmeyer, F.J. (1986) Linguistic Theory in America, London, Academic Press Inc.
- Njogu, K. et al (1999) Ufundishaji Wa Fasihi: Nadharia na Mbinu, Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.
- Osiemo, D.O. (1997) 'Fani Katika Ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa Upisho wa Umalenga na Dafina ya Umalenga', Tasnifu ya Uzamili – Haijachapishwa
- Pottle, F.A. (1963) The Idiom of Poetry, Bloomington, Indiana University press.
- Preminger, A. (1979) Princeton Encyclopaedia of Poetry and Poetics, London, Macmillan Press Ltd.
- Robert, S. (1968) Kielezo cha Fasili, Dar es Saalam, Nelson & Sons Ltd
- _____ (1968) Siku ya Watenzi Wote, Nairobi, Evans brothers (k) ltd.
- _____ (1968) Utubora Mkulima, Nairobi, Evans Brothers (K) Ltd.
- Roberts E.V. (1992) Literature: An Introduction to Reading and Writing.

Englewood Cliffs, Prentice Hall.

- Roberts, M. (1960) The Faber Book of Modern Verse, London, Faber & Faber Ltd.
- Senkoro, F.E.M.K (1982) Fasihi, Dar es Salaam. Press & Publicity centre.
- Thompson, D. (1974) The Users of Poetry, Cambridge, C.U.P
- TUKI, (1983) Mulika Kioo cha Lugha, Dar es Salaam.
- Vuzo, A.M. (1986) Mwongozo wa Mashairi Yetu, Nairobi, Heinemann, Kenya.
- Wamitila, K.W. (2002) Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake, Nairobi, Phoenix Publishers.
- _____ (2003) Kichocheo cha Fasihi, Misingi na Vipengele vyake, Nairobi, Phoenix Publishers.